

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Tatu – Tarehe 2 Februari, 2012

(Kikao Kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, leo mtihani mwingine hapa, walioamka saa kumi na moja asubuhi kuja kuomba kumwuliza Waziri Mkuu ni Wabunge 26 na wanaotakiwa ni Wabunge nane tu kwa muda tulionao. Kwa hiyo, tutakachokifanya hata kama wengine waliwahi, nitahakikisha kwamba angalau kila Chama kinawakilishwa humu ndani. Kwa hiyo, wengine wengi itabidi niwaombe msamaha, hakuna namna ya kufanya.

Leo Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa kuwa hayupo tunaanza moja kwa moja na Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika ahsante.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa uchumi wa nchi umeharibika sana hasa kwa wananchi wa kawaida. Kwa kuwa, tunauza bidhaa kidogo ambazo zinatupa hela za kigeni chache na tunanunua bidhaa nyingi ambazo tunatumia pesa nyingi za kigeni.

Je, Serikali ina mkakati gani kabambe kuokoa tatizo hili ambalo linawafanya wananchi wa kawaida washindwe kununua bidhaa muhimu, mfano sukari na bidhaa nyingine kwa sababu ya kukosa fedha? *(Makofi)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane tu na Mheshimiwa Diana Chilolo kwamba Taifa linapita katika mtikisiko mkubwa wa hali ya uchumi ambao kwa kweli unatokana na mambo mengi, ndani yake ikiwemo mfumuko wa bei ambao ndiyo unachangia kwa sehemu kubwa sana katika kufanya maisha ya Watanzania kuwa magumu. Lakini mfumuko wa bei nao una sura nyingi, kwa sababu upo ambao unasababishwa na bei kubwa kwa upande wa chakula, lakini vile vile mafuta kwa sababu tunaagiza mafuta mengi kutoka nchi za nje na bei zake hazijashuka kwa kiasi kikubwa, lakini zipo sababu zingine nyingi tu zinazohusiana na jambo hili. Kwa maana ya mkakati kabambe katika mazingira tuliyonayo, kubwa ni Watanzania kutambua kwamba hali hiyo ipo, na katika hali tuliyonayo tusidhani kwamba ni Tanzania peke yake kwa sababu athari zake kiuchumi ni zile zinazosababishwa kwa sehemu kubwa na mazingira ya ulimwengu. Kwa hiyo nchi zote sasa hivi zinakabiliwa na tatizo la namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa ni Watanzania kuendelea vile vile kufanya kila litakalowezezana kufanya kazi kwa juhudi kubwa zaidi na hasa kwa upande wa kuzalisha chakula, tuweze kujitosheleza hapa nchini na kiweze kupatikana kwa bei ambayo ni nafuu kutokana na wingi wake. Hapa katikati Serikali imechukua hatua mbalimbali lakini sehemu kubwa ya chakula vile vile ilivuka kwenda nje ya nchi yetu ambako waliona kuna bei nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini pengine siwezi kulieleza kwa kirefu sana kwa sababu ni mambo ya kiuchumi, nimsihi tu Mheshimiwa Diana Chilolo kwamba kwa sababu Jumatano ijayo tutakuwa na semina juu ya Hali ya Uchumi itakayounganisha masuala yote, inaweza vile vile ikampa fursa lakini kubwa ni fursa

ya sisi Waheshimiwa Wabunge kuelewa hali ilivyo na namna Serikali ilivyojipanga kujaribu kukabiliana na hali hiyo.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na majibu yako mazuri sana, kwa kuwa kilimo umetambua kabisa kinachangia pato la nchi hii kwa kiwango kikubwa sana, na kwa kuwa, wananchi wengi wanakimbilia mijini hasa Vijana na kukwepa suala la kilimo kwa sababu mbalimbali.

Je, Serikali itatumia ushawishi gani ili vijana hawa waweze kuvutika kurudi kijijini wajunge na kilimo ili kuinua pato la nchi hii? (Makofi)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ni kweli upande mmoja ni jukumu la Serikali kuweka sera, kuweka mikakati, mbinu mbalimbali za kuhakikisha mazingira yetu yanakuwa na mvuto siyo kwa vijana tu, lakini kwa Watanzania kwa ujumla na hasa kwa kutambua kwamba zaidi ya asilimia themanini (80) *basically* ni wakulima. Kwa hiyo kubwa ni kujaribu kufanya kilimo kile kiwe kizuri na chepesi na chenye tija.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa nadhani Diana Chilolo utakuwa umeona miaka miwili mitatu iliyopita Serikali imejitahidi sana kuweka nguvu zake nyingi katika kilimo, na hili maana yake nini, Maana yake ni kwamba ni lazima tuweke matumizi ya zana bora za kilimo ili kumwondolea Mtanzania ile kazi ya kufanya kwa mikono, na ndiyo maana umeona shughuli zetu zote zimeelekeza nguvu kubwa huko, tunajaribu kutafuta matrekta makubwa na madogo, na juzi tukaamua matrekta yale kutoka India kuyateremsha bei kwa asilimia kati ya kumi na tano mpaka thelathini na tano maksudi tu ili watu wengi waweze kuona uwezekano wa kukopa na kuweza kuyatumia kujaribu kurahisisha kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo juhudi hizi mimi sioni namna nyingine, kubwa ni hili litatusaidia sana kurahisisha kilimo kwa sababu siyo rahisi kwa vijana wote wale kuwapa kazi ama za kuandika za ukarani au kwamba kuna viwanda vya kutosha, lakini kupitia kilimo tunaweza vile vile sasa tukaingia katika hatua nyingine ya pili ya kuwa na viwanda vya kusindika mazao ya Wakulima hao hapa nchini. Hilo nalo litatusaidia sana kuweza kuchukua baadhi ya vijana na kuwaingiza katika sekta iliyorasmi kwa maana ya ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nafikiri ni kujipanga vizuri, na wote tushirikiane, tujaribu kuona kwamba kilimo *basically* ndiyo hasa msingi ambao unaweza ukatupunguzia tatizo hili la ajira. (Makofi)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kuniona nami niweze kumwuuliza Waziri Mkuu swali moja.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Jeshi la Polisi ni moja ya idara muhimu zilizopo ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ambayo ina jukumu la kuhakikisha suala la ulinzi na usalama linakuwepo katika jamii yetu.

Kwa kuwa, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 14, ambayo inazungumzia juu ya haki ya kuishi ya mtu yeyote ndani ya mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeonekana kukiukwa ndani ya Wilaya ya Kasulu na baadhi ya Askari wapato nane wa Jeshi la Polisi na hivyo kupelekea raia moja kupoteza maisha na mwingine ndugu yake na marehemu kutengenezewa kesi ya kwamba ni mhalifu ili kuweza kuwakwepesha hawa Askari wasiweze kuadhibiwa,

Hivi sasa taarifa zilizopo Askari wale inaonekana kwamba wamehamishwa kutoka Wilaya ya Kasulu na kupeleka katika Wilaya za Kibondo na Kigoma Mjini ili kuweza kupoteza suala hili ambalo hata Waziri wa Mambo ya Ndani ana taarifa hizi na Mawaziri wengine.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilikuwa naomba kujua ni sababu gani zinazopelekea Askari wale wamehamishwa kutoka Kasulu kabla hawajachukuliwa hatua zozote zile wakati taarifa za mwisho ilionekana kwamba jalada lilikuwa kwa DPP, naomba kupata maelezo kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Kasulu ni kwa nini Askari hao wamekiuka Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na hatua za kuwashughulikia Askari hawa zinachelewa, kwa sababu tukio ni la tangu tarehe 6 Mwezi Agosti, mwaka jana 2011.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, fupisha swali.

MHE. MOSES J. MACHALI: Naomba maelezo.

SPIKA: Ingawa swali hili kwa kweli ni *very specific* kwa kipindi kama hiki siyo maswali yanayotakiwa, labda Waziri Mkuu sijui unajua hizo habari?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika nakushukuru, nilikuwa kwa kweli nataka kuchukua mstari huo huo kwamba ukiniuliza swali ambalo ni mahsusi kiasi hiki na hukuwa hata umenipa taarifa ya awali ili niweze na mimi kusaidiwa kupata maelezo, kwa sababu mimi siyo Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, mimi ni Waziri Mkuu. Kwa hiyo, yapo mambo mapana hivi ambayo naweza nikayazungumza kwa uhakika, lakini unapoanza kuzungumza juu ya tukio lililotokea Kasulu na Askari kuhamishwa na ukategemea mimi nitakuwa na maelezo siyo rahisi sana.

Kwa hiyo naomba nikuombe sana kwa hili, mimi nimelisikia lakini nitamwomba Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aandae maelezo akupatie, halafu uone kama yatakuridhisha kuhusiana na jambo ambalo umeliuliza. (Makofi)

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika ahsante, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali yetu imekuwa na mipango mizuri ya kuendeleza maeneo mbalimbali kwa shughuli mbalimbali za maendeleo, lakini cha kushangaza miradi hiyo haiendelezwi ikiwemo ile ya uendelezaji wa Mji mpya wa Kigamboni pamoja na ule mradi wa uendelezaji wa bandari ya Dar es Salaam eneo la Kurasini. Je, miradi hii itatekelezeka lini na wananchi wa maeneo hayo waweze kupata faraja kwa sababu wametathminiwa muda mrefu lakini hawajui kinachoendelea, hawakopesheki katika mabenki, hati zao hazikubaliki.

Waziri Mkuu, unawaambia nini wananchi wako wa Kigamboni na wale wa Kurasini?

SPIKA: Hata swali hili pia liko *very specific*, lakini Waziri Mkuu labda anajua jua maana anakaa karibu na Kigamboni. (Kicheko)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, labda kwa ujumla tu maana *details* siwezi kuwa nazo kwa vyovyote vile, lakini labda nimweleze tu dada yangu kwamba inawezekana kweli tumechelewa, lakini tumechelewa vile vile kwa sababu wananchi wenyewe walifika mahali wakasema hawakushirikishwa katika mradi ule.

Kwa hiyo, ikabidi tuunde timu ambayo inajaribu kufanya maandilizi tupite kueleza mradi huo una manufaa gani na utaratibu ukoje kama ni masuala ya nini, kwa hiyo imechukua kidogo muda kuweza kukamilisha hilo zoezi. Lakini *specifically* zile *details* zake siwezi nikakuambia kwa uhakika.

SPIKA: Tunaendelea na Mheshimiwa Murtaza Ali Mangungu.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika nashukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali kwa nia njema kabisa iliamua kuanzisha wakala wa usimamizi wa vyombo vya usafiri wa nchi kavu na majini:

Je, unafahamu kwamba pamoja na uanzishwaji na sheria hizo zilizotungwa, sheria hizi mara nyingine zinakuwa ni kandamizi kwa watumiaji hasa wamiliki wa shule za binafsi na tamko la Serikali ni nini ili kuweza kuwasaidia wamiliki hao ambao wanalazimishwa kupaka rangi magari yote kuwa ya njano hali ya kuwa wakati mwingine magari yale wanakuwa wameyakodi?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu sijui kama umeelewa swali lenyewe?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kama sheria ile inaonekana ni gandamizi kwa upande wa jamii, jambo hilo linaweza kufanyiwa marekebicho, sasa labda nimwombe tu Mheshimiwa Mangungu kwamba

pingine tungepata tu maelezo hasa mahsusi eneo ambalo anadhani linahitaji marekebisho. Kwa sababu *function* ya Bunge hilo ni kuondoa mambo ya namna hiyo.

Kwa hiyo kama ana mapendekezo *specific* kwenye eneo fulani, mimi nitakuwa radhi kabisa kumwambia Waziri anayehusika alete mapendekezo hayo Bungeni, tufanye marekebisho kwa sababu hakuna anayetunga sheria hapa kwa lengo la kwenda kumkandamiza Mtanzania hapana, ndiyo maana Bunge hili ni chombo muhimu na kinaheshimika sana.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa Bunge hili Tukufu mwezi April 2009, ilipitisha sheria ya Bima na mwezi wa Mei 2009, sheria ile Rais akaisaini.

SPIKA: Sheria gani?

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Sheria ya Bima, na ilipofika mwezi Julai mwaka huo huo 2009 ikaanza kutumika rasmi; na kwa kuwa, mpaka sasa Serikali imechelewesha kuweka sera ya Bima kwa ajili ya magari yake.

Je, magari haya ambayo yanatumia barabara ambazo wanatumia wananchi wote, huoni kwamba ni makosa makubwa kwa Serikali kuyachia vyombo vyake vikatumia barabara hizi ambazo wananchi na wao wanalipia Bima hizo hizo bila ya wao kutokulipia Bima?(*Makofi/Kichekoj*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kupanga ni kuchangua, kwa hiyo Serikali ilichagua hivyo na ilikuwa na sababu zake, lakini kama utakavyokuwa unafahamu, tumekuwa vile vile tunafanya marekebisho katika mtazamo kwa sababu yapo magari ambayo tumefika mahali tukaona kwamba ni vizuri yakawa na mfumo wa bima vile vile.

Kwa hiyo tukakubali kwamba magari hayo yaingizwe kwenye utaratibu huo. Sasa wewe swali lako ni rai ya jumla ungependa magari yote ya Serikali yakawekewa bima.

Ni kweli jambo zuri, lakini lazima Serikali ilifikirie mara mbili tatu, kabla haijafikia uamuzi wa namna hiyo kutokana na wingi wa magari, lakini vile vile kutokana na mambo mengine ya kisera ambayo nayo ni lazima yazingatiwe.

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Spika ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakumbuka wakati wa Bunge la bajeti tulizungumza sana hapa kuhusu umuhimu wa kuwa na soko la kimataifa pale Himo, na kazi ile naona dalili ni nzuri, naona magreda yanachimba barabara, nimeona ofisi za soko zimejengwa, pamoja na vyoo.

Ningeomba nikuulize sasa kwa mkakati wako huo ulionao unategemea hilo soko litamalizika lini na thamani yake itakuwa kiasi gani?

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mrema, Waziri Mkuu hawezi kujua masoko yote, yaani hili swali ni *very specific* ungemwuliza Waziri wa masoko huko, lakini Waziri Mkuu labda alikuwa anapita huko Kilimanjaro.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nafikiri Mzee Mrema anajua kwamba ni nini kinaendelea pale na ndiyo maana anataka wapiga kura wamsikie tu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, juzi nilikuwa na vikao viwili Kanda ya Kaskazini na moja ya jambo ambalo nililisisitiza sana ni umuhimu wa kujenga soko kubwa pale Himo.

Lakini nalihitaji lile soko hasa kwa sababu nataka Serikali tuone uwezekano wa kuweka mazingira yatakayoweza Wakenya na majirani wengine waje kununua mazao mbalimbali kutoka pale na hasa chakula, ili kuondoa uwezekano wa kupitisha mazao kwenye njia za panya kwa kuwa na mfumo rasmi kabisa.

Kwa hiyo, bahati nzuri pale fedha ya kuanzia ipo na tumewaagiza waanze kujenga na tutaboresha kile kituo ili tuweze kuweka mazingira yawe bora zaidi na mimi ninahakika utafurahi tu baada ya muda si mrefu sana.

SPIKA: Ahsante, swali la nyongeza hujaridhika? Washa *microphone*.

MHE. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Spika, kuna swali dogo tu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hilo zoezi la kukamata watu ambao walikuwa wanavusha mahindi, kwa bahati mbaya Jimbo la Vunjo halipakani na Kenya, wajasiriamali walikuwa wanakamatwa pale Himo ndani ya Jimbo la Vunjo, Marangu Mtoni Jimbo la Vunjo, Chekereni, Jimbo la Vunjo, mpaka hata Siha ingawa siyo Jimbo.

Mheshimiwa Spika, langu nilikuwa nafikiri ungeweza ukafanya jambo moja jema, wale watu waliokamatiwa vimahindi vyao ambavyo tayari walikopa hela benki, walikopa kwenye VICOBA nimeona malori kumi na mbili (121) yameachiwa.

MBUNGE FULANI: Hatusikii.

SPIKA: *Microphone* ama haisikiki ama Mzee ameamua kusema taratibu.

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Spika, labda niongeze sauti kuna watu wamekamatiwa malori yao, wajasilimali wa Jimbo la Vunjo na bahati nzuri Mkuu Mkoa ameamuru mahindi yale yarejeshwe, lakini bado kuna mahindi yenye thamini ya shilingi milioni mia tatu (300) ambayo wenyewe wakiyataka wanaambiwa waende mahakamani.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, huwezi kuwahurumia wakarudishiwa mahindi yao ili hiyo biashara unayotaka ifanyike pale, ifanyike vizuri.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumekwishaondoa kizuizi cha Mtanzania kuuza zao la mahindi nje ya nchi yetu. Lakini wakati magari yale yanakamatwa, kizuizi kile bado kilikuwepo. Kwa hiyo, kwa yeye ambaye alifanya hivyo kwa wakati ule ni dhahiri alikiuka utaratibu tuliokuwa tumekubaliana. Sasa suala la kuyaachia magari yale na mazao yake na nini siwezi nikalijibu kwa sababu sehemu nyingine inabidi twende mahakamani ili kuweza kupata maamuzi rasmi ya Mahakama. Kwa hiyo, mimi nitakachoweza kukusaidia ni kuwaomba Wakuu wa Mkoa katika maeneo yale waangalie utaratibu mzuri wa kuharakisha ili waweze kupata maamuzi ya haraka kuhusiana na mambo yaliyojitokeza.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, suala la maafa limekuwa likishughulikiwa chini ya Ofisi yako. Hivi karibuni Mkoa wa Dar es Salaam umekumbwa na mafuriko makubwa yaliyosababisha maafa makubwa, hali iliyopelekea Serikali kutoa maelekezo kupitia kwa Rais, Wahanga wa Mafuriko yale wakiwemo wapangaji wahamishiwe katika eneo la Mabwepande. Nilitaka kufahamu ni kwa kiasi gani zoezi hilo limefanikiwa?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba Mkoa wa Dar es Salaam ulipata mafuriko makubwa na tulipoteza roho za watu pale kwa kiasi kikubwa lakini mali zao vile vile zilipotea katika mazingira hayo. Lakini msingi wake hasa ni kwa sababu wakazi wale walikuwa katika maeneo ambayo kwa kweli ni hatarishi kwa maana ya kwamba mabonde yale wakati wote maji yakijaa huwezi ukatabiri nini kitatokea. Kwa hiyo, kufuatia tukio lile, Serikali ikaona pengine sasa ni wakati muafaka tuwatake wananchi wale wakubali kutoka katika maeneo yale tuwatafutie maeneo mengine ambayo ni salama zaidi.

Kwa hiyo, bahati nzuri tukapata eneo la Mabwepande na pale tumeshapima viwanja vya kutosha. Kihesabu tulikuwa tuna kaya karibu 500 hivi na zaidi kidogo ambazo lazima tuhakikishe zinapata viwanja pale Mabwepande. Mpaka hivi karibuni tulikuwa tuna hakika na viwanja 300 ambavyo vilikuwa vimeshatolewa tayari kwa wakazi waliokuwa wametoka katika eneo lile.

Kwa hiyo, zoezi lile linaendelea tunajaribu kuweka miundombinu pale kwa maana ya maji, barabara, umeme kwa sasa tulichofanya kwanza ni kuweka turubai katika kila kiwanja pale kwa ajili ya

hatua za dharura ili kuwawezesha waendeleo na mazingira yale wakati wanajiandaa kujenga nyumba za kudumu.

Faraja niliyoipata na nataka niwashukuru sana wakazi wale ni kwamba baada ya kuona mazingira yale wengi wamepokea uamuzi wa Serikali vizuri. Kwa hiyo, kazi kubwa tutakayokuwa nayo ni kushirikiana nao tuone namna ya kuendelea kuwasaidia zaidi hasa katika hatua ile watakapofika kuanza kujenga majengo.

Kwa hiyo, lazima pale na Serikali tushirikiane nao tuhakikishe wanakuwa na ramani nzuri siyo za kubangaiza bangaiza tena. Hapana iwe ni nyumba ambayo itampa mazingira mazuri zaidi kuliko yale alikotoka.

Sasa tunayo changamoto ya pili kwa sababu hawa ni wale waliokuwa ni wamiliki wa nyumba, changamoto ya pili ni wale waliokuwa wapangaji katika hizo nyumba Mheshimiwa Rais, alipokwenda pale alisema pengine ni vizuri nao hawa tukatazama uwezekano wa kuwapa viwanja katika maeneo ambayo tunafikiri yanaweza kuwa na viwanja vya kutosha. Kwa hiyo, Serikali agizo lile tunaendelea kulifanyia kazi. Ni changamoto kubwa lakini tutajitahidi tuone namna tunavyoweza nalo hilo kulishughulikia.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni kweli kabisa wananchi wa Mabwepande hawana tatizo na Watanzania wenzao ambao wamepata maafa. Nina swali moja dogo la nyongeza. Miaka minne iliyopita Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, ilichukua maeneo kwa madhumuni ya kuwa na mpango maalum wa Wizara ya Ardhi, vile vile Chuo cha *IFM* kilichukua maeneo kwa maelezo kwamba kingewapa wananchi waliokuwa wanamiliki hayo maeneo fidia.

Lakini zoezi lilifanikiwa kwa watu wachache sana. Sasa kufuatia maafa haya kama ambavyo umeeleza kuna viwanja ambavyo tayari watu wamepewa. Lakini katika viwanja hivyo ni katika baadhi ya maeneo ambavyo wananchi walitakiwa walipwe fidia lakini hawajalipwa fidia.

Sasa kumekuwa kuna mkanganyiko sana kwa hiyo, naomba leo nipate kauli ya Serikali ukiwa kama Waziri Mkuu, ili Wananchi wa Mabwepande kama wanaangalia TV leo wajue hatima yao, ama wajue kauli ya Serikali ni nini kuhusiana na wale ambao walikuwa wanastahili fidia na tathimini ilikuwa imeshafanyika? Ahsante.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, uamuzi ule ni wa Serikali na kwa makusudi tuliona lile eneo linaweza kuwa ni eneo stahiki kwa ajili ya kuwasaidia hawa ndugu zetu.

Kwa hiyo, kwa wale ambao kwa namna moja au nyingine watakuwa pengine wameathirika kutokana na uamuzi ule. Lakini kwa ridhaa yao halina tatizo hata kidogo, Serikali inalijua na tunaendelea kujipanga ili wale watakaostahili kupata fidia tuwape fidia yao kwa sababu uamuzi ule umetokana na nia njema ya Serikali.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali langu linahusu wastaafu, wastaafu sehemu mbalimbali hapa nchini wanalamikia ucheleweshwaji wa malipo ya pensheni ya kila mwezi. Kwa mfano:-

SPIKA: Mheshimiwa Profesa huruhusiwi kusoma hapa.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Kwa mfano, wengine hawajalipwa kutoka Julai, 2011 na wengine wamelipwa Januari hadi Machi lakini hawajalipwa Julai mwaka jana. Tunachoomba kauli ya Serikali kuhusu tatizo hili. Kwa nini wastaafu wanaendelea kuteseka namna hii na kwa nini Serikali isiwe na mkakati wa makusudi wa kumaliza tatizo hili kuhusu wastaafu? (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, tatizo la wastaafu lina sura nyingi ninavyolielewa mimi kwa sababu nimekuwa nahangaika nalo sana.

Upande mmoja kikwazo kikubwa ilikuwa ni masuala ya utunzaji wa kumbukumbu kwa ajili ya wastaafu na hasa pale unapokuwa umehama kutoka ofisi moja kwenda nyingine na kadhalika, unapokuja kustaafu tumekuwa na hilo tatizo kwa kipindi kirefu. Lakini Serikali kwa kutumia mfumo wa sasa wa TEKNOHAMA imejizatiti sana katika eneo hilo na sasa hivi kwa kweli hali ya utunzaji wa rekodi zao ume-improve sana. Kwa hiyo, imetupa kidogo *leverage* moja kubwa.

Kwa hiyo, upande mwingine ni pale ambapo tayari umeshaingia katika mfumo lakini kunakuwa na tatizo la ucheleweshaji wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya malipo ya wastaafu. Hili si tatizo ambalo ni la kudumu hapana na wala si kwamba linapoathiri linaathiri makundi yote kwa wakati mmoja hapana kwa sehemu kubwa inategemea mambo mengi ambayo yanatokana na mfumo unaotumika wa malipo ya pensheni kama ni kupitia benki mara nyingi hatuna tatizo kubwa sana. Tatizo ni pale ambapo unaipata kwa kutumia hundi za kawaida kwenda kwa huyu mstaafu katika maeneo mbalimbali nchini kutokana na ukubwa wake.

Lakini Serikali inalijua na tunajitahidi kujaribu kujipanga vizuri zaidi ili tuweze kurahisisha mfumo huo hasa kwa kutumia hazina ndogo katika kila Mkoa kwa hivi sasa.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Spika, nina swali dogo la nyongeza hasa kuhusiana na wastaafu ambao wamekuwa wakiniipigia kutoka Jimbo la Bukombe kuna maaskari polisi ambao hawajalipwa toka Julai hadi Desemba kuna wafanyakazi wa Idara ya Afya na wafanyakazi wengine. Sasa ninachouliza Serikali inawapatia maelekezo gani kuhusu namna ya kufuatilia malipo yao?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kama wako kwenye mfumo tayari wa malipo ya pensheni jambo. Hilo siyo tatizo kubwa tutacheke tu na watu wa Hazina na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuona sababu zilizosababisha kuchelewa kwa malipo. Kwa sababu malipo haya yanalipwa kwa kawaida kila miezi sita (6), kila miezi 6 unalipwa. Kwa hiyo, kama kuna kuchelewa ni lazima tujue sababu za msingi zilizosababisha jambo hili.

Kwa hiyo, pengine ninachoweza kusema tu kwa sababu Waziri wetu wa Mambo ya Ndani na Hazina wapo nadhani kulifuatia tu hili tuone wapi pamekwamisha jambo hili na tutashukuru sana kama tutapata, kama una orodha kamili tuchukue hata majina yale ili tuweze kutatua hilo tatizo haraka sana. Lakini kimsingi kama wamo kwenye mfumo wa pensheni nadhani litashughulikiwa haraka sana.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu, nashukuru kwa kujibu maswali yote yaliyotakiwa 8 na ndio haya 8 yamejibiwa. Lakini Waheshimiwa Wabunge, msisahau tunapomwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuulize maswali ambayo ni ya kiseru, ukimwuliza kitu *specific* kwenye jimbo lako kwa kweli hawezi. Wengine nawashauri kwamba tukiwepo hapa Bungeni hawa Mawaziri wanayo kazi ya kuwasikiliza ninyi matatizo ya majimboni. Kama hawana majibu wao wana *connection* kule majimboni. Mengine ni *very specific* muwatumie Mawaziri walioko hapa wote. Lakini Waziri Mkuu mnamwuliza maswali ya kiseru ya ujumla ambayo na yeye anayajua. Lakini mengine haya mtakuwa mnapoteza wakati wenu kwa sababu hatayajua. Lakini vinginevyo nawashukuru tutaendelea kuimarisha utaratibu huu maana yake bado siyo mzuri sana. (*Makofi*)

MASWALI NA MAJIBU

Na. 31

Mashamba Yaliyopimwa Viwanja vya Makazi Morogoro Mjini

MHE. ABDUL-AZIZ MOHAMED ABOOD aliuliza:-

Wananchi waliokuwa wanamiliki Mashamba ya Asili maeneo ya Kiegea, Lukobe, Mgulu wa ndege mashamba hayo yamechukuliwa na Halmashauri na kupimwa viwanja vya makazi na baadhi ya waliomiliki mashamba hayo wamelipwa fidia na wengine bado:-

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia hao ambao mpaka sasa hawakufidiwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul-Aziz Abood Mbunge wa Morogoro Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ilitwaa mashamba ya asili kutoka kwa wananchi wapatao 361 katika maeneo ya Kiegeya "A" Lukobe na Mkundi Nguvu Kazi na kupima viwanja vya makazi kwa ajili ya kuendeleza Mji wa Morogoro. Baada ya kufanya uthamini wa ardhi katika mashamba hayo, ilibainika kuwa wananchi hao wanadai fidia kiasi cha shilingi kiasi cha shilingi 795,391,663.00 kati ya hao wakulima 351 tayari wamekwishalipwa fidia zao jumla ya shilingi 777,455,041.00.

Mheshimiwa Spika, jumla ya wakulima 10 hawajalipwa fidia zao kiasi cha shilingi 17,936,622.00 kutokana na sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima watano waliohakikiwa mashamba yao katika eneo la Kiegeya wamechelewa kulipwa fidia ya kiasi cha shilingi 5,790,225.00 kutokana na kukosekana kwa majina kamili. Aidha, juhudi za mawasiliano zinaendelea kufanyika ili kupata majina yao kamili kwa kushirikiana na Ofisi ya Kata na Mtaa ili waweze kulipwa fidia zao.

Mheshimiwa Spika, wakulima wengine watano wa Mkundi Nguvu kazi hawajalipwa fidia zao kwa sababu wakati wa zoezi la uhakiki wa mashamba yao, awali yalionekana kuwa nje ya eneo la mradi ambalo limepimwa viwanja lakini baadaye ilibainika kuwa wako ndani ya eneo la mradi.

Utathamini wa mashamba na mali umeshafanyika na kubaini kuwa wananchi hawa wanadai kiasi cha shilingi 12,146,397.00. Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imetenga jumla ya shilingi 17,936,622.00 kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi wa maeneo haya ya Kiegeya na Mkundi Nguvu Kazi. Malipo yao yatafanyika baada ya taarifa ya uthamini (*Valuation Report*) kuthibitishwa na mthamini Mkuu wa Serikali.

MHE. ABDUL-AZIZ MOHAMED ABOOD: Mheshimiwa Spika, mpaka sasa wanaodai ni wananchi 720 lakini Halmashauri imekuwa inawapiga chenga.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuunda Tume na kuchunguza suala hilo kwa sababu mpaka sasa Serikali inasema imewalipa, watu 720 wakati hawajalipwa?

Je, haya malipo yamekwenda wapi? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdul – Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jana wakati najibu maswali hapa nilisema kwamba kamwe Serikali hatutapuza jambo lolote ambalo linaletwa mbele yetu na Mheshimiwa Mbunge. Mimi nataka nimpe takwimu hizi nitakazompa na yeye ata-*compare* na kama anahitaji sisi tuunde tume au twende kule sisi wenyewe tukacheki kinachozungumza ili tuweze kuelewana.

Malipo ambayo yamefanyika ni haya ambayo nimeyazungumzia hapa na wako wakulima 10 tu ambao ndio wanaonekana kwamba hawajalipwa mpaka sasa hivi. Majina yao ninayo hapa ambayo mwingine anaitwa Sania, majina mafupi mafupi ambayo huwezi kujua kwamba ukitoa hela zikienda kule zitakuwa zinakwenda kwa nani ndio tafizo tunalo.

Majina ninayo hapa nimekuja nayo, nimekuja na faili zima liko hapa. Kwa hilo tatizo huwezi kumpa tu mtu anaitwa Bahati, sasa Bahati ni nani huwezi kupeleka zile hela utakuwa unapoteza hela za Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge wako wakulima 165 ambao wanaonekana kwamba walikuwa wanalima katika shamba la katani ambalo lilikuwa ni mali ya Serikali hawa wakasema hivi tunaomba mtupatie viwanja hatuna haja ya hela na nini.

Hivi ninavyozungumza hapa nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji asubuhi ya leo na amenithibitishia kwamba kazi hiyo inaendelea na viwanja hivyo vinatolewa.

Sasa Mheshimiwa Mbunge anazungumza habari ya watu 720 hili si jambo dogo mimi hapa nalichukua kwa uzito tena nikitoka hapa nakwenda nje kupiga simu. Nitamwambia Mkurugenzi wewe unaniambia habari ya watu 165 Mbunge anasema 720 ili tuweze kukamilisha jambo hili tuweze kukaa na Mbunge tuweze kujua ni nini kinachoendelea.

Lakini taarifa ndio hiyo majina ninayo na yale mengine ambayo yamekuja mengine matano nayo tunayafanyia kazi tuhakikishe kwamba wanalipwa. (Makofi)

Na. 32

Ghala Lililojengwa Kwenye Kijiji cha Miangalua – Mkoani Rukwa

MHE. ABIA MUHAMU NYAKABARI aliuliza:-

Serikali ilijenga ghala katika Kijiji cha Miangalua Mkoani Rukwa kwa niaba ya wanakijiji lakini sasa ghala hilo linaonekana limeuzwa kwa mtu asiyejulikana bila kuwashirikisha wanakijiji husika.

- (a) Je, Serikali inaweza kuwaambia wanakijiji ni nani aliyeuza ghala lao bila kuwashirikisha?
- (b) Je, inawezekanaje ghala la kijiji liuzwe na mtu asiyejulikana na Serikali ikakaa kimya tu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abia Muhama Nyakabari, lenye sehemu 'a' na 'b' kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ghala lililojengwa katika Kijiji cha Miangalua ambalo lilikuwa ni mali ya Chama cha Ushirika cha Msingi Lwangulo liliuzwa kwa kufuata taratibu zote za kisheria na wanachama walishirikishwa katika kutaja mali na madeni ya Chama kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 15 ya mwaka 1991. Zoezi la kuuza ghala hili lilifanyika chini ya Mfilisi aliyeteuliwa na Mrajisi wa Vyama vya Ushirika.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa Mrajisi wa Vyama vya Ushirika ndiye Afisa mwenye dhamana ya kukifuta Chama chochote cha Ushirika kilichofilisika kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika Na. 15 ya mwaka 1991 na kuteua Mfilisi ambaye atasimamia kubaini halisi ya Chama kama kuchunguza madeni ya Chama, kudai madeni ambayo Chama kilikuwa kinadai na kuwalipa wale wote wanaokidai chama. Kama nilivyoieleza katika kipengele 'a' hapo juu uuzaji wa ghala la Chama cha Ushirika cha Msingi cha Lwangulo ulizingatia taratibu zote za kisheria.

MHE. ABIA MUHAMU NYAKABARI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu aliyotoa Mheshimiwa Waziri swali langu nilikuwa nauliziana nani aliyeuza ghala hilo dalali au wakili?

Pamoja na hayo basi Serikali inamtambua Afisa mwenye dhamana ya kumteua mtu kwenda kuchunguza kama ghala lile labda lilikuwa na madeni au lilikuwa linahitajika kulipa.

Wananchi wa Miangura walijitolea kwa hali na mali kubeba mawe kutoka mbali mlima Kipala kule Chombe na si hivyo tu walikuwa wakisomba michanga kutoka sehemu ya mbali kichwani na bado walihudumia chakula, walikuwa vibarua wao wenyewe, walichangia michango mbalimbali ili waweze kuwezesha ghala lao likamilike.

Je, wananchi hawa nao walipewa nini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abia Muhama Nyakabari, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, labda mimi nilisaidie Bunge lako hapa na nimsaidie Mheshimiwa Mbunge ambaye anazungumza hapa. Kwa hatua hii ambayo mimi naona imefikwa na kwa namna tulivyoliona hili jambo kama Wazara, mimi nilikuwa nafikiri kule anakoeeleka kule unaweza usipate jawabu kabisa.

Hili eneo ukiangalia *historical background* yake lilikuwa ni eneo la Chama cha Ushirika *that is the bottom line* na eneo hili Chama cha Ushirika kile kilifilisika chini ya utaratibu wa PSRC na kupitia kwa mrajisi wakafika hapa tunapozungumza. Akaja mfanyabiashara pale anaitwa SUMRY akanunua lile eneo akalitumia lakini baadaye wananchi hawa ambao Mheshimiwa Mbunge anawazungumza wakalalamika wakasema kwamba tungependa sisi tutumie hili eneo kwa matumizi yetu sisi kama Kijiji na kama anavyoeleza Mbunge.

SUMRY akasema mimi sina tatizo, mkitaka mnapatie eneo lingine sasa hivi Halmashauri inachofanya imetafuta eneo lingine ambalo liko katika Manispaa. Hii inayozungumzwa ni *District Council* ya Sumbawanga alipopewa SUMRY lile ni eneo lingine SUMRY akasema hivi mimi eneo hili bado sijaridhika nalo bado sijalipenda. Kwa hiyo nataka mimi *District Council* ikishirikiana na *Municipal Council* wanipatie eneo lingine.

Mheshimiwa Mbunge na wenzangu wote hapa wanaonisikiliza mimi nilifikiri hatua ile ni hatua nzuri, nimezungumza na RAS asubuhi ya leo, nimezungumza na *District Commissioner*, nimezungumza na watu wanaohusika na jambo hili wanafanya kazi sasa ya kutafuta eneo lingine ambalo atapewa SUMRY ili sasa hili eneo libaki chini ya Kijiji. Mimi nilikuwa namwomba tuanze hapo na mimi nitamsaidia ili tuweze kumaliza jambo hili liweze kwisha.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi mzuri maana ghala hilo lipo katika Jimbo langu ufafanuzi alioutoa namshukuru sana na ni ufafanuzi mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina swali la nyongeza. Yapo maghala mengi nchini yaliyokuwa yanatumiwa na Vyama vya Ushirika, VYama vya Msingi bahati mbaya Vyama hivyo vilifilisika na maghala hayo yakakabidhiwa kwenye Vijiji husika au Kata husika yapo maghala mengi ambayo yamechakaa na Vijiji havina uwezo wa kuyakarabati.

Kwa mfano Kijiji cha Mpui kina ghala zuri lakini limechakaa. Kata ya Sandrula ina ghala zuri lakini limechakaa. Serikali ina mpango gani wa kuyakarabati maghala hayo ambayo karibu nchi nzima yapo na yanaweza kutoa huduma kwa wananchi katika kuhifadhi mazao? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Malocha kama ifuatavyo. Swali hili ni rahisi kwa sababu tulishaanzisha mambo ya stakabadhi ghalani na ndiyo habari inazungumzwa hapa. Mimi namshukuru Mheshimiwa Malocha kwamba amefuatilia hili jibu ambalo tumetoa hapa, namshukuru sana. *(Makofi)*

Tunachosema hapa ni kweli kabisa anachozungumza, yako maghala mengi sana ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi lakini yametelekezwa hapa yameachwa. Hiyo sio tatizo, yako mapya yamejengwa halafu hayatumiki, yako mapya tumeyakuta hayatumiki wengine tumewaambia kwamba tutawafukuza kazi potelea mbali hata kama watapigiwa kelele humu ndani na nini tutawafukuza tutawaambia waondoke, tutafuata taratibu.

Tunachosema hapa maghala haya yako katika Halmashauri na *planning unit* yetu ni Halmashauri, Halmashauri ikiona kwamba kuna gala limetelekezwa pale wakae na wale wahusika watengeneze mpango watuambie.

Kuna kitu kinachoitwa *O and OD (Opportunities and Obstacles to Development)* hii ya kuchochea maendeleo na kuleta ninyi wenyewe hitaji letu ni hili. Wakituletea sisi wakituambia kwamba tuna gala limetelekezwa hapa kwa sababu tumeanzia huu utaratibu wa stakabadhi galani, sisi tutashirikiana kuhakikisha kwamba maghala yale yanafufuliwa ili yatumike kwa ajili ya maendeleo ya wananchi. (Makofi)

Na. 33

Ahadi ya Kuwapatia Kisima Kirefu Wananchi wa Kijiji Cha Mlandala

MHE. MOHAMED H. MISSANGA aliuliza:-

Mnamo mwaka 2003 aliyekuwa Waziri wa Maji na baadaye kuteuliwa kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowasa aliwaahidi wananchi wa Kijiji cha Mlandala, Tarafa ya Sepuka kuwapatia kisima kirefu cha maji kutokana na adha ya maji katika Kijiji hicho ambayo yeye mwenyewe aliishuhudia:-

(a) Je, kwa nini ahadi hiyo haijatekelezwa kwa zaidi ya miaka nane(8) sasa?

(b) Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Hamis Missanga, Mbunge wa Singida Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Singida Vijijini tayari ilianza kutekeleza ahadi ya Serikali ya kuwapatia huduma ya majisafi wananchi wa Kijiji cha Mlandala. Mwaka 2004/2005 Serikali ilitenga shilingi milioni 16 zilizotumika kuchimba kisima kimoja kirefu chenye uwezo wa kuzalisha maji lita 9600 kwa saa. Mwaka 2009/2010 Serikali ilitenga shilingi milioni 52 lakini fedha hizo hazikupatikana kutokana na uhaba wa fedha Serikalini.

Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Serikali imetenga shilingi milioni 54 zitakazotumika kununua pampu na injini kwa ajili ya kusukuma maji, kununua tanki dogo na kujenga kituo kimoja cha kuchotea maji karibu na kisima.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha ili kukamilisha kazi nyingine ikiwa ni pamoja na ujenzi wa bomba kuu, tanki kubwa la maji, mtandao wa mabomba ya kusambaza maji na vituo sita vya kuchotea maji.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ingawa majibu yenyewe hayajaondoa kiu ya kupata maji kwa wananchi wa Mlandala kama walivyohidiwa na Mheshimiwa Lowasa alipokuwa Kiongozi wetu wakati ule. Maswali mawili yafuatayo:-

(a) Katika majibu yake ameeleza wazi kwamba mwaka 2009/2010 Serikali ilitenga shilingi milioni 52 ambazo hazikupatikana, sasa anasema wametenga milioni 54 kwa mwaka 2011/2012 maana yake ni kwamba mwaka 2009/2010 hazikupatikana pesa, mwaka 2010/2011 hazikutengwa pesa, hizi

anazosema milioni 54 zilizotengwa kwa ajili ya mwaka 2011/2012 zitapatikana wapi kama hiki sio kiini macho?

Nataka anithibitishie hizi zitapatikana wapi kama sio kiini macho kwa ajili ya Wananchi wa Mlandala ambao wana kiu ya maji?

(c) Serikali inafahamu kwamba fedha za miradi ya maendeleo, fedha za ruzuku hazijaenda kwenye Halmashauri zetu takribani siji miaka karibu miwili sasa na kwa maana hiyo hakuna chochote ambacho kinachofanyika sasa katika Halmashauri zetu labda Halmashauri zingine.

Singida kule hamna chochote ukiuliza hamna kitu kinachofanyika kwa sababu fedha za maendeleo hakuna, fedha ya ruzuku hakuna, fedha ya fidia hakuna imeshafutwa, vyanzo vya mapato vya ndani hakuna. Kwa hiyo hamna kinachofanyika, hivi Serikali inalifahamu hilo maana yake sasa imefika mahala hata vikao vya kisheria vya Kihalmashauri havifanyiki. Serikali inatoa tamko gani juu ya hali mbaya hii? (Makofi)

SPIKA: Haya, sasa hilo atajibu nani maana yake ilikuwa Naibu Waziri wa Maji, hili wala sio yeye. Mheshimiwa Naibu Waziri jibu la kwako.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, Serikali ipo.

SPIKA: Aha! Sasa umeuliza swali halifanani. Haya Mheshimiwa Naibu Waziri jibu lile linalokuhusu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Missanga kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa Wakuu wetu wa nchi, Waziri Mkuu au Rais au Makamu wa Rais wanapokuwa wanatembelea Vijiji kitu cha kwanza wakifika pale wanaanza kukuta kuna tatizo la maji, sasa yeye lazima akubali kwamba maji tutawapeleka. Sasa akisha ahidi Rais au Waziri Mkuu tunarudi kwenye mipango yetu tukaangalie Kijiji kile kiko kwenye mpango?

Kama hakipo tunakiwekea kwenye mpango maalum. Tuna mpango wa Vijiji 10 kwa mfano, kama kile Kijiji hakipo kwenye mpango wa Vijiji 10 inabidi tuitafutie utaratibu wa kupata bajeti yake na ndiyo maana tulianza kutekeleza kwa shilingi hizo milioni 52. Sasa swali ni kwamba hizi shilingi milioni 52 zilizopangwa mwaka huu, naomba nikuhakikishie kwamba na mimi nitafuatilia fedha hizo ziweze kupatikana ili tutekeleze ahadi hiyo ya muda mrefu ya Viongozi wetu wa Kitaifa. (Makofi)

Suala la fedha za maendeleo kwamba hazijafika, nikuhakikishie kwamba kuanzia sasa tutapeleka fedha za maendeleo katika Halmashauri zetu.

SPIKA: Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri, fedha za maendeleo ipi ya maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, nazungumza kuhusu Sekta ninayoismamia fedha za maendeleo kwenye sekta ya maji tutazipeleka kwa sababu tumeshakubaliana na washirika wa maendeleo tunaanza kuzipeleka.(Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Mukuchika swali lile lingine? Swali la pili la Mheshimiwa Missanga la nyongeza.

MHE. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Spika, ninaomba swali hilo lirudiwe tena kwa sababu sikulisikia vizuri.

SPIKA: Haya Mheshimiwa Missanga uliza swali hilo tena.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, nilisema hivi Serikali inajua kwamba fedha za miradi ya maendeleo katika Halmashauri hazijaenda takribani miaka miwili, fedha za ruzuku hazijapeleka takribani miaka miwili, fedha za fidia zilishafutwa kwa hiyo hamna kitu.

Vyanzo vya ndani havipo kwa hiyo Serikalini kule Halmashauri ni kwamba hamna kinachoendelea kila unachoulizwa hamna na kwamba baya zaidi, hata vikao vya Kisheria chini ya Halmashauri sasa maamuzi yanapitishwa na watendaji.

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya jambo hilo? *(Makofi)*

MHE. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji..

SPIKA: Hii kwa niaba yako mwenyewe na Waziri Mkuu, hiyo la Waziri Mkuu sio la maji, yeye kamaliza.

MHE. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Spika, nilidhani kwamba maswali ya Wizara yangu tuliyamaliza ndiyo maana nikasema kwa niaba lakini kama ni swali langu ningelipenda kujibu swali la kaka yangu Mheshimiwa Mlssanga, kama ifuatavyo:-

Nataka nikiri kwamba Halmashauri zote hivi sasa tuna matatizo makubwa ya fedha yaliyosababishwa na bajeti iliyokuwa imepangwa katika Halmashauri zetu, fedha zilizotoka hazifanani na matakwa ya Halmashauri.

Hili katika hata tulipofanya kikao cha wakuu wa Mikoa na Mheshimiwa Rais kuzungumzia suala la bajeti, waliomba kwamba ikiwezekana basi pamoja na *inflation* pamoja na kushuka kwa thamani ya shilingi basi tupate fedha angalau zile za mwaka jana, lakini bado hatukuweza kufikia kiwango kile cha mwaka jana.

Jambo la pili, Halmashauri zimetakiwa mwaka huu zikusanye fedha ile tunaita *own sources*, maamuzi yale tuliyafanya Halmashauri hazikuwa zimejiandaa kwa sababu walikwisha ambiwa kwamba sasa zile kodi kodi za kero tunazifuta. Kwa hiyo wakaambiwa Halmashauri tukusanye hizo fedha wenyewe, fedha zinazokusanywa na Halmashauri hazifikii kiwango ambacho walikuwa wanapata kutoka Serikalini.

Jambo hili liko mezani kwa Waziri Mkuu, tumezungumza juzi katika kikao cha matumizi ya Wizara, Waziri Mkuu ameagiza kwamba ataita kikao baina yetu TAMISEMI, Wizara ya Fedha na wote wanaohusika tuangalie namna gani jambo hili litashughulikiwa. Lakini kuonyesha kwamba tatizo ni kubwa, hata ALAT, Jumuiya ya Serikali hii za Mitaa ya Tanzania, wameomba kukutana na Uongozi wa juu wa Serikali ili kujadili tatizo hili kwa sababu hali ya fedha katika Halmashauri zetu katika kipindi hiki sio nzuri sana. *(Makofi)*

SPIKA: Siku nyingine Alhaji Missanga usiulize swali lililoko nje ya swali lingine kwa sababu ya *public interest* nimeruhusu lijibiwe.

Na. 34

Matatizo Yanayowakabili Wafugaji Nchini

MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI aliuliza:-

Wafugaji wengi wa asili nchini wanakuwa wanahamishwa hamishwa kwa makusudi na Serikali baada ya kuwapa wawekezaji maeneo makubwa kwenye Sekta ya Kilimo na Madini na kutangazwa maeneo mbalimbali kuwa Hifadhi za Kitafa hali inayofanya wafugaji kukosa maeneo ya malisho ya mifugo yao:-

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa yenyewe ndio chanzo cha kusababisha wafugaji wa asili kuenea nchi nzima bila mpango?

(b) Sekta ya Mifugo ni muhimu na inachangia kwa kiasi kikubwa pato la Taifa. Je, Serikali iko tayari kurekebisha kasoro hizo na kuwapa wafugaji maeneo ya kudumu kwa mifugo yao?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester Muhoja Kasulumbayi, Mbunge wa Maswa Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wafugaji kuhama kutoka eneo moja kwenda eneo jingine kunatokana na sababu nyingi ikiwa ni pamoja na upungufu wa malisho na maji kwa mifugo, kukimbia magonjwa ya mifugo, kubadilisha mazingira ya ufugaji, kufuata jamaa zao na wengine kufuata huduma muhimu za kijamii kama vile shule, hospitali, maji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhimiza wafugaji kuzingatia Sheria ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi Na. 6 ya mka 2007 na Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali ya Vyakula vya Mifugo Na.13 ya mwaka 2010 ili wafugaji hao warasimise maeneo ya kufugia. Aidha, wafugaji wanaelimishwa ili wafuge kulingana na uwezo wa maeneo yaliyopo. Kwa kufanya hivyo, watakuwa na ufugaji wenye tija, unaoendeshwa kibiashara na kuzingatia hifadhi ya mazingira na utakaoboresha maisha yao na kuongeza pato la Taifa.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha wafugaji kuwa na makazi ya kudumu, Serikali inaendelea kuchukua hatua kulingana na upatikanaji wa fedha kwa kutenga na kupima maeneo ya ufugaji na kuyaweka miundombinu muhimu kama majosho, vyanzo vya maji vya mifugo na pia kusogeza huduma za kijamii katika maeneo hayo.

Kati ya mwaka 2006 na 2010, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine, ilitenga na kupima maeneo ya ufugaji yenye ukubwa wa jumla ya takribani hekta milioni 8.9 katika Vijiji 728 katika Wilaya 67. Kati ya hizo hekta 1.244, 260.0 zimehakikiwa na kupewa hati na Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi. Mpango huu ni endelevu na utatekelezwa hadi Vijiji vyote nchini vitakapopimwa na kutenga maeneo ya wafugaji.

MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata majibu haya, lakini napenda nieleweshwe katika hizi hekta milioni 8 ambazo zimelenga kunufaisha Wilaya 67, mimi swali langu nauliza wafugaji wa Wilaya ya Maswa wao wametengewa kiasi gani na sehemu hiyo iko wapi?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kasulumbayi, Mbunge wa Maswa Mashariki, kama ifuatavyo:-

Nadhani swali lake hili linahitaji takwimu, kwa hiyo namshauri Mheshimiwa Mbunge baada ya kipindi cha maswali na majibu nitampatia takwimu hizo kwamba ni Vijiji vipi vimepimwa na viko sehemu gani.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kuna maeneo ya *ranch* ya Serikali ambayo hayatumiki, hayana matumizi tena kama zamani na kuna wafugaji waliozunguka katika maeneo ya hizo *ranch*. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuwapa wale wafugaji maeneo hayo ya *ranch* wafugie kama walivyokuwa wakifugia awali?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa kwamba Serikali katika maeneo ambayo *ranch* zetu hatuzitumii ama hatutakuwa na uwezo wa kuzitumia ni kweli kabisa kwamba tunapunguza baadhi ya maeneo na kuwapatia wananchi na Mheshimiwa Laizer anavyouliza ni kwamba eneo lake la Longido tuko karibu kuwakabidhi eneo la *ranch* la *West Kilimanjaro* ili waweze kutumia maeneo hayo kwa ajili ya ufugaji.

Lakini pia *ranch* ya Ruvu tuko kwenye *process* ya kuigawanya kwa maeneo madogomadogo kwa ajili ya kuwakabidhi wafugaji ambao wako *interested* kufuga ili waweze kuchukua baadhi ya eneo hili. *In fact* eneo watakalopewa Ruvu litakuwa kubwa kuliko lile ambalo tutabaki nalo sisi kama Serikali.

Kutokomezwa kwa Ugonjwa wa Sotoka Nchini

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawatambua na kuwaenzi wataalam wake waliochangia kwa kiwango kikubwa katika kutokomezwa Ugonjwa wa Sotoka (*Rinderpest*) nchini hadi kupata Cheti cha Kimataifa cha kuwa huru kwa ugonjwa huo?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ugonjwa wa Sotoka ni ugonjwa wa ng'ombe na wanyama wengine wenye kwato kama vile nyati, unaoambukizwa kwa kasi kubwa na kusababisha vifo vingi kwa muda mfupi. Ugonjwa huu uliingia hapa nchini mwaka 1920 ambapo mwaka 1923 uliua ng'ombe 42,992, sawa na asilimia 11.4 ya mifugo yote iliyoambukizwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tishio hili, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo cha Chakula Duniani (FAO) na Shirika la Afya ya Wafanyama Duniani (*World Organization for Animal Health*). Mwaka 2005 Ugonjwa huu ulitokomezwa nchini. Mwezi Mei 2007 ikathibitika kwamba virusi vinavyosababisha ugonjwa huu vimedhibitiwa na hivyo Tanzania kutunukiwa Cheti cha Kuutokomezwa Ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, sherehe za kuutokomezwa Ugonjwa wa Sotoka duniani zilifanyika Mjini Rome, Italy, tarehe 28 Juni, 2011. Vyeti 67 vya Heshima vilitolewa kwa makundi mbalimbali yaliyoshiriki katika kuutokomezwa Ugonjwa wa Sotoka na Wataalam 38 wakiwemo watatu wa Kitanzania ambao ni Profesa Mark Rweyemamu, Dkt. John Nyange na Dkt. Johnson Mollé. Aidha, Maadhimisho ya Kitaiifa ya Kutokomezwa Sotoka Nchini yalifanyika tarehe 29 Julai, 2011 ambapo Wizara ilitunuku vyeti kwa Wataalam 20 na Taasisi 16, kutambua michango yao iliyosaidia nchi yetu kupata mafanikio hayo makubwa.

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, Ugonjwa huu kwa kweli ni hatari kwa mifugo na unaathiri Biashara za Kimataifa za Mifugo na Mazao yake. Ugonjwa huu ulikuwa unaathiri Tanzania, lakini sherehe za kuipongeza nchi au za kutangaza kwamba nchi hii iko huru kwa Ugonjwa huu zimefanyika Roma:-

(i) Sasa ni vipi Watanzania wanalielewa hili na kunufaika au kupata ufahamu kuhusu manufaa ya nchi hii kuwa huru kwa Ugonjwa huu?

(ii) Kati ya watu waliotunukiwa vyeti ni Watanzania watatu tu kati ya 38 lakini shughuli hii ilikuwa inafanyika ndani ya nchi hii. Katika kufuatilia mwenendo wa ugonjwa katika nchi siyo Idara ya Mifugo peke yake wanaowajibika; huwa kuna Sekta ya Wanyamapori kwa sababu ugonjwa huu unaathiri wanyamapori na ni kazi ambayo inahitaji utaalum wa kipekee.

SPIKA: Mheshimiwa uliza swali, wanakupigia makofi swali sasa.

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Spika, ni lini sasa Serikali itafanya utaratibu wa kuwabaini Wataalam walioko katika Taasisi za Wanyamapori waliochangia kwa kiasi kikubwa katika kupata suluhisho la Ugonjwa huu? (*Makofi*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, Ugonjwa huu wa Sotoka kwa Kiingereza *Rinderpest* umeathiri dunia nzima na Afrika uliingia mwaka 1890 lakini Tanzania uliingia mwaka 1920. Sherehe kufanyika Roma ni kwa sababu ni ugonjwa uliokuwa unaathiri dunia nzima na hivyo ulikuwa umesimamiwa na FAO na Shirika la Magonjwa ya Mifugo (IOE). Tanzania pia tulifanya sherehe hizi kama nilivyosema kwamba, Wataalam 20 pamoja na Taasisi 16 zilitunukiwa vyeti. Nipende kusema kwamba,

katika Bunge hili yuko mwenzetu ambaye ni Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla, ambaye pia ni mmojawapo wa Wataalam ambao waliwezesha kuutokomeza Ugonjwa huu. (Makofi)

Kwa hiyo, Taasisi hizo 16 kwa sababu muda ni mdogo nisingeweza kuzisoma hapa, lakini pia majina yapo 20 ya watu ambao walitunukiwa vyeti walishiriki katika kuutokomeza Ugonjwa huu; baada ya kipindi hiki nitamkabidhi Mheshimiwa Mbunge aweze kuwa na orodha hii ya Taasisi pamoja na Wataalam na majina ya Wataalam ambayo ninayo hapa.

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE: Nashukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kuniona. Katika mazingira ambayo kuna Hifadhi ya Taifa pamoja na makazi ya binadamu na wanyama wa majumbani kuna mwingiliano na hii inasababisha mlipuko ya magonjwa ikiwemo kichaa cha mbwa. Hivi sasa kuna mlipuko wa kichaa cha mbwa Wilaya ya Serengeti. Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya kampeni kwa ajili ya janga hili?

SPIKA: Hiyo siyo *rinderpest*. Mheshimiwa Waziri jibu. (Kicheko)

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, mapema iwezekanavyo nitatuma Wataalam kwenye Jimbo lake na Wilaya yake ili kutathmini ugonjwa huu wa kichaa cha mbwa na kisha tuangalie kama kuna uwezekano wa kufanya kampeni au ni kiasi ambacho kinaweza kuwa *controlled* bila kampeni.

Na. 36

Fedha Zilizotumika kwa Matibabu Katika Balozi

MHE. LETICIA M. NYERERE aliuliza:-

Katika Mwaka wa Fedha wa 2009/2010 Serikali ilitumia takriban shilingi milioni 32 kwa ajili ya matibabu kwenye Balozi zetu bila uthibitisho wa maelezo kwa matumizi hayo. Je, ni lini Serikali itatoka stakabadhi na nyaraka Bungeni ili kuthibitisha matumizi ya fedha za walipa kodi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mbunge Viti Maluum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, katika ukaguzi wa hesabu za Balozi mbalimbali kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010, Wakaguzi wa Serikali walihoji kuhusu marejesho ya takriban shilingi milioni 32 zilizotumika kwa ajili ya matibabu kwenye Balozi zetu bila uthibitisho wa maelezo yenye ushahidi kuhusu matumizi hayo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, hoja zote zilizochoji matibabu kwenye Balozi zetu zilijibiwa na nyaraka husika kuwasilishwa kwa Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama Wizara ilivyoelekezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Matibabu kwa Maafisa wetu kwenye Balozi zetu, kila Ubalozi unatakiwa kuwapatia Maafisa wake matibabu kwa utaratibu wa kuteua na kuilipa Kampuni ya Bima ya Afya kila mwezi na kampuni hiyo hulipia matibabu ya watu wetu. Katika nchi ambazo hazina utaratibu huo au utaratibu upo lakini kutokana na malimbikizo ya madeni, Kampuni ya Bima inalazimika kusitisha huduma, Maafisa hulazimika kujigharamia wenyewe na baadaye kudai kurejeshewa malipo ya gharama hizo.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huo ndiyo uliozua hoja ya matumizi ya shilingi milioni 32 bila utaratibu unaokubalika kati ya shilingi bilioni 1.5 zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya matibabu katika kipindi cha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo juu, hoja hizo zimejibiwa na Wizara yangu ipo tayari kumpatia Mheshimiwa Mbunge, nakala ya maelezo tuliyoyatoa kwa ajili ya ukaguzi. Ahsante.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu.

(i) Kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kukiri kwamba Serikali ilipoteza shilingi milioni 32 ambazo hazikuwa na uthibitisho kinyume na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Umma ya Mwaka 1995; je, kwa nini sasa Serikali inatunga sheria halafu inakuwa ya kwanza kuzivunja sheria ambazo imezitunga yenyewe?

(ii) Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba gharama matibabu zilipanda au kougezeka kutokana na uzembe wa Serikali kushindwa kulipa Bima ya Afya kwa muda uliotakiwa. Je, ni lini sasa Serikali itaanza kuwa makini ili iweze kulinusuru Taifa letu na upotevu wa mamilioni ya pesa yanayosababishwa na uzembe wake?

SPIKA: Isipokuwa anayetunga Sheria ni Bunge siyo Serikali. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwanza, inawezekana sikueleweka, sikukiri kwamba tumepoteza fedha. Nilichosema kulikuwa na hoja ya shilingi milioni 32, ndicho ambacho nimekiri na nimesema kwamba, kumetolewa maelezo ambayo yametoshleza Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Sekali. Kwa hiyo, hakukuwa na upotevu wa fedha na Mheshimiwa umeliweka vizuri kwamba kwa nini tunatunga Sheria; zinatungwa na Bunge na Serikali tunatekeleza. Katika hili tumetekeleza kwa sababu Sheria hiyo hiyo iliyoelekeza pale ambapo kuna hoja, Serikali ijibu kama ambavyo tumejibu na majibu mazuri yametoshleza. Ahsante. *(Makofi)*

MHE. CHRISTOPHER OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na ukweli kwamba nakubaliana na hoja ya Naibu Waziri kwamba hoja ya shilingi milioni 32 ni hoja ya Ukaguzi, lakini katika siku za karibuni kumekuwepo na upotevu mwingi wa fedha katika kile kinachoonekana kama ni kulipa huduma za Serikali bila kufuata utaratibu. Uliitolewa mfano wa ufujaji wa hoja ya shilingi bilioni kumi iliyoripotiwa jana kulipa kwa Kampuni ya Chiko katika mradi hewa, iliyoripotiwa kwamba imetolewa na Maafisa wa TANROAD wakishirikiana na Wizara ya Miundombinu.

Sasa kwa kuwa ufujaji huu wa fedha za umma ni jambo linalohitaji kusimamishwa au kushughulikiwa vyema; je, Serikali ina mpango gani wa kuchunguza ufujaji mkubwa wa fedha kama hizi zilioripotiwa jana ili kuondoa aibu na fedha za umma kupotea katika visingizio vya kulipa huduma hewa?

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, wewe ukifikiria swali huoni kama ni tofauti kabisa na wala Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa hajui. Naomba tuendelee na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Assumpter Mshama.

Na. 37

Ahadi ya Kupeleka Umeme Kata za Nkenge

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA aliuliza:-

Wakati wa Kampeni za Uchaguzi wa mwaka 2010 aliyekuwa Mgombea wa Urais kwa tiketi ya CCM, Rais Jakaya Mrisho Kikwete, aliahidi kupeleka umeme katika Kata za Mutukula, Buyango, Ruzinga, Ishozi na Ishunju Nsunga:-

(a) Je, ni lini umeme utapelekwa katika Kata hizo?

(b) Je, katika Kata za Kitobo, Bwanjai na Gera kuna umeme ambao hautoshelezi; je, ni lini Serikali itaweka transfoma ili umeme utosheleze kwa wakazi wa maeneo husika?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mbunge wa Nkenge, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme nchini TANESCO, imefanya makadirio ya gharama za kupeleka umeme katika Kata za Mutukula, Buyango, Ishozi na Ishunju.

Gharama za kupeleka umeme katika Kata ya Mutukula ni shilingi bilioni 1.3. Umeme utatokea Bunazi kupitia Igayaza, Nsunga, Kabwaba hadi Mutukula. Kazi zitakazofanyika ni ujenzi wa njia ya umeme wa msongo kv 33 yenye urefu wa kilomita 26 na ufungaji wa transformo tano kati ya hizo tatu za 50kVA na 2 za 200kVA.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ziara yangu Mkoani wa Kagera kati ya tarehe 9 hadi tarehe 11 mwezi huu wa kwanza mwaka huu, niliwaagiza Wakala wa Nishati Vijijini (REA) pamoja na TANESCO washirikiane kutenga fedha kwa ajili ya kupeleka umeme Mtukula ili upande wa nchi yetu nao upate huduma hiyo muhimu ambayo tayari inapatikana upande wa pili wa nchi jirani ya Uganda.

Gharama za kupeleka umeme katika Kata ya Buyango ni shilingi 785,748,467.36. Umeme utatokea Kashasha kupitia Luzinga, Bwera, Lushasha, Kyazi hadi Buyango. Kazi zitakazofanyika ni ujenzi wa njia ya umeme wa msongo kv 33 yenye urefu wa kilomita 14 na ufungaji wa transformo sita kati ya hizo tano zenye ukubwa wa kVA 50 na moja yenye ukubwa wa 100kVA. Gharama za kupeleka umeme katika Kata za Ishozi na Ishunju ni shilingi bilioni moja. Umeme utatokea Gera kupitia Mkeyambe, Ishunju na Ishozi. Kazi zitakazofanyika ni ujenzi wa njia ya umeme wa Msongo wa kv 33 yenye urefu wa kilomita 20. Ufungaji wa transformo nane kila moja yenye ukubwa wa KVA50. Maombi ya fedha za upelekaji wa miradi hii yamewasilishwa REA kwa ajili ya kupata fedha za utekelezaji.

(b) Mheshimiwa Spika, Kata za Kitobo, Bwanjai na Gera zina umeme, isipokuwa Kata za Kitobo na Bwanjai zina tatizo la Wananchi kupata umeme mdogo hasa wakati wa jioni. Jumla ya shilingi bilioni 52.2 zimetengwa kwenye bajeti ya mwaka 2011 ya TANESCO kwa ajili ya uboreshaji wa umeme katika Kata ya Kitobo. Kazi zitakazofanyika ni ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kv 33 umbali wa km 2.5 pamoja na uwekaji wa transformo moja yenye ukubwa wa 50kVA. Kazi imeshaanza kwa kusimika nguzo na itakamilika mwaka wa 2012.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Bwanjai, imeombewa fedha katika bajeti ya Shirika la Tanesco ya mwaka 2012 ili kuweza kuweka transformo yenye ukubwa wa 50kVA itakayosaidia Wananchi kupata umeme wa kutosha muda wote. Kata ya Gera, umeme upo wa kutosheleza muda wote na hakuna matatizo ya umeme mdogo isipokuwa mahitaji ya umeme kwa watu walioko vijiji vya mbali ndani ya Kata hiyo bado ni makubwa na maombi ya umeme ya Kata hii tayari yameshapelekwa kwa Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Kwanza, napenda kuipongeza Serikali kwa namna ya pekee kwa jinsi ambavyo wameliona tatizo hili kubwa kwa muda mrefu. Swali ni kwamba:-

(i) Katika umeme utakaotoka Bunazi kulelekea Mtukula kuna vijiji kama vinne umevitaja pale. Je, hivyo vijiji navyo vitapata umeme; maana isije ikawa kama ulivyopita juu kwa juu mpaka Bukoba?

(ii) Waziri hajaeleza ni lini hizo pesa au Mradi huu utakapoanza katika Kata za Buyango, Luzinga, Ishozi na Ishunju. Zaidi ya hapo nashukuru sana kwa namna ya pekee.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninamshukuru Mheshimiwa Assumpter Mshama, kwa kutoa pongezi kwa Serikali kwa jinsi inavyosimamia utekelezaji wa Miradi hii ambayo iliwaahidi. Ahadi ni deni na tutaendelea kuyatekeleza yale tuliyoyaahidi. Naomba pia nitumie nafasi hii kujibu maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Jimbo la Nkenge kwamba, vijiji vyote ambavyo vinakidhi vina sifa ya kupatiwa huduma hiyo kutokea mahala ambapo tutauchukua umeme huo na kuupeleka Mtukula, vitapatiwa hiyo huduma. Tumeshalijadili hili na tumeshajipanga. Hii bajeti ya shilingi bilioni 1.3 inazingatia hilo. Vijiji vyote ambavyo nimevisema vya Ishozi, fedha yake itatoka katika mwaka huu wa fedha na tunatarajia kuanzia kati ya mwezi wa tatu au mwezi wa nne kutangaza tender kwa ajili ya kupata wakandarasi watakaotekeleza Miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. VITA R. KAWAWA: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa hii nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikituahidi kwa vipindi tofauti kuanzia mwaka 2006 kuwa Mji wa Namtumbo utapatiwa umeme; na kwa kuwa TANESCO sasa kuanzia siku 12 tu zilizopita ndiyo wameanza kupeleka nguzo za umeme; Serikali inaweza kuharakisha mkataba na mkandarasi atakayefunga jenereta hilo ili kazi hiyo iende sambamba na *distribution line*?

SPIKA: Swali la Namtumbo. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwanza kabisa ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Vita Kawawa, kwa ufuatiliaji wake wa karibu sana kuhusu utekelezaji wa ahadi ambao Serikali tulishatoa. Pili, napenda kutumia nafasi hii kumhakikishia yeye binafsi kama Mwakilishi wa Jimbo la Namtumbo na Wananchi wa Namtumbo kwamba, ratiba kwa kupitia mkataba uliofungwa kati ya Serikali kupitia Shirika la TANESCO na mkandarasi utazingatiwa.

Napenda pia kutumia nafasi hii kukuhakikishia kwamba, utekelezaji wake utafanywa kwa kadiri ambavyo tumekusudia.

Kuhusu ombi la Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha ujenzi wa mahala ambapo mitambo itawekwa na njia za usambazaji uende sambamba, hayo ndiyo makusudio na ndiyo maana amesema Mheshimiwa Mbunge kwamba, hivi karibuni kwa sababu TANESCO wameanza kupeleka vifaa kwa ajili ya kuanzia shughuli hiyo.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ahadi hizi za Serikali zinakwenda sambamba na ahadi kubwa ya Serikali ya Mradi wa Umeme kwa msaada wa Ubalazi wa Sweden kutoka Makambako ukipita Vijiji vya Igawisenga, Wino, Madaba, Mkongotema, Lutukila mpaka Bumbilo na hatimaye kuingia Songea na mradi huu umekuwa ukisubiriwa kwa takriban miaka saba mpaka sasa na utekelezaji wake haujaanza:-

Je, Mheshimiwa Waziri anawapa kauli gani Wananchi wa vijiji hivyo ndani ya Jimbo la Peramiho lakini Wananchi wa Mji wa Songea na Mji Mdogo wa Peramiho kwamba Mradi huo sasa utaanza kutekelezwa ili tatizo kubwa la umeme katika Mkoa wa Ruvuma kwa kuanzia na maeneo niliyosema liweze kuwa limeondoka kabisa?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Kwanza; ni kweli kwamba, Mradi huu ulitarajiwa uwe umeshafanyika miaka kadhaa iliyopita, lakini ukweli pia ni kwamba, Miradi inayotekelezwa kutokana na fedha ya kusaidiwa ina changamoto zake. Ninapenda kutumia nafasi hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu na Taifa kwa ujumla kwamba, changamoto zilizokuwepo sasa zimekamilika; mtaalamu sasa hivi anatarajisha makabrasha kwa ajili ya kuwapata wakandarasi watakaotekeleza Mradi ule. Inakusudiwa kwamba, kabla ya katikati ya mwaka huu, utekelezaji wa Mradi huo utakuwa umeanza na utakapokuwa unakamilika, maeneo aliyoyataja yakiwemo maeneo ya Wino na Madaba, yatapata huduma hiyo. Pia tunakusudia umeme huo ufike mpaka Mbinga kwenyewe na hata Jimboni kwa Mheshimiwa Vita Kawawa, Namtumbo. Kwa sababu lengo ni kuhakikisha kwamba Mkoa wa Ruvuma unaunganishwa katika Gridi ya Taifa kupitia Mradi huo. *(Makofi)*

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri imeonekana wazi kabisa Wizara yake kwa niaba ya Serikali ina mipango mbalimbali ya kuweza kuhakikisha kwamba umeme unafika katika maeneo mbalimbali. Kasusu ni eneo mojawapo ambapo kuna Mradi wa kuhakikisha kwamba, umeme unawafikia Wananchi karibu katika maeneo yote ya Mji wa Kasulu lakini kuna tatizo la nguzo.

Nilikuwa naomba pengine Waziri anisaidie maelezo nijue ni lini nguzo zitafika ili hatimaye yale maeneo ambayo yamesalia katika ukamilishaji wa Mradi ule zitapatikana lini kwa sababu ni tatizo la muda mrefu na mwaka jana niliuliza juu ya swali hili?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Moses Machali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, tutumie nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza sana Wananchi wa Kasulu, ahadi ya umeme iliyokuwa imetolewa miaka ya nyuma imetekelezwa, lakini ambacho kimefufurahisha na sisi Serikali tunajipanga kukabiliana na hizo changamoto za mapokeo ya huduma hii ya umeme ni namna ambavyo Wananchi wamehamasika sana kuunganishiwa umeme kwa kasi kuliko ambavyo labda pengine Wataalamu wetu walitarajia. Hitaji la ongezeko la nguzo linaenda sambamba na mahitaji ambayo Wananchi wa Kasulu pamoja na Wilaya ya Kibondo walivyohamasika na inaonesha kwamba walikuwa wamejiandaa kuupokea umeme.

Mheshimiwa Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali kupitia Shirika la TANESCO, tunaendelea kuhakikisha kwamba, vifaa vya kutosha vinapatikana kwa ajili ya kuongeza huduma ya umeme. Ahsante sana.

Na. 38

Tabia ya Akina Mama Kutelekeza Watoto

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS aliuliza:-

Kumekuwa na tabia mbaya kwa baadhi ya akina mama kuzaa watoto na kisha kuwatupa wakiwa hai ama wamekufa:-

Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya jambo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inakemea vikali uwepo wa tabia mbaya ya akina mama wanaozaa watoto na kuwatupa wakiwa hai kwa kuwa pamoja na kusababisha vifo, watoto wanaopatikana wakiwa hai wanalazimika kuishi katika vituo vya kulelea watoto na kukosa mapenzi ya wazazi wao. Hali hii ni uvunjwaji wa haki za mtoto kwa vile watoto hao wanaotupwa wanakosa haki yao ya kuishi na kupata malezi stahili kutoka kwa wazazi wao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukemea suala hili, hatua mbalimbali za kisheria zimechukuliwa na zitaendelea kuchukuliwa kwa wanaofanya vitendo hivi ikiwa ni pamoja na kufunguliwa kesi mahakamani. Hata hivyo, mara nyingi inakuwa vigumu kuwatambua wahusika wa vitendo hivi kwa vile hufanya matukio hayo mbali na maeneo wanayoishi.

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kumuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Je, Serikali ina mkakati gani endelevu kwa kushirikisha Polisi Jamii Ulinzi Shirikishi kukomesha vitendo vya dhuluma ambavyo wanafanyiwa watoto wasiokuwa na hatia?

(ii) Je, Serikali ipo tayari kuweka kituo cha malezi katika kila Wilaya kwa wale akina mama ambao wanapenda kuzaa tu na kuwatupa watoto badala yake wawapeleke katika vituo hivyo kwa malezi? Ahsante sana. (Makofi/Kicheko)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge, kwa kutambua kazi ambayo Polisi Jamii inaweza kufanya katika kukomesha tatizo hili. Napenda kutumia Bunge lako Tukufu kutoa rai kwa jamii kwamba, tuendelee kukemea vitendo hivi, lakini pia sisi wenyewe jamii tuwafuatilie wanawake wajawazito kuanzia katika ngazi ya Mtaa, Kijiji na Kata ili kuweza kuwabaini wote wanaofanya vitendo hivi na kuripoti katika vituo vyetu vya Polisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili niseme kwamba, kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto, Namba 21 ya Mwaka 2009, imeweka wazi pale ambapo Halmashauri ya Mtaa, Kata, Wilaya, itaona kwamba watoto hawa ni watoto yatima au wanakosa malezi kwa kuwa wazazi wao hawana uwezo, basi ni wajibu wa Halmashauri kuanzisha mipango husika ya kuwalea watoto hawa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nitumie Bunge hili kumshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama anaona swala hili ni muhimu kila Halmashauri tuwe na sehemu za kuwalea watoto na akina mama wanaotupa watoto, basi alipeleke katika Vikao vya Baraza la Madiwani na wakiona kuna umuhimu huo, Serikali Kuu haiwezi kuwazuia, itategemea na *resources* ambazo zipo katika *level* ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Nami ningependa niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mbali na kwamba kuna akina mama ambao wanazaa na kutupa watoto, lakini pia kumekuwa na tabia ya watoto ambao wamepoteza wazazi wao ambao wanalelewa na ndugu na jamaa, wamekuwa wakifanyiwa vitendo vya ukatili katika familia na wengine wakibakwa bila Wizara husika kupata taarifa. Pindi wanapogundulika kufanyiwa vitendo hivyo, wototo wengi wanakuwa wameathirika sana.

Je, Serikali au Wizara husika ina mkakati gani kabambe wa kuhakikisha wanawagundua watoto wao na kuwasaidia kabla hawajapata athari zaidi?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tatizo la ukatili dhidi ya watoto ni tatizo ambalo limekuwa kubwa katika nchi yetu. Ninafurahi kusema kwamba, Tanzania ni nchi moja ya kwanza katika nchi za Afrika ambapo tumefanya utafiti kujuu ni kiasi gani Watoto wa Tanzania wanakumbana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Kwa kweli tutawaletea Waheshimiwa Wabunge taarifa hii waone; ni taarifa ambayo inasikitisha sana! Ukatili wa watoto wa kijinsia, ukatili wa kingono, *physical* na wa kisaikolojia, umekuwa ni mkubwa sana. Kwa hiyo, tuna mkakati gani sisi kama Wizara?

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana kwa kushirikiana na *UNICEF* tulifanya huo utafiti tuone ni kiwango gani ukatili dhidi ya watoto ni mkubwa nchini mwetu na baada ya hapo tumeanzisha mpango mkakati wa kila Wizara, Wizara ya Elimu, kwa sababu ukatili unatokea katika mashule, *TAMISEMI* nao, Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na tumeshaanza kuwabaini. Swala lililokuwepo ni kuwapeleka katika Vituo vya Polisi. Kwa kushirikiana pia na *UNICEF*, katika baadhi ya vituo tumeanzisha madawati ya wanawake na watoto tukiwaambia kama kuna tatizo la watoto wanaonyanyaswa na kufanyiwa vitendo vya kikatili, basi tunaomba Wananchi wakaripti ili hatua husika zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, hatujaweza kuanzisha madawati ya wanawake na watoto katika kila kituo, lakini katika baadhi ya Vituo vya Polisi, tumeshaanza kufanya hili. Hili tunaona litatusaidia sana kukomesha vitendo vya ukatili dhidi ya watoto; wawe wanalelewa na walezi, wawe watoto yatima au watoto ambao wanalelewa na wazazi wao.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema hata kama mzazi ni mtoto wako, hauruhusiwi kumfanyia vitendo vya kikatili; kumfinya au kumpiga. Tafuta adhabu nyingine ambayo unaona inaweza ikamrekebisha mtoto, lakini haturuhusu umpige viboko vitano, sita, mtoto wako wa miaka mitano sidhani kama unamfunza.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Haya jamani muda umekwisha na maswali yamekwisha. Kwanza, ninapenda kuwatambulisha wageni tulionao hapa Bungeni.

Tunao wanafunzi wanne kutoka *BBC Media Action* na wanahabari. Kwanza, wasimame wale wanne kutoka *BBC Media Action*; wako wapi? Ahsante.

Wapo Wanahabari wa Tanzania 18, wakiongozwa na Ndugu Anthony Hausan, Mkufunzi Mwandamizi, wasimame walipo. Ahsante sana.

Tuna maafisa kumi kutoka *Bank ABC* ya Dar es Salaam, wakiongozwa na Mkurugenzi wao Mkuu, Ndugu Boniface Nyoni. Naomba nimwone Ndugu Boniface Nyoni na wale wengine wote wasimame; wale wa *Bank*. Ahsante sana. *(Makofi)*

Kuna wanafunzi 75 kutoka Chuo Cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, wakiongozwa na Mwalimu wao Ndugu Paul Michael na Mlezi wao Bwana George Banoba. Bwana Paul Michael, tumwone na huyo Mlezi wao Bwana George Banoba na wanafunzi hao 75 wasimame tuwaone. Ahsante sana. Tunawategemea sana katika hii fani ya Mahakama; hawa jamaa wanalalamika hakuna Mahakimu kule kwao wala Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo hawapo, kwa hiyo, someni vizuri. *(Makofi)*

Kuna wanafunzi kutoka Chuo Kikuu Kishiriki cha Biashara Moshi, ambapo yupo *counterpart* wangu Ezra Shauri, Spika wa Chuo; yupo wapi huyo? Ahsante sana *Mr. Speaker*. Tuna Naibu Spika wa Chuo hicho, Ndugu Baraka Mashaka; ahsante sana, wasalimie hao unaowasimamia huko. *(Makofi)*

Tuna Wanachama watatu kutoka Chama cha Albino, Mkoa wa Morogoro; wako wapi hao wenzetu? Hatujawaona, labda watakuja baadaye. Ahsanteni sana.

Shughuli za kazi; kuna tangazo la vikao vya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Sitta, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo mara baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge, saa saba mchana, kutakuwa na Kikao cha Kamati kitakachofanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa C.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dokta Abdalla Kigoda, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo mara baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge, yaani baada ya Kipindi cha Maswali, kutakuwa na Kikao cha Kamati ambacho kitafanyika katika Ukumbi Namba 231, Ghorofa ya Pili, Jengo la Utawala. Nimewaruhusu hawa wakutane sasa hivi kwa sababu kuna kazi ya dharura niliyowapa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Edward Lowassa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo, leo saa saba mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa B.

Halafu nina tangazo lingine linalotoka kwa Afisa Habari wa Ofisini kwangu pale anasema; Waheshimiwa Wabunge wote wanatangaziwa kuwa *ABC Bank*, hawa niliowatambulisha hivi sasa, watakuwa na maonesho katika Viwanja vya Bunge leo, kwa lengo la kuelezea shughuli za Benki yao.

Aidha, jioni ya leowameandaa tafrija kwa Waheshimiwa Wabunge katika Hoteli ya Dodoma. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa sana. Sikuwaambia mwende na vitambulisho, lakini wote mnakaribishwa sana, itakuwa usiku baada ya Kikao cha Bunge bila ya shaka.

Waheshimiwa Wabunge, nimemaliza matangazo. Kesho ni Siku ya Sheria katika nchi yetu. Kwa kawaida Mihimili yote mitatu husherehekea sherehe hiyo; kwa hiyo, nitakuwa katika sherehe hizo na kwa sasa ninamwomba Mheshimiwa Naibu Spika, anipokee kazi hii ya Bunge. Ahsanteni. *(Makofi)*

Hapa Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, asalaam alaykum. Ni muda mrefu sana hatujaonana.

Katibu, tuendeleo na hatua inayofuata.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Naibu Spika - Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Mwongozo wapi? Aah, ni wawili eeh?

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo wawili.

NAIBU SPIKA: Basi, tunaanza pale halafu tutamalizia.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Nilitaka kupata mwongozo wako; hivi sasa tuna mgomo wa Madaktari ambao unaendelea nchini. Suala hili ni la dharura na la umuhimu mkubwa sana katika umma wetu. Nilikuwa nataka nipate mwongozo wako kwa nini tusitumie kifungu cha 47(1) cha Kanuni zetu kuahirisha mjadala ambao unaendelea sasa hivi ili tupate fursa ya kujadiliana na kushauriana vizuri jinsi gani ya kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mnyika?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa ni suala hilo hilo ilita niongezee tu kwamba, kulitolewa maelezo siku chache zilizopita wakati Kanuni hii ya 47 ilipotaka kutumika kujadili jambo la dharura juzi na jana kukatolewa tena maelezo mengine kuhusiana na kauli ambayo ilipaswa kuwasilishwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningependa kupata mwongozo wako kwa sababu Kanuni ya 49 iliyozungumzwa jana, inahusu mambo ambayo yanaihusu Serikali. Pili inatoa wigo kwa Spika, kuamua kwa mujibu wa wakati atakaoona unafaa hiyo hoja kuweza kuja. La tatu, Kanuni ya 49, inasema hilo jambo litakalotolewa Kauli na Serikali liwe halizui mjadala.

Jambo lililoko mbele yetu la Madaktari, kwanza, linaonesha kwamba siyo hoja ya Serikali tu peke yake ni hoja ya Wananchi ambao sisi kama wawakilishi wa Wananchi tunataka iingie Bungeni. Pili ni jambo ambalo ni la dharura, haliwezi kusubiri muda mrefu kwa sababu hii ya Kauli ya Serikali ni *discretion* ya Spika, kuweza kulileta Bungeni. Tatu, hili ni jambo ambalo linazua mjadala; kwa hiyo, Kauli ya Serikali ambayo haitakuwa na mjadala haiwezi kutufaa kwenye jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kupata mwongozo wako ili tuwe na mfumo, haitatolewa tu Kauli ya Serikali bali Bunge litajadili kwa dharura jambo hili kwa haraka ili tuweze kuokoa maisha ya Wananchi wanaofariki hivi sasa kutokana na mgomo wa madaktari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ambayo Waheshimiwa Wabunge wameitumia zaidi ni ya 47(1), ambayo inasomeka kama ifuatavyo: "Baada ya muda wa maswali kwisha Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kuwa shughuli za Bunge kama zilivyooneshwa kwenye Orodha ya Shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma." Kwa kweli Mheshimiwa Ndugulile na Mheshimiwa Mnyika, wameitumia kanuni hii vizuri kwamba tufikirie jambo hilo la kuahirisha shughuli zote ili tujadili jambo hili muhimu la mgomo wa Madaktari. Tatizo ni moja tu kwamba; walipotoa hoja zao hawakuungwa mkono. Kwa hiyo, Katibu tunaendelea na hatua inayofuata. *(Kicheko/Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

M A A Z I M I O

Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Jedwali la Nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kuridhia mapendekezo ya amri ya marekebisho ya Jedwali la Nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147, yanayokusudia kurekebisha Jedwali la Nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa unaozwa kwenye maji yanayohifadhiwa katika chupa kutoka shilingi 99 kwa lita hadi shilingi 12 kwa lita.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuishukuru Kamati ya Fedha na Uchumi, chini ya Mwenyekiti wake mahili Mheshimiwa Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa michango yao waliyoitoa wakati wa kujadili Azimio hili jana tarehe 1 Februari. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwamba, michango yao tunaithamini na pia tumeifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba, kupitia Sheria ya Fedha Namba Tano ya Mwaka 2011 hususan kifungu cha nane, Bunge lilipitisha marekebisho ya Jedwali la Nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147, ambapo pamoja na mambo mengine, marekebisho hayo yaliweka ushuru wa bidhaa wa shilingi 69 kwa lita kwa maji yanayohifadhiwa katika chupa, yaani *bottled and packed water*. Kabla ya marekebisho haya, bidhaa hii ilikuwa haitozwi ushuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini iliyofanyika baada ya ongezeko hili la ushuru wa bidhaa imebaini kwamba:-

- (i) Bei ya maji yanayohifadhiwa kwenye chupa imepanda kwa kiasi kikubwa na hivyo kuwafanya watumiaji wengi ambao ni Wananchi wa kawaida kushindwa kumudu bei husika na hivyo kutumia maji ambayo siyo salama na hivyo kuhatarisha maisha.
- (ii) Ongezeko hili la ushuru wa bidhaa limesababisha bei ya maji yanayozalishwa na viwanda vya hapa nchini kuwiana na bei za maji yanayoagizwa kutoka nje ya nchi na hivyo kuondoa ushindani uliokuwepo hapo awali. Hali hii itapunguza uzalishaji wa viwanda vya hapa nchini na hivyo kupunguza mapato ya ndani na ajira kwa Wananchi.
- (iii) Aidha, tathmini imebaini pia nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki za Kenya, Ruanda na Uganda zinatozwa ushuru wa asilimia kumi. Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kidogo cha saba cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147, kinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya fedha kwa kupitia amri itakayochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, kufanyia marekebisho Jedwali la Nne la Sheria kwa lengo la kupunguza au kuongeza viwango vya ushuru wa bidhaa vilivyoainishwa kwenye Jedwali husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na tathmini iliyofanyika, Waziri wa Fedha kupitia amri iliyotangazwa kwenye Tangazo la Serikali (Na. 332) la Mwaka 2011, lililochapishwa tarehe 30 Septemba, 2011, alipunguza ushuru wa bidhaa kwa maji kutoka shilingi 69 kwa lita hadi shilingi 12 ili kuwawezesha Wananchi wa kawaida ambao hawapati maji safi na salama kumudu gharama za ununuzi wa bidhaa hii

na hivyo kuwaepusha na uwezekano wa kupata magonjwa na kuhatarisha maisha yao kwa kutumia maji yasiyo salama. Aidha, shilingi 12 za ushuru zinazopendekezwa ni sawa na asilimia kumi ya wastani wa bei yakiwa ndani ya uzalishaji, yaani *extra factory price* ya uzalishaji ya shilingi 120 kwa lita.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini iliyofanyika inabainisha kwamba, baada ya kurekebisha ushuru wa bidhaa kwenye maji ya chupa kutoka shilingi 69 kwa lita hadi shilingi 12 kwa lita, matokeo ya lita yanayotarajiwa kimapato ni kama ifuatavyo:-

- (i) Ushuru wa bidhaa uliotegemewa kukusanywa kwa kipindi cha Julai 2011 hadi Juni 2012 katika kiwango cha 29 kwa lita ni shilingi milioni 12,549.5;
- (ii) Mapendekezo mapya ya kupunguza ushuru wa bidhaa kutoka kiwango cha 69 kwa lita hadi kiwango kinachopendekezwa cha shilingi 12 kwa lita yatatupatia shilingi milioni 2,704.2;
- (iii) Mapendekezo ya kurekebisha ushuru wa bidhaa kutoka shilingi 69 kwa lita hadi shilingi 12 kwa lita yataleta upungufu wa mapato kwa kiasi cha shilingi 12,000,845.1; na
- (iv) Kuanzia Julai hadi Desemba 2011, Serikali imekusanya kiasi cha shilingi 6,000,730 kama ushuru wa bidhaa wa maji ya chupa kwa kiwango cha shilingi 69 kwa lita. Kati ya hizo shilingi milioni 1,440 ni maji yanayoagizwa kutoka nje na shilingi milioni 5,290 ni maji yanayozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mchanganuo katika kipengele cha nne hapo juu, Serikali inahitaji kupata vyanzo vya mapato kuziba pengo na shilingi 8,000,819.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali inategemea kukusanya shilingi 2,000,704.2 kwa kiwango kipya cha shilingi 12 kwa lita, ina maana kwamba, kila mwezi itahitaji kukusanya shilingi milioni 225. Hivyo, kwa kiwango kipya cha ushuru wa bidhaa cha shilingi 12 kwa lita, Serikali inahitaji kukusanya shilingi milioni 900 kuanzia mwezi Machi hadi Juni 2012. Hivyo, kwa kutumia kiwango kipya cha shilingi 12 kwa lita na nakisi ya mapato itapungua kutoka shilingi 8,000,819.3 hadi shilingi 7,000,719.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapendekeza kuziba nakisi hiyo kwa kupunguza matumizi yake kwa kiasi cha shilingi 7,000,719.3 kwa kupunguza matumizi ya kawaida, yaani OC. Maeneo yanayokusudiwa kupunguzwa ni pamoja na haya yafuatayo: Posho; fedha zinazotumika kwenye kongamano; ununuzi wa magari; ununuzi wa samani; gharama za uendeshaji wa ofisi; mafunzo ya Ndani na Nje; safari za Ndani na Nje; na ukarabati wa majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchapishwa kwa amri hii, Serikali iliendelea na mchakato wa kuwasilisha amri hii Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha Azimio husika kwa mujibu wa kifungu cha 124(8) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 137, kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Sheria ya Fedha (Na. 5) ya Mwaka 2011 ilifanya marekebisha kwenye Jedwali la Nne na Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147, kwa kuweka tozo ya ushuru wa bidhaa kwenye maji yanayohifadhiwa kwenye chupa kwa kiwango cha shilingi 69 kwa lita;

NA KWA KUWA tathmini ya ushuru huo imebainisha kwamba tozo hiyo imeathiri ushindani wa bidhaa za maji yanayozalishwa hapa nchini na kuathiri uzalishaji wa bidhaa hii kwa viwanda vya ndani ya nchi;

NA KWA KUWA kifungu kidogo cha saba cha kifungu cha 124 cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147, kinampa mamlaka Waziri wa Fedha kwa kupitia amri iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali,

kufanya marekebisho kwenye Jedwali la Nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147, kwa lengo la kupunguza au kuongeza viwango vya ushuru wa bidhaa zilizoainishwa katika jedwali hilo;

NA KWA KUWA kifungu cha kidogo cha nane cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147, kinaelekeza kwamba marekebisho yatakayofanyika kwenye Jedwali la Nne lazima yaridhiwe na Bunge kupitia Azimio la Bunge;

NA KWA KUWA Waziri wa Fedha kwa kuzingatia umuhimu wa kulinda viwanda vya ndani kutokana na ushindani kwa viwanda vya nje na kwa lengo la kuongeza mapato na ajira kwa Watanzania na kwa kupitia amri iliyotangazwa kwenye Tangazo la Serikali (Na. 332) la Mwaka 2011, amefanya marekebisho kwenye Jedwali la Nne na Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147, kwa kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye maji yaliyohifadhiwa kwenye chupa kutoka shilingi 69 kwa lita hadi shilingi 12 kwa lita; na

HIVYO BASI kwa kuzingatia umuhimu wa marekebisho hayo, Bunge hili katika Mkutano wa Sita na kwa mujibu wa kifungu cha 124(8) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147, sasa linaazimia kuridhia punguzo la ushuru wa bidhaa kutoka shilingi 69 na kuwa shilingi 12 kama Waziri wa Fedha alivyotangaza kupitia Tangazo la Serikali (Na. 332) la Mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, kwa mawasilisho hayo. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati iliyochoambua jambo hili; namwona Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi; karibu. *(Makofi)*

MHE. DKT. ABDALLAH KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la Mwaka 2007 na kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, naomba kutoa maoni na ushauri kuhusu Azimio la Bunge kuridhia amri ya Marekebisho ya Jedwali la Nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba, wakati Waziri wa Fedha akiwasilisha Bungeni mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, alifanya marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2011 kwenye Jedwali la Nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147, kwa kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye maji yanayohifadhiwa kwenye chupa kutoka kiwango cha sifuri kwa lita hadi shilingi 69 kwa lita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 124 cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, kifungu kidogo cha saba na cha nane, Waziri wa Fedha ana mamlaka ya kurekebisha Jedwali la Nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa. Waziri wa Fedha alitumia mamlaka hayo kupitia amri ya Serikali ya tarehe 13 Agosti 2011 iliyotolewa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 30 Septemba 2011.

Hata hivyo, kifungu kidogo cha nane cha kifungu 124 cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, kinamtaka Waziri wa Fedha kuwasilisha au kupata ridhaa ya Bunge kwa uamuzi aliouchukua wa kurekebisha Jedwali Namba Nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa. Ridhaa hiyo inatakiwa ipatikane mara moja pale Bunge linapokaa na kama Bunge halijakaa basi suala hili litapelekwa katika mkutano wa Bunge unaofuata.

Kwa mtiririko huu, ridhaa ya Bunge ilitakiwa ipatikane katika Mkutano wa Tano wa Bunge la mwezi Novemba 2011 na hivyo hili halikufanyika kama Sheria inavyotaka. Kamati inasisitiza umuhimu wa Serikali na vyombo vyake kufuata taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inakubaliana na kuunga mkono Azimio la Bunge la Kuridhia Amri ya Marekebisho ya Jedwali la Nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147, linalolenga

kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye maji yaliyohifadhiwa kwenye chupa kutoka shilingi 69 kwa lita hadi shilingi 12 kwa lita.

Hatua hii inatokana na ukweli kuwa, ongezeko hilo la ushuru wa bidhaa hii kutoka kiwango cha sifuri hadi shilingi 69, limeathiri sana ushindani wa bidhaa za maji yanayozalishwa hapa nchini na hivyo kuathiri uzalishaji wa bidhaa hii kwa viwanda vya ndani ya nchi.

Pamoja na ushauri uliotolewa na Kamati hapo awali wakati wamewasilisha mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 kuwa, kiwango kilichopendekezwa kwenye bajeti ni kikubwa, Kamati inaipongeza Serikali kufikia uamuzi huu ingawa kwa kuchelewa na kulileta Azimio hili mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zote Duniani zinazopiga hatua za kimaendeleo hasa katika kukuza sekta zake za uzalishaji na zile za huduma za kiuchumi, zimekuwa makini sana katika kuhakikisha kuwa zile bidhaa ambazo zinaweza kuzalishwa katika nchi husika kwa gharama zinazohimilika (*comperative advantage*) na zinaweza kutoa ushindani mzuri wa bei kibiashara ni lazima zilindwe. Kutokana na ulinzi huu, kutaifanya nchi yetu iwe ikitegemea bidhaa kutoka nchi za nje na kudumaza uzalishaji wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto zinazokumba uchumi wetu, takwimu zinatuoonesha dhahiri kuwa ni muhimu kujiimarisha katika suala la uzalishaji wa bidhaa zetu ili kuimarisha uchumi wetu. Kwanza, mahitaji yetu ya bidhaa kutoka nje ya nchi ni makubwa kuliko mapato mauzo yetu nje ya nchi. Mauzo ya bidhaa nje ya nchi yana uwezo wa kulipia mahitaji yetu kutoka nje ya nchi kwa asilimia 60 tu.

Pili, katika nyanja ya biashara za bidhaa na huduma nje, kipindi cha Julai mpaka Novemba 2011, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ilifikia Dola za Kimarekani milioni 3010.1 wakati thamani ya bidhaa na huduma zinazoagizwa nje kwa kipindi cha miezi ya kwanza ya Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 ilifikia Dola za Kimarekani milioni 5,427.1.

Pengo hili ni kubwa. Picha hii inahitaji Serikali kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha kuwa, inachukua hatua imara za kuimarisha uzalishaji wa bidhaa zetu za ndani. Yapo maeneo kadhaa ambayo Serikali inabidi kuyaangalia kwa haraka ili kukuza ushindani wa bidhaa zetu zinazolishwa hapa nchini. Maeneo haya ni pamoja na yale ya kiseru, kisheru, masuala ya kodi na ushuru pamoja na taratibu zetu tunazojiweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema kutoa mifano kadhaa; takwimu zilizotolewa na Baraza la Kilimo Tanzania (*Agricultural Council of Tanzania*), zinaonesha kuwa upo utitiri mwingi wa kodi mbalimbali zinazoathiri tija katika uzalishaji wa Sekta ya Kilimo. Kwa njia hii hatuwezi kulinda Sekta ya Kilimo. (*Makofi*)

Taifa linaagiza zaidi ya tani 300,000 za mafuta ya kula; ya pili kwa utumiaji wa fedha za kigeni baada ya dizeli na petroli wakati tuna uwezo mkubwa wa kuzalisha mbegu za mafuta hapa nchini na kutengeneza mafuta ya kula hususan pamba na alizeti. Serikali inaagiza tani 500,000 za ngano kwa mwaka kutoka nchi za nje kwa thamani ya shilingi bilioni 300 wakati tuna uwezo wa kuzalisha mahitaji yetu yote ndani ya nchi pamoja na kuuza nje.

Serikali inaagiza kutoka nje maziwa ya thamani ya shilingi bilioni tano kila mwaka na kiasi hiki kinaonesha kinaongezeka kwa asilimia 9.5 kila mwaka wakati kwa uangalizi mzuri maziwa haya tunaweza kuyazalisha hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaagiza zaidi ya tani 200,000 kutoka nje wakati uwezo wa viwanda vyetu katika kuzalisha zao hili ni mkubwa. Yapo maeneo mengine kama vile uzalishaji wa magunia ya katani, maboksi ya vifungashio na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mantiki ya maelezo haya ni kuwa Kamati inaamini kuwa maeneo haya yakiangaliwa vizuri na kushughulikiwa kwa umakini yatasaidia sana kupunguza athari za ushindani wa bidhaa zetu zinazolishwa hapa nchini na hivyo kupunguza athari ya viwanda vya ndani ya nchi yetu. Matokeo yake ni uzalishaji wa bidhaa za kutosha na hivyo kujenga umadhubuti na uendelevu wetu wa

fedha za kigeni katika uchumi wetu. Hatua zote muhimu zitakazochukuliwa zinahitaji ukubali wa uongozi pamoja na *management* sahihi ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi inakubaliana na Azimio lililowasilishwa na Waziri wa Fedha na hapo hapo inasititiza kuwa ili kuliongezea Taifa mapato yake na kuimarisha uchumi wake katika maeneo mengine, maeneo mengine yaangaliwe kwa umakini na hatua za haraka za kisheria, kisera, kodi na ushuru, taratibu na kadhalika zichukuliwe ili kuibua uchumi wetu. Aidha, Kamati inaishauri Serikali jinsi muda unavyoendelea iangalie mikakati ya kukomesha uagiza wa maji kutoka nje ili kulinda matumizi ya fedha za kigeni yawe ya tija zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati, sasa napenda kuwatambua kwa majina Wajumbe wa Kamati walioshughulikia Azimio hili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Maulida Komu, Mheshimiwa Dokta Binilithi Mahenge, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Christine Mughwai, Mheshimiwa Mwigulu Mchemba, Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Danstan Kitandula, Mheshimiwa Dokta William Mgimwa, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Alhaji Mohamed Missanga, Mheshimiwa Andrew Chenge na Mheshimiwa Luhaga Mpina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Fedha na Naibu Waziri wa Fedha na watendaji wakuu wa Wizara pamoja Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuandaa na kukamilisha azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nikushukuru wewe mwenyewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika kwa kutupatia miongozo na maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge Dokta Thomas D. Kashillila na Katibu wa Kamati ya Fedha na Uchumi Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa ya Azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dokta Abdallah Kigoda Mwenyekiti wa Kamati, nakushukuru sasa. Sasa nimuombe Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika Wizara hii Mheshimiwa Christine Mughwai.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI – NAIBU MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Kwa niaba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge na kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni ya 86(6) Toleo la mwaka 2007, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu marekebisho ya jedwali la nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura ya 147. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kukutakia wewe na Bunge lako Tukufu kheri na baraka za mwaka wa 2012. Pia, napenda kutoa salamu za mwaka mpya kwa viongozi wangu wote wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wanachama na wafuasi wetu wote kwa juhudi na kazi kubwa wanayoifanya ya kujenga CHADEMA nchi nzima. Aidha, nitoe pongezi zangu za dhati kwa viongozi wangu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na hususani Waziri Kivuli Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge kwa ushirikiano mkubwa na kwa kunipa miongozo katika utendaji wangu wa kazi za Kibunge katika Wizara ya Fedha. Sambamba na hilo, nimshukuru pia Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati yangu ya Fedha na Uchumi kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia pindi ninapohitaji msaada na maelekezo kutoka kwao. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuweka kumbukumbu sahihi maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Fedha wa mwaka 2011 ambayo niliyawasilisha hapa Bungeni tarehe 22/6/2011 kwa niaba ya Waziri Kivuli wa Fedha, tulitoa ushauri kuhusiana na jedwali la nne kama ifuatavyo na ninaomba kunukuu: "Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha sita cha Muswada huu kinafanyia marekebisho jedwali la nne la Sheria ya Kodi kwa kuongeza katika bidhaa mbalimbali kama maji na vinywaji baridi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa Serikali haina nia ya dhati ya kushusha mfumuko wa bei za vyakula ambao pia unajumuisha maji na vinywaji hivyo. Waziri alishakiri kuwa mfumuko wa bei kwa kiasi kikubwa unasababishwa na ongezeko la bei za vyakula kwa hiyo, ongezeko hilo la kodi katika maji na vinywaji baridi kwa vyovyote vile litasabadisha kuongezeka kwa mfumuko wa bei katika vyakula na maisha kuzidi kuwa magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hizo, Kambi ya Upinzani inapendekeza kifungu hicho kifanyiwe marekebisho kwa kuondoa ongezeko hilo la kodi katika maji na vinywaji baridi na kurejea kodi iliyokuwepo zamani." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutoa ushauri huo Serikali haikuona umuhimu wa ushauri wetu kwa wakati huo na waliamua kuongeza ushuru huo wa maji ya kunywa ya chupa hadi kufikia shilingi 69. Iwapo ushauri wa Kambi ya Upinzani ungezingatiwa kusingekuwa na athari za ushindaji wa bidhaa za maji yanayozalishwa hapa nchini na hivyo kuathiri uzalishaji wa bidhaa hii kwa viwanda vya ndani ya nchi kama ambavyo Serikali inatueleza hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tunashukuru kuona kuwa Serikali sasa imerudi na kuona kuwa kuna makosa yalifanyika katika maamuzi yake. Kambi ya Upinzani inaridhia mabadiliko haya kwani ndiyo ulikuwa ushauri wetu. Muda umefika sasa kwa Serikali kuondokana na dhana ya kukataa kila ushauri unaotolewa na Kambi ya Upinzani, kwani sisi sote tuna lengo la kuhakikisha wananchi na jamii nzima ya Watanzania wanapunguziwa ukali wa maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio lilioletwa na Serikali linatambia kwamba tathmini ya ongezeko la ushuru wa maji kutoka shilingi 12 kwa lita hadi shilingi 69 limeathiri ushindani wa bidhaa za maji yanayozalishwa hapa nchini na hivyo kuathiri uzalishaji wa bidhaa hiyo kwa viwanda vya ndani ya nchi. Jambo la msingi tunaporidhia marekebisho haya ni kwamba tunaitaka Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu mambo haya yafuatavyo:-

Moja, ikiwa lengo ni kulinda viwanda vya ndani ni kwa nini sasa Serikali isiongeze ushuru wa bidhaa hiyo inayoagizwa kutoka nje ya nchi? Serikali itoe mchanganuo wa kina ni kwa vipi itafidia upungufu wa mapato ambayo yangepatikana kwa ushuru wa maji wa shilingi 69 kwa lita na kuwa shilingi 12 ukizingatia kuwa Bajeti ya Serikali ilishapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tunajadili Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na kwa kuwa katika hotuba ya Bajeti yetu mbadala tulisisitiza juu ya ukwaji wa uchumi vijijini na kwa kuwa watumiaji wengi wa mafuta ya taa wako katika maeneo mengi ya vijijini ambayo hayajaunganishwa na umeme wa Gridi ya Taifa, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali ilekeze mapato yote yanayotokana na ongezeko la kodi ya mafuta ya taa kwenye ruzuku kwa Wakala wa Umeme Vijijini yaani REA na utekelezaji wa miradi mingine ya maendeleo yenye kupunguza gharama za nishati kwa Watanzania wa kipato cha chini kama fidia ya ongezeko la bei ya mafuta ya taa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inakusudia kuleta hoja ili Bunge lipitishie Azimio kuhusiana na ushuru wa mafuta ya taa ulioongezwa kwa shilingi 358/= kwa lita ili upelekwe kwa Wakala wa Umeme Vijiji (REA) kukabiliana na tatizo la nishati kama fidia ya ongezeko la bei ya mafuta ya taa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Christina Mughwai, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Fedha. Sasa tunaendelea na uchangiaji kuhusu Azimio lililo mbele yetu na mchangiaji wetu wa

kwanza atakuwa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Abdallah Amour. (Makofi)

Mheshimiwa Hamad Rashid! (Makofi)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ni mwingi wa rehema na utukufu lakini nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kuchangia Azimio hili lililowasilishwa na Waziri wa Fedha. (Makofi)

Lakini kabla ya hapo naomba nitoe shukrani za pekee kwa wananchi wa Jimbo la Wawi kwa mapokezi makubwa na ya heshima waliyonipa na kwamba bado naendelea kuwa Mbunge wao hadi hapo tarehe 13 Machi Mahakama itakavyoamua vinginevyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja iliyoanzishwa na Waziri wa Fedha asubuhi hii ni ya muhimu sana lakini tunafikiri twende kwa upana zaidi kama vile ambavyo Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha kwa niaba yetu alivyowasilisha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni vema Serikali ikazingatia sana kuheshimu taratibu zetu za kisheria, kama Kamati ilivyosema kwamba ilitakiwa Bunge lililopita ndiyo Azimio hili lingeletwa lakini kwa bahati mbaya halikuletwa. Zipo sababu ambazo Waziri labda atazieleza baadaye lakini ni vema kila wakati Serikali ikawa makini katika kusimamia sheria za nchi na taratibu ambazo tumejiwekea sisi wenyewe, vinginevyo Bunge hili wakati mwingine litakuja na mambo kama haya linaweza kabisa likakataa. Kwa hiyo, ni vema Serikali ikajipanga vizuri katika kuwasilisha hoja kama hizi kwa kufuata taratibu za sheria na kanuni tulizojiwekea. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili hivi sasa Waziri alipokuwa anawasilisha amesema kuna maeneo ambayo atapunguza matumizi yake ili kufidia pengo la shilingi bilioni 7.7, kati ya hayo kuna posho, fedha zinazotumika kwenye makongamano na kadhalika, lakini kubwa kuna gharama za uendeshaji wa Ofisi yaani OC.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tumesikia asubuhi ni kiasi gani Halmashauri zetu za Wilaya kwa muda mrefu ambapo zimekosa fedha na katika eneo ambalo limeathirika sana moja ni OC, sina hakika kama bajeti iliyokuja ambayo tuliipitisha katika Bunge hili kama kweli imesimamiwa vizuri na inatekelezwa vizuri. Nasema hivyo kwa sababu wiki moja tulikuwa na watu wa TRA katika Kamati ya Fedha na Uchumi na walieleza kwamba mapato yamezidi kwa 102%, sasa inapokuwa Serikali imepata mapato makubwa lakini Halmashauri hazina fedha au Serikali yenyewe katika matumizi yake yenyewe haina fedha, kunakuwa na uelewa mdogo sana kwetu sisi Wabunge na wananchi kwa ujumla. Hii fedha inayokusanywa kwa ziada lakini baadaye kwenye matumizi kuna upungufu, upungufu unatokea wapi na fedha hiyo inakwenda wapi? Hayo maswali lazima Mheshimiwa Waziri utupe majibu.

Leo tuna matatizo ya madaktari, tuna matatizo ya wanafunzi na pia tuna matatizo kadha wa kadha lakini fedha inayokusanywa kwenye Serikali inaonekana TRA inafanya kazi nzuri ya kukusanya fedha je, kuna matumizi nje ya bajeti tuliyoipanga katika Bunge hili au kuna nini kinachotokea? (Makofi)

Mimi nafikiri hili Waziri atakapokuja atufafanulie vizuri sana vinginevyo tutakuwa tunapata mashaka kwamba bajeti tunayoipitisha hapa na matumizi yanayokwenda mbele ya safari ni vitu viwili tofauti na hii itaifanya Serikali ionekane kila wakati tupo kwenye lawama.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze kwanza haya mafungu aliyoyasema ni kwa kiasi gani kila fungu katika hii shilingi bilioni 7.7 itakuwa imeathirika? Maana yake ameyataja mengi tu na yapo nane, kila fungu litaathirika kwa kiasi gani na kwa maana hiyo bajeti tulipitisha katika Bunge hili itakuwa siyo sahihi tena yaani siyo ile bajeti tuliyoipitisha. Je, Waziri anakusudia kuja na *supplementary budget* baadaye? Au atabaki na bajeti hivyo hivyo kama ambavyo anapendekeza? Nalo ni jambo ambalo itabidi atueleze vilevile. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba hivi sasa kwenye zao la korosho peke yake tani ambazo zilinunuliwa ni 65,000; tani 85,000 bado hazijanunuliwa ziko kwa wakulima. Haya ni mazao ambayo

yangeweza kutusaidia katika kutupatia mapato makubwa katika Serikali. Sasa wakati mmoja tunawahimiza watu wazalishe lakini upande wa pili hakuna *efforts* zinazochukuliwa za makusudi za kuonekana kilichozalishwa ama kinaingia kwenye soko na mkulima anafaidika, matokeo yake mapato ya Serikali yanaathiri, leo bajeti ya Serikali ina uwezo wa kujikimu miezi mitatu mpaka minne tu kwa sababu bado urari wetu wa biashara siyo mzuri kama alivyoelezea Mwenyekiti wa Fedha.

Lakini matatizo ni mipango dhaifu iliyopo na moja ambalo lipo ni kwamba hakuna *coordination* kwenye Serikali, kwenye korosho kuna tani 85,000 hazijanunuliwa, ukihesabu misimu ya korosho duniani hivi sasa watu wanakwenda zao *West Africa* kununua korosho na korosho za Tanzania zitakuwa hazinunuliwa tena maana yake msimu wa kununua korosho kwa upande wetu sisi kutoka nje umepita. Wanunuzi watawalalia wakulima wetu wa korosho, badala ya kununua kwa shilingi 800/= watanunua kwa shilingi 500/= kwa sababu msimu wa kununua huku kwetu umeshapita. Sasa kama kungekuwa na *coordination* baina ya taasisi hizi za wakulima na Serikali na wakajua *programme* nzuri ikawekwa ya kununua bidhaa hizi, hayo matatizo ambayo tunayapata kwenye bajeti sasa hivi yasingepatikana, hilo halipo! Lakini hata *coordination* ya miradi ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika,, Serikali hivi sasa ina matatizo makubwa sana katika miundombinu, lakini tumepitisha katika Bunge hili Sheria ya *PPP* ambayo ingeruhusu *Private Sector* kuingiza ndani na kuweza kusaidia kuziba pengo la Serikali. Ukienda Serikalini ukauliza hivi sasa kwamba ni mradi gani mliouweka unahitaji *investors* kuja kuwekeza, hakuna majibu tokea tupitishie sheria mpaka hapa tulipofika. Sasa hili ni tatizo la msingi kwa hiyo wawekezaji wapo wengi wanahitaji kuwekeza kwenye *Private Sector* lakini bado hakuna mipango ya kuweza kusema kunazipa vipi *gap* ya miradi ambayo hatuna pesa na kwa kiasi gani *Private Sector* ishiki.

Kwa hiyo, matatizo haya yatakuwa yanaendelea kila siku. Ukimuuliza Waziri wa Fedha hana majibu, ukimuuliza Waziri anayehusika na Uwekezaji atakwambia bado tupo katika mipango ya kuweka na kadhalika. Mimi nafikiri bado tuna matatizo, *coordination is very poor* kwenye *government*, tumelisema kwenye Kamati hilo kwa Mawaziri wote wanaohusika lakini bado hatua haijachukuliwa.

Mimi ninaomba sana hatuna sababu ya kubeba mzigo ambao watu wa kuubeba wapo, kama Serikali ingekuwa na mipango mizuri na utaratibu mzuri, akijua *private investor* akienda mahali fulani atapata majibu kazi ya kupata wawekezaji ipo na ingewezekana haraka sana na tupo tayari kuisaidia Serikali katika hilo lakini kama mtu atakuja akirudi kila siku nani atakuja kufanya *investment* mahali ambapo bado utaratibu wa kufanya biashara ni mgumu sana.

Kwa hiyo, nasema Serikali ni lazima ijipange katika hilo, kuwe na *coordination* ili kupunguza huu mzigo, vinginevyo tutaendelea hivyo miaka miwili kama Halmashauri haikupata pesa mwaka mnaopata pesa mnarudi tena nyuma mara 10 kwa sababu miradi ya nyuma mmeiacha muda mrefu hamjaitokeleza, hakuna maendeleo mtakayoyapata hata siku moja. Kwa hiyo, bado tutaendelea kupiga hadithi tu kila siku bado hatua haijachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri katika Bajeti alituhidi suala zima la kuacha Bajeti tegemezi. Hivi sasa Bajeti yetu *donors* wametoa 46% ya fedha kwa hiyo, tuna pengo kubwa tu la miradi ya maendeleo kwa kutegemea wawekezaji. Rasilimali za nchi zipo, wawekezaji wapo, tungeweza kuachana kabisa na mambo ya kutegemea *donors* kama tulivyozea, lakini bado Serikali haijajielekeza hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwanza nilitaka nimuombe sana Mheshimiwa Waziri suala la *coordination* ni la msingi sana ili tujue *centre* moja ya kushughulikia *engagement* ya *private sector*, uchumi ambao hauna mahusiano mazuri haujengi maelewano mazuri, haurahisishi mahusiano baina yake na *private sector*, huo uchumi hauwezi kuendelea hata siku moja katika dunia ya leo. Hakuna Serikali inayoweza kujikimu kiuchumi kama haishirikiani kikamilifu na *private sector*. Mimi nafikiri hilo halijafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wenzangu asubuhi walikuomba mwongozo wako ili tuzungumzie suala hili la madaktari. Kwa bahati mbaya hatukusimama kuwaunga mkono. Jambo lenyewe ni la muhimu sana, mimi nataka nitoe rai kama mmoja kati ya wazee katika Bunge hili. Niiombe Serikali i-engage hii Kamati ya Wataalam (Madaktari Bingwa) waliopo ili mgogoro huu umalizike, lakini vilevile niwaombe Madaktari ambao wamegoma, niwaombe sana, Watanzania wengi wanaathirika, watoto wanaathirika,

akinamama wanaathirika na wao najua katika hali ya maisha wanaathirika, lakini anayepoteza maisha anaathirika zaidi. Niwaombe Madaktari wakati Madaktari Bingwa na Serikali wanazungumza, warudi kazini. Nawaomba sana! Nawaomba sana. (Makofi)

Wabunge tukubali kwamba wenzetu wana matatizo, tuyatatue matatizo yao lakini tatizo la kwanza kabisa watu wetu wakatibiwe. Mgonjwa ambaye yupo hospitali, ile kumuona Daktari peke yake ni sehemu ya matibabu mbali na kupata dawa, ile kumuona Daktari ni sehemu ya matibabu. Nawaomba sana Madaktari, lakini naiomba sana Serikali, hizi *symptoms* za kwamba kuna mgomo au kutatokea jambo lolote lile, jamani tuzikinge. Haiwezekani watu hawalipwi mishahara yao kwa wakati, hawalipwi posho zao kwa wakati na tunatumia *cash budget!* Tunapotumia *cash budget* na ukaniambia kama umekusanya mapato zaidi hakuna sababu zaidi ya mtu kukopwa. Mtupe maelezo mengine, kama una mapato ya ziada na bado unaendelea kuwakopa watu na unatumia *cash budget* lazima kuna maelezo ambayo mnapaswa kuyatoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya matatizo ambayo yanatokea kwa kweli hayana sababu ya kutokea. Kama yana sababu yaelezwe mapema, tusingoje yakafikia katika hali kama hii tuliyofikia hivi sasa. Tume-*deploy* leo vijana wetu wa Jeshi kwenda kufanya kazi, si hali nzuri hata kidogo. Hizo ni hatua za mwisho kabisa katika Taifa. (Makofi)

Kwa hiyo, naomba mambo mawili, moja, naiomba Serikali iharakishe hiyo *process* ya kuzungumza na Madaktari Bingwa wafikie ukomo. Lakini wakati huo huo niwaombe Madaktari tena bila ya masharti ya aina yoyote, Serikali msitoe masharti, wakatoe huduma lakini ombi lao lisikilizwe kwa haraka na wapatiwe majibu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Kama nilivyosema Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, atafuatiwa na Mheshimiwa Leticia Nyerere na Mheshimiwa Dokta Charles Tizeba ajiandae. (Makofi)

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nianze tu kwa kuishukuru Serikali kwa kufanya haraka tathimini ya maji baada ya kuweka ongezeko la shilingi 69 kwa lita kutoka zero, kwa hivyo kwa hili naishukuru Serikali. Wameweza kufanya tathimini ya haraka na wakaelewa kwamba watu wenye kipato cha chini wanashindwa kununua haya maji na wakaja hapa wakaleta Azimio la kutaka tubadilisha haraka na irudi kwenye shilingi 12 kwa lita. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni pongezi kubwa. Serikali iliyokuwa makini imeweza kufanya tathimini kwa haraka na inawajali watu wenye kipato cha chini. Watu wenye kipato cha juu wanaweza kununua maji kwa bei yoyote, lakini Serikali hii imewajali watu wa kipato cha chini na ikatambua vijijini watu wengi wanatumia maji na hivyo ikabadilisha haraka huu ushuru. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nina masikitiko makubwa kuona hadi hii leo tunaagiza maji kutoka nje, hata maji! Kuna bidhaa nyingine unaweza ukaagiza kutoka nje, lakini hata maji tunaagiza kutoka nje! Maji ni kitu muhimu, kila mtu anatumia maji. Kwa hiyo, naishauri Serikali iangalie kiwango cha maji kinachotakiwa kutumika kwa nchi nzima halafu ishirikiane na sekta binafsi tuweze kuzalisha maji hapa hapa nchini. Wazo hilo wakilitekeleza vijana wataweza kupata ajira na tutaweza kuongeza pato la nchi kwa wingi sana kuliko kutumia fedha za kigeni (dola) nyingi kununulia haya maji.

Kuna moja hili amelisema Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kuhusu kuheshimu Sheria na Kanuni na mimi naligusia kidogo. Mheshimiwa Waziri pale penye matatizo njoo kwenye Bunge lako utuelezee na Bunge litaidhinisha na utaweza kuitisha hicho kikao wakati mwingine. Siyo busara kuamua tu wewe mwenyewe ambapo hili Azimio lilitakiwa kuja katika Mkutano wa Tano lakini halikuja na badala yake limekuja katika Mkutano huu wa Sita. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kidogo nataka kugusia habari ya pengo dogo ambalo litajitokeza hapa kwenye hii Bajeti. Nilitaka Waziri aniambie hili pengo la milioni sijui 72 au ngapi ambalo amelisema hapa atali-cover vipi? Nataka nijue hili pengo atali-cover vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kweli sisi tumeshapunguza ushuru wa maji, lakini wasiwasi wangu mkubwa ni kwamba wafanyabiashara watauza maji kwa bei iliyopo. Hawatazingatia kuwa wananchi hawawezi kununua hayo maji ili waje na lile punguzo la bei katika maji. Sijui Serikali itafanya nini katika kuliangalia jambo hili. Kwa hiyo, tunataka tuone maji yameshuka bei. Siyo kupunguziwa ushuru na maji yakabakia kuuzwa katika bei ile ile. Kwa hiyo, ni jukumu la Serikali lakini pia sisi wananchi kuhakikisha kwamba jambo hilo linafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba ili kufanikisha hili naomba matangazo ya kutosha yatolewe ili watu waelewe kwamba ushuru umepungua. Kwa sababu huko vijijini hawatapata habari na wataendelea kununua maji kwa bei hiyo hiyo na wengine huwa wanashindwa kununua maji na wakaamua kunywa maji machafu. Tunajua maji machafu yanaleta madhara, kwa hiyo, tuangalie jambo hili na tulifuatilie vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kidogo nataka kuzungumzia kuhusu hali ya uchumi. Hali ya uchumi ni mbaya sana. Namuomba Mheshimiwa Waziri kwa makusudi aifanye kazi kwa sababu sasa mfumuko wa bei umekuwa mkubwa sana. Kama kuna vitu ambavyo anaweza kuvipunguzia ushuru basi vipunguziwe kwa haraka ili wananchi wote waweze kumudu kununua hivyo vitu. Kuna mwenzangu hapa aligusa bei ya mafuta ya taa.

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa juzi niliuliza swali nikaambiwa uchakachujaji umekwisha, lakini mwananchi wa kawaida itamsaidia nini wakati anashindwa kununua chakula? Kwa sababu mafuta ya taa yanapanda bei na hawezi kumudu kuyanunua, chakula kinapanda bei, ushuru wa vyakula pia unapanda bei kila siku, mwananchi wa kawaida huwa hawezi kununua chakula.

Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie wananchi wengi wanateseka mijini na vijijini, mtu anashindwa kununua mlo mmoja. Tusijitazame siye tu na kuona mtu anakula kutwa mara tatu, lakini wenzetu hao waliotupigia kura, hao wananchi wa kawaida wanashindwa kununua hicho chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mie niseme japokuwa hatujasimama kuunga mkono hiyo hoja aliyoitoa Mheshimiwa John Mnyika, hata sijui tuseme vipi, lakini tunasema tunaunga mkono. Tuko pamoja na yeye na itakapokuja tutaichangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niipongeze Serikali kwa kuwa sikivu na kufuata ushauri ambao Kamati yetu ya Fedha na Uchumi ilikuwa imewapatia tangu awali, lakini bahati mbaya wakati huo hawakuweza kupata ushauri wetu, lakini sasa tunashukuru Serikali hatimaye imefuata ushauri wetu, imepunguza ushuru wa maji kutoka shilingi 69 hadi shilingi 12 kwa lita. Nawapongeza kwa usikivu wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie punguzo la ushuru huu wa maji hadi shilingi 12 kwa lita. Kuna upungufu wa takribani shilingi bilioni 7.7 ambazo Mheshimiwa Waziri anapendekeza pengo hili litazibwa kutokana na kupunguza matumiuzi ya kawaida zikiwemo gharama za ukarabati wa majengo. Sioni mantiki ya kupunguza gharama za ukarabati wa majengo ukizingatia kwamba hali ya majengo ya ofisi zetu inatakiwa iwe katika hali njema ya kiafya na katika *standards* za kawaida za Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kupuuza kukarabati majengo kwa sababu matokeo yake unaweza ukakuta panya wanaanza kufukuzana maofisini tena mbele ya wageni ambao ndiyo mnawaheshimu wakiwemo wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia wawekezaji naomba nigusie ushuru unavyotolewa katika bidhaa zinazotoka nje ukilinganisha na bidhaa ambazo zinakuwa *manufactured* nchini. Serikali yetu imekuwa na tabia ya kutokujali wawekezaji wa ndani au *manufacturers* wa ndani

wakiwemo wenye viwanda na matokeo yake huweka *tariffs* za ushuru sawa na bidhaa ambazo zinawekwa na hawa wanaoitwa wawekezaji kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu unawavunja moyo wenye viwanda nchini. Utaratibu huu unawafanya wenye viwanda waingizwe kwenye ushindani ambao siyo wa lazima (*unfair competition*) na hawa watu ambao wanaitwa wawekezaji lakini ukweli wenyewe siyo wawekezaji kwa sababu maana ya kuwa mwekezaji ni kuleta pesa zako uka-*invest*. Hawa watu wanaoitwa wawekezaji na ninaposema wawekezaji kwa Mtanzania wa leo maana yake anafikiria yule aliyetoka Ulaya au Marekani ndiye mwekezaji. Hatuna utamaduni wa kufikiria kwamba tuna wawekezaji wetu makini ambao wapo nchini na tumeshindwa kuwapa *support* au kuwasaidia ili waendeleze biashara zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwamba hawa siyo wawekezaji kwa sababu wakija hawaleti fedha isipokuwa wanakuja kutumia fedha zetu wenyewe. Hawa ndiyo wanapata access ya mikopo benki bila hata dhamana. Hawa ndiyo wanaopata mikopo kwa masharti nafuu. Hawa ndiyo wanapata misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukifanya hivyo hawa wenye viwanda nchini, kwa mfano viwanda vya maji wanapozalisha maji kodi zao zinawekwa kiwango sawa na hawa walioleta maji nchini kutoka nje, matokeo yake ni kuwaondoa hawa kwenye biashara na hivyo kupoteza ajira, jambo ambalo limekuwa likilalamikiwa wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sioni haja ya kuendelea isipokuwa naweka msisitizo kwamba wakati sasa umefika Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iwe sikivu. Tunapotoa mapendekezo ama kutoka kwenye Kamati husika au kutoka vyama vingine vya Upinzani, naomba Serikali ijifunze sasa kuchukua mawazo bila kufikiria anayetoa hayo mawazo anatokea Kamati gani, anatokea chama gani cha siasa, vinginevyo Taifa letu tutaendelea kulididimiza kwa sababu tunaruhusu tofauti ambazo hazileti mantiki katika maendeleo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nishiriki katika mjadala huu ulio mbele yetu. Lakini kabla ya kuanza nitumie nafasi hii pia kuwapa heri ya mwaka mpya Watanzania wote na nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwamba sisi leo tuko hapa Bungeni tukiendelea kutekeleza wajibu wetu kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Waziri inavutia masikioni kwamba angalau sasa Serikali imeona umuhimu wa kuvihami viwanda vyetu. Lakini ningemshukuru sana Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha kama angekuwa mkweli zaidi kwanza akatwambia sababu iliyomfanya akaidi ushauri wa Kamati, kwa sababu suala hili lilitolewa ushauri katika Kamati. Wale ni Watanzania nadhani wanayo mapenzi tu kwa nchi yao lakini ushauri huo haukuzingatiwa. Leo ingekuwa vyema zaidi pia kama angetueleza ni hasara kiasi gani Taifa tumepata kutokana na ukaidi huo kwa sababu haitoshi tu kutuambia kwamba sasa tubadilisha ili maji yetu na bidhaa zingine ziweze kushindana wakati tayari miezi sita imepita ya hasara kwa utaratibu ambao hawezi kuutolea maelezo mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wasemaji waliotangulia wamesema huu ni usikivu lakini sina hakika kama kweli huu ndiyo usikivu kwamba umeshauriwa na Kamati ya Bunge ambayo ipo kwa mujibu wa sheria halafu umeamua kwa makusudi kwamba hutaki huo ushauri *down the line* miezi sita unasema; jamani sasa nimeleta hoja.

Niombe sana tuelezwe angalau kwamba sasa haya maeneo yanayopata hasara haya, posho, fedha kwenye makongamano, ununuzi wa magari, samani, gharama za uendeshaji, safari za nje na ukarabati wa majengo, vinakuwa *affected* kwa sababu ya ukaidi wa kusikiliza ushauri. Niseme tu kwamba si mwenendo mzuri. Tungependa sana Serikali yetu ielewe tu kwamba ushauri wa Wabunge hauna nia yoyote mbaya zaidi ya kuisaidia Serikali yenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tutakubaliana vizuri tu kwamba ipo haja ya kupunguza kweli huo ushuru kutoka hiyo shilingi 69 mpaka shilingi 12. Lakini najuiliza, kwa nini katika mtiririko huu huu na utaratibu

huo wa kuhami viwanda vyetu vya ndani, Mvinyo unaozalishwa hapa Tanzania unatozwa ushuru wa shilingi 420 kwa chupa na unaoingizwa kutoka nje unatozwa shilingi 122? Hivyo viwanda vyetu vitadumu? Hivyo viwanda vyetu vya Mvinyo hapa Dodoma vitadumu? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, basi katika kujumuisha hoja hii atuambie na ushuru wa Mvinyo aushushe ili hawa wenzetu wanaozalisha na wakulima wa zabibu hapa Dodoma wawe na uhakika wa soko la bidhaa zao hizo. Mbao zinazoagizwa kutoka nje ushuru wao mdogo kuliko mbao zinazozalishwa hapa nchini. Nani ataendelea kupanda miti kama mbao kutoka Msumbiji na Malawi zinazuzwa kwa bei ya chini hapa nchini kuliko zinazozalishwa hapa hapa kwetu? Niombe sana haya ni maeneo machache tu ambayo yanaonekana kwamba lazima na yenyewe yafanyiwe kazi.

Sasa hivi pale Mufindi watu wamepewa vibali vya kuvuna wameshindwa kuvuna kwa sababu ushuru unatozwa kwa mbao zinazotoka Malawi na Msumbiji uko chini sana, soko Dar es Salaam linachukua mbao za kutoka nje na wanaziacha zile za kwetu zinazozalishwa Mufindi na hii haitii afya katika uchumi wetu. Lakini utaratibu mzima wa ukusanyaji bado mimi nauona uko legelege. TRA wanaangalia tu vyanzo vilevile na kuvifanyia marekebisha muda wote na wigo wa mapato haupanuki. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, liko hili suala la vitambulisho vya Taifa. Vitambulisho vya Taifa pamoja na faida zake zingine lakini kubwa zaidi nadhani ni ile ambayo itasaidia Serikali kuwa na taarifa za walipa kodi zilizo sahihi kote nchini. Tulimsikia Waziri wa Mambo ya Ndani anasema mwezi wa Aprili, Mungu akitujalia vitaanza kutolewa, sasa vitaanza kutolewa kwa nani ndio tatizo langu. Kama sikosei Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani alisema vitambulisho hivyo vitaanza kutolewa kwa wafanyakazi wa Serikali. Naomba niishauri Serikali kwamba hebu iachane na wafanyakazi wake kwa sababu hawa wanajulikana wanavyo vitambulisho na kodi wanalipa *at source* huko huko, vitusaidie kupanua wigo wa walipa kodi. Leo walipa kodi wanaofahamika kwa idadi ya TIN zilizoko TRA wachache sana hata asilimia 20 ya Watanzania hawafiki, wengine wamo tu wanaendelea wanaishi wanapata vipato hawalipi kodi. Mimi nadhani vitambulisho vingeanzia huko kwa wale ili wigo wa ukusanyaji upanuke, uwafikie watu wengi zaidi ambao leo hawako katika mfumo rasmi wa ulipaji kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, TRA urasimu wapunguze. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed anasema TRA wamekusanya asilimia 102 sawa kwa malengo yao, lakini hiyo haitoshi, haimaanishi kwamba mahitaji ya Serikali na yenyewe yamekuwa *surpass* kiasi hicho hicho. Maana yake katika kukusanya hizo asilimia 102 wahisani wale washirika wetu wa maendeleo hawajaleta fedha wameleta siji asilimia 40 tu.

Kwa hivyo, kwa sababu bajeti yetu bado tegemezi kwa kiasi kikubwa namna ile hata wangekusanya asilimia 140 bado Serikali hii ingeendelea kuonekana fedha haitoshi. *No wander* Mheshimiwa Missanga amelalamika jambo la kusikitisha kweli kwamba leo tuko katika *quarter* ya tatu ya mwaka wa fedha ya Serikali, fedha ya maendeleo iliyotolewa katika Halmashauri zetu asilimia 20, 21. Sisi wana-CCM tunazidi kunyong'onyea tu kwa sababu kwa utaratibu huo ilani haitekelezeki inatuuma kweli. Tumefanya ahadi kalenda inasoma siji tutasemaje kwamba hatukuzingatia ushauri wa Kamati. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana ndugu zangu kwamba mapato yakusanywe kwa usahihi na ule urasimu ulioko katika ile Idara yetu ya kukusanya kodi upungue. Saa 24 walizosema wanafanya kazi ni wao peke yao, bandari inafungwa, hizo saa 24 wanafanya na nani? Maana yake tungetegemea kwamba forodha kama wanafanya kazi saa 24 basi na taasisi zingine ambazo ni washirika wao na wao wanastahili wafanye kazi saa 24. Lakini sasa inakuwa kwamba wao wanajikita wanafanya kazi saa 24, lakini wenzao wale ambao wanawa-*facilitate* kazi zao hawako kazini. Hivyo inaweza ikaonekana mwisho wa siku ni kwamba ni utaratibu wa kulipana posho. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwa kumuomba sana Mheshimiwa Mkulo atakapokuwa anafunga hii hoja atuambie kama bidhaa hizo chache nilizozitaja nazo zitaingizwa katika utaratibu huo. Nakushukuru sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dokta Charles Tizeba. Kama nilivyokwisha kuhidi Mheshimiwa William Mchimwa atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Lulida. (Makofi)

MHE. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nipate nafasi ya kuchangia. Ni kweli kabisa nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha Azimio hilo. Nianze kwa kutoa *declaration* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana kabisa na Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwamba yale ambayo yamesomwa hapa ndani ya Bunge ya Kamati yetu ndivyo tulivyokuwa tumeamua na ndivyo awali tulikuwa tumeishauri Wizara. Kwa bahati mbaya Wizara ilikuwa imeendelea na kuweka shilingi 69 katika maji, ilikuwa kinyume na ule ushauri tuliokuwa tumewapa. Lakini leo tunafurahi kwamba wamebadilisha baada ya kuona athari kama tulivyokuwa tumeshauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba nichangie katika mambo matatu. La kwanza ni kweli tulishauri Waziri kwa kupunguza kutoka shilingi 69 na kuja kuwa shilingi 12 kwa lira basi atafute maeneo ambayo punguzo hilo litafidiwa. Katika mapendekezo yake aliyoyasoma hapa Bungeni ni kwamba pamoja na mambo mengine anaelekeza vilevile kupunguza gharama za uendeshaji wa ofisi, mafunzo ya ndani pamoja na ukarabati wa majengo. Inapendeza kama huko kunakopunguzwa kulikuwa kuna ziada au kulikuwa hakuhitajiki. Kwa maana nyingine tunatarajia vilevile kutokana na athari na tungepata picha athari hizo kama zipo kutakuwa na athari gani. Lakini ingependeza vilevile kwamba kila kilichoelezwa kwamba kitapunguzwa pengine kitapunguzwa kwa kiwango gani tuone kitakwimu namna kitakavyoainishwa na punguzo kubwa lililodhamiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili ni suala zima ambalo linasemwa kiujumla kwamba Serikali inaonekana ina mapato mengi kulingana na ripoti ya *TRA*. Sisi kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi tumeomba tupate takwimu kiundani kitu gani kinatokea. Ikiwa *TRA* inaripoti makusanyo mpaka asilimia 102, lakini hakuna fedha zinazowasilishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Halmashauri lazima kuwe na tatizo la msingi na sisi kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi tuliomba tupate maelezo ili tusaidie namna ya kushauri, maelezo ambayo tunatarajia tutapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitazama vilevile utekelezaji wa bajeti ya maendeleo hasa katika ahadi za wahisani. Mpaka Desemba tumeona kwamba utekelezaji ni asilimia 23 tu katika ahadi zote maana yake hakuna miradi ya maendeleo inayopata fedha katika fungu la wahisani ambalo walikuwa wameahidi. Tunahitaji kutazama kitu gani kinatokea ili tatizo kama lipo ambalo tayari tunaliona kwa dalili tuweze kulitatu hatuwezi tukakaa tukiona kwamba fedha inaingia kwa wingi kitakwimu, lakini kimatumizi haielekei inatumika namna gani. Kwa hivyo, hili sisi kama Kamati ya Fedha na Uchumi tulishakuwa tumeomba maelezo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili la msingi kabisa ni suala la mfumuko wa bei ambalo na wenzangu wameeleza. Tumeona kwamba sasa hivi ukitazama, ukinyambua ile *analysis* ya vitu gani vinavyosababisha mfumuko wa bei kitu kikubwa kinatokana na chakula ambacho kinafikisha mpaka karibu asilimia 50, lakini nchi hii ina chakula tatizo ni mfumo wa masoko ulio dhafi sana katika Tanzania. Inakuwaje chakula kinakuwa kingi sana sehemu moja ya nchi mpaka dakika hii tunakuwa na matatizo ya bajeti ya kununua kile chakula wakati tulinamasisha sisi wenyewe na tokeo hilo likasababisha mfumuko wa bei wa *food inflation* ikapanda mpaka karibu asilimia 50 na kuchangia athari kubwa sana katika gharama zote za mfumuko wa bei ikiongozwa na chakula, chakula ambacho tunacho hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tulipochambua tukaona kwamba kinachofuata ni kweli ni gharama ya mafuta, lakini chini ya mafuta kuna mafuta ambayo ni ya chakula, kama alivyoeleza Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Fedha na Uchumi gharama ya mafuta ya chakula ni kubwa sana ambayo tunaagiza nchi za nje kwa kutumia fedha zetu za kigeni wakati mafuta ya chakula tuna mazao mengi ambayo tunalima hapa hapa nchini na tungeweza tuka-process na kupata mafuta ya kutosha tukaepuka uagizaji wa mafuta kutoka nchi za nje ambao unachangia katika *inflation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi hili ni suala la kiseru, ni suala la kuweka mkakati ili kuhakikisha kwamba tunaepukana na mwenendo huo wa mfumuko wa bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni vivutio vya uwekezaji. Takwimu tulizonazo tuna uwekezaji chini sana ulio dhifu katika kuelekea kuhamasisha uwekezaji wa ndani. Tumekuwa tukizungumza kwa mapana na marefu sana juu ya namna gani tunaweza tukapata uwekezaji wa nguvu kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli lakini wote hata tukatembea dunia nzima wanajua kwamba mahali ambapo pana miundombinu hafifu haiwezekani wakavutika wawekezaji wakaja mahali ambapo pana *cost of doing business* ipo *very high*, kuna umeme ghali sana haiwezekani wawekezaji wakafika na tukategemea watawekeza. Mahali ambapo uwekezaji haujahamasisha kulenga ambao ndio walio wengi nchini basi hali halisi ya uwekezaji na ukuaji wa uchumi katika nchi utakuwa mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kitu kimoja kikubwa tutazame sasa uwekezaji wa ndani kwa *seriousness* inavyohitajika. Uwekezaji wa ndani una matatizo sawa wa miundombinu kama wanavyosema wanaokuja kuwekeza wanaotoka nchi za nje. Tuna tatizo vilevile la gharama, la kufanya biashara kubwa kuliko sehemu zingine na vilevile zinazochangiwa kwa sababu ya umeme.

Lakini kitu kikubwa tutazame sera ambazo zitasaidia uwekezaji huu uelekezwe kwa vijana walio wengi katika vijiji, namna gani vyombo vya fedha (*financial institutions*) zinavyoweza zikahamasishwa kwa utaratibu wa *tax system* wao wakaelekea kuwekeza katika maeneo ya *agriculture*. Tusipofanya hili kwa juhudi kubwa uwekezaji katika Tanzania kutoka ndani utaendelea kuwa duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nikizungumza hili kwa muda mrefu, lakini hilo ndivyo ninaloliona hatuwezi tukulikwepa ikiwa asilimia zaidi ya 70 ya wananchi wa nchi hii wapo vijijini na hatujawa na programu ya kuwawezesha kikamilifu kabisa. Tuna mifuko ya hapa na pale, lakini mifuko yenyewe haijawa *proper distracted, financial system* ya nchi ikiwa *addressed* itasaidia sana kusaidia kundi hili likabadilika kiuchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo ninachoomba tuje na sera za ushawishi katika *system* ya mabanki, mabanki yale yatakayokuwa tayari kuwekeza kwa maana ya kusaidia vijana na wananchi walio vijijini hao ndio walio wengi. Sera hizo za fedha ndizo zitakazotusaidia kukwamua ukuzaji wa kilimo ambacho ni *agricultural based*. Kilimo ambacho tunazungumza kwamba ndio *agro based industries* haiwezekani ikiwa ulimaji wa msisitizo huo wa uwekezaji hatujaupa nguvu ya kutosha.

Pili, mfumo wa masoko ambao tunakuwa na vyakula nchini na vikaoza, vikaharibika na tukawa sehemu ya ku-discourage wazalishaji wakati tuna chakula nchini tuutazame upya ili tuwe na vyote viwili, *financial system* kielekea kusaidia walio wengi na pili mfumo wa masoko ukiwa umetazamwa utakaokuwa na ufanisi wa kutosha kwamba vinavyozalishwa mara moja vinafika mahali ambapo kuna mahitaji yaani *from the supplies side* kwenda kwenye *demand side* kuwe na *system* iliyo *very efficient*. Tusipolizingatia hili kwa muda mrefu tutaendelea kuwa na tatizo ambayo kiutaratibu ni *structure* tu na linatufanya tuwe na *weak economic management* kwa sababu ya mambo haya mawili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema mchango wangu ni huo na naunga mkono hoja ya Waziri, lakini vilevile naomba ushauri huu uzingatiwe ili mwelekeo wa uchumi wa watu walio vijijini ambao walio wengi uweze ukakwamuka. Ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa William Mgimwa. Mheshimiwa Riziki Lulida atafuatiwa na mchangiaji wetu wa mwisho nadhani Mheshimiwa Henry Shekifu. (Makofi)

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia na mimi kupata nafasi ya kuweza kuchangia siku ya leo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa leo wakati Mheshimiwa Missanga anatoa hoja ya fedha za maendeleo katika Halmashauri huwa hazipo kwa kweli nimesikitishwa sana. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya LAAC tukiwa katika Kamati ya LAAC tulisikitishwa kuona tunapata waraka ambao unatoa maelekezo katika Manispaa ya Mtwara wasichukue ushuru kwa wanunuzi wa korosho ambao umewaingizia hasara ya shilingi bilioni tatu, kwa kweli nitaileta ile barua muone kwa uhakika kwa hili ninalozungumza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumzia Halmashauri zetu zimekuwa katika mazingira magumu, zinashindwa kujiwezesha, kujipatia kipato cha kujiendesha katika on source zake, lakini anatokea mtu anaandika barua hamna ruhusa kwa wale wanaokuja kununua mazao kutoza ushuru wa shilingi 30 ambao ungeuingizia Manispaa ile fedha shilingi bilioni tatu. Hii sio Mtwara tu tumekwenda katika Halmashauri ya Kilosa katika uwekezaji wa shamba la miwa Kilombero Ilovo wao vilevile wamepata waraka ambao mwananchi ndio atozwe ushuru, lakini yule mwekezaji hana ruhusa ya kutozwa ushuru, matokeo yake Kilosa tumeipatia Halmashauri yetu hasara ya shilingi 844,000,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuja Mvomero hivyo hivyo, sasa tumefikia mahali tunajiuliza hawa watendaji wana nia nzuri na nchi yao au wameamua kwa makusudi kuiweka nchi katika mazingira magumu? Hayo nimekupa sehemu mbili lakini inaonekana sehemu nyingi wana matatizo kama hayo. Kuna mchanganyiko kati ya watendaji na baadhi ya Manispaa kupewa waraka kabisa msifanye hili, msifanye hili hiki ni kiburi cha aina yake. Hilo nikitaka kutoa kama angalizo ambalo matatizo ambayo unasema Serikali tunashindwa kukusanya ushuru, wengine wanazuia kukusanya ushuru na hiyo barua nitaileta na hii imetoka ndani ya Kamati yetu ya LAAC kuonyesha kabisa kwamba watu hawana uzalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia suala la viwanda vya korosho katika mikoa ya Pwani ya Tanzania. Tulikuwa na kiwanda cha korosho Masasi, Newala, Mtwara, Lindi mpaka Kibaha na Mbagala, wawekezaji wakajifanya wanataka kuchukua vile viwanda kwa ajili ya uwekezaji wa korosho. Kwanza ingeleta faida ya kupata ajira kwa wananchi wa maeneo hayo ili angalau zile korosho zingebanguliwa katika viwanda vyao wakafaidika na ajira. Pili, soko la ndani lingefanya kazi maana yake bado tuna walaji wakubwa wa korosho ambao wanazihitaji korosho Tanzania hii. Lakini pameingia ukiritimba ambao mpaka sasa hivi sielewi ni kwa nini vile viwanda havifanyi kazi matokeo yake wananchi wameitikia wito wa kuzalisha korosho zimekaa katika mikono ya wananchi hali ya umaskini inazidi kuwa kubwa. (Makofi)

Nikijijuliza ni nini, hatuna wataalam ambao wanatoa ushauri mzuri wa kutusaidia nchi hii na sisi tukaweza kuvuka? Kwa kweli hii inasikitisha. Tunarudia tena, Watanzania turudi katika uzalendo na turudi katika kuipenda nchi yetu. Tumefikia mahali nchi ina utajiri mkubwa, lakini tunazidi kurudi nyuma kuwa maskini. Mazao yetu ya Tanzania yanauzwa nchi ya jirani, wanaonekana wao wa nchi za jirani ndiyo wanauza haya mazao ambayo hata wao hawalimi na wala hawana katika nchi zao. Lakini sijaelewa huyu mdudu ameingia wapi Tanzania mpaka ametufanya sisi tumekuwa maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Lindi ni mmoja wa Mikoa ambayo unalima ufuta na karanga na katika historia niliyonayo tulikuwa na reli ambayo ilikuwa inatoka Mtwara mpaka Nachingwea. Ile reli ilijengwa makusudi kwa ajili ya kwenda kuchukua korosho, karanga na ufuta ambavyo vinapatikana mitaa ile. Bahati mbaya sielewi ile reli iling'olewa, lakini bado ufuta tunao na karanga tunazo za kutosha. Viwanda vyetu vya mafuta mpaka leo amekuja mwekezaji, amezima zoezi la kutengeneza mafuta, katika hayo maeneo ajira hakuna, karanga zinazoza na ufuta wote unaopatikana Kusini unapelekwa nje, tunaletewa mafuta machafu. Haya mafuta yanamsaidia nani? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakula mafuta Tanzania ambayo ubora wake hatujui na tunapitisha lakini tunaacha ufuta ambao unalimwa Tanzania ambao ni safi ungefanya kazi ya kutengenezwa hapa Tanzania, nafikiri tungekula mafuta ya kutosha na tukapata mafuta ambayo ni masafi, hayana cholesterol na yakawa na afya bora kwa wananchi. Hata haya vilevile hamyaoni?

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na *ginnery* za pamba kwa Mikoa yote ambayo inalimwa pamba, tukawa na alizeti Tanzania, lakini je, viwanda vile vilivyokuwa vinatengeneza mafuta ya pamba viko wapi? Vina msaidia nini Mtanzania? Lakini matokeo yake tunaletewa mafuta machafu hata yanakotoka hayajulikani na saratani sasa hivi Tanzania pengine inaongezeka kwa ajili ya kula vitu ambavyo havieleweki. Naomba Tanzania tujirudishe katika hali yetu ya kuipenda nchi yetu angalau tuyaone yale matatizo ambayo Tanzania yanatuzingira. Lakini ni sisi wenyewe wa kujilaumu na tutakuwa kila siku tunajilaumu, lakini kama huna moyo wa kujipenda wewe mwenyewe, basi hapa hakuna tatizo la kufanya, itakuwa ni ugonjwa ambao inabidi urudi Makanisani na Miskitini uombewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kuna mfumko mkubwa sana wa bei za vyakula. Wananunua mchele mzuri wa Tanzania wanapeleka nje, tunaletewa mchele mbovu lakini bei yake sasa hivi mchele Dar es Salaam kilo shilingi 2,700/= Tutapunguza tozo la maji, sawa. Hiki chakula ambacho mwananchi

ndiyo kila siku anahitaji ale. Atapata faida gani kwa bei ya shilingi 2,700/=, ina maana chakula hiki kinawasaidia kundi la watu wachache ambao wanaweza kufaidika nacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Waziri aliangalie suala la mfumko wa bei ya chakula hasa mchele, unga wa sembe na ngano, vipunguzwe bei pamoja na sukari na chumvi ili tuweze kuwapunguzia mzigo mkubwa waliokuwa nao wananchi wa Tanzania. Pia kipindi cha msimu wa chakula ijiwekee mikakati kuhakikisha chakula chote tunachokivuna Tanzania kitunzwe kwa ajili ya faida ya Watanzania. Sio kuchukuliwa chakula kizuri kupelekwa nje halafu kinaletwa chakula kibovu ambacho hata kwa binadamu wa kawaida hakimfai, ni chakula cha wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli inanisikitisha kuona hali ya viwanda vyetu imefikia hapa, vyakula vyetu na mazingira kwa ujumla lakini wataalam wanaviona na wanashindwa kutoa ushauri mzuri ambao unaweza kuipelekea nchi hii ipate nusra kutokana na hali hii. Mikoa ya Pwani yote tunavuna chumvi, lakini soko la chumvi limekuwa gumu. Katika tafiti zangu nimeona chumvi inavunwa karibu Mikoa mingi Tanzania mpaka Kigoma, lakini uingizwaji wa chumvi nchini ni mkubwa wakati yetu imekaa haina soko. Je, hawa wananchi wadogo wadogo ambao wanachukua mikopo ya chumvi na mikopo mingine ili wajiendeleze kibiashara, wananufaika vipi na uletaji wa chumvi nyingi kutoka nje? Hivyo kwa hali hii, naona tufikie mahali wataalam turudi, tuwasaidie wananchi wetu ambao wametusaidia kutufikisha hapa kwa kutusomesha, sasa na wao tuwawekee mazingira wanufaike na hali ngumu ya uchumi ambayo inakwenda katika hali hii. Turekebishe mazingira ambayo yatatufanya na sisi vilevile wale watu watuone kuwa tumekuja kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. (Makofi)

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ambayo inaonekana kama ni ya mwisho na nianze pale ambapo wenzangu wamemaliza na hasa pale ambapo Kamati ya Fedha na Uchumi ilimalizia katika kifungu chake cha 1(10). Kamati ilisema; "Kamati yangu inakubaliana na azimio lililowasilishwa na Waziri wa Fedha na hapo hapo inasisitiza kuwa ili kuliongeza Taifa mapato yake na kuimarisha uchumi wake, maeneo mengine yaangaliwe kwa umakini na hatua za haraka zile za kisheria, kisera, kodi na ushuru, taratibu na kadhalika zichukuliwe ili kuibuha uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira yangu inanisuta kidogo katika suala hili. Kwanza nakubaliana na hoja ya kupunguza ushuru na pengine hapa nitangaze rasmi kwamba na mimi ni katika wale wazalishaji wa maji. Lakini sikutumia njia yoyote ile kuiomba Serikali, umuhimu waliuona wenyewe. Katika hili nianze kwa kusema maji ya chupa ni sahihi, lakini kwa kweli gharama kubwa ya maji ni kile kifungashio, chupa yenyewe sio maji. Kwa hiyo, ukisema maji unayapunguza ushuru kwa kweli unapunguza ile gharama tu ya kifungashio ambayo hata kama ukipunguza huyu anayeweka bei atazingatia alivyoagiza kifungashio.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa yapo maji yaliyokuwa yanatumiwa sana na mtu wa chini ambayo gharama yake kutokana na kifungashio ilikuwa ndogo. Yale maji ya viloba yalifutwa, lakini nakuhakikishia yamerudi kwa njia nyingine, kwa lugha inayoitwa samahani kwa lugha hii, nitaizungumza lakini ndiyo ukweli wa mjini, yanaitwa nipatie maji ya kondomu. Maji yale yanauzwa kwenye viloba ambavyo vinazibwa kwa kutumia mshumaa au taa na yanauzwa kwa wingi kwa sababu watu wetu hawana uwezo wa kununua haya maji ya chupa. Sasa naishauri Serikali na kuiomba ili angalie suala hili kwa undani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nisiendeleo katika hilo, nje katika hoja tunayoizungumzia. Sikubaliani kabisa na suala la kufuta vifungu vya matumizi yanayotokana na mapato ya maji. Nimekuwa Kiongozi wa Serikali, naelewa unapoiambia Serikali unafuta mapato au unafuta matumizi ni rahisi kusema, lakini kutekeleza ni ngumu sana. Maeneo yote ambayo yanafutiwa matumizi ndiyo kwa kweli injini ya kusimamia Serikali, ndiyo nyenzo muhimu. Ukifuta *other charges* huyu kiongozi atakwendaje kufanya kazi? Ununuzi wa magari, ununuzi wa vifaa vya kutendea kazi, unamfutia huyu atatekelezaje kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi kulikuwa na *test question*, swali la msingi lililotustua kwamba fedha hazijapelekwa kwenye Halmashauri na zilizokwenda hazikusaidia. Leo tunakubaliana tupunguze

matumizi na unamwambia mtendaji wa Serikali kwamba sitakuletea hiki. Nafikiri ni jibu rahisi kwa swali gumu sana. Sisi kama Wabunge tukalikubali hili utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi itakuwa hovyoya sana. 2015 tutakuwa katika hali ngumu sana. Naiomba Serikali na Waziri tumwagize Waziri wakakae, watafute vyanzo vingine vya mapato. Yako maeneo ambayo Serikali ikikaa, dhahiri ikiangalia mapato yatapatikana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kungeza ushuru wa bidhaa ambazo sio muhimu. Kuna maji haya ambayo tunasema yanatoka nje kwa nini msiongeze ushuru? Kuna vitu vingi, mitandio vinakuja Dar es Salaam, ukienda kuviangalia vina *expire* kesho kutwa, kwa nini hamuongozi ushuru? Vitu vingi sana vinaletwa na Wachina na ukiviangalia thamani yake kwa uchumi wetu ni ndogo sana. Ndiyo vinakidhi haja lakini kwa nini haviongezewi ushuru ili tupate mapato? Lipo tatizo leo la kutoa fedha za kigeni hovyoya hovyoya. Hakuna udhibiti wa kutosha. Fedha za kigeni zinapatikana lakini hawa wenye kuleta bidhaa zao wanakwenda kuzichota kwenye *Bureau de Change* na hakuna udhibiti wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama wewe unatafuta fedha za kigeni leo zinatoka hovyoya, hakuna nchi duniani ambayo kuna urahisi wa kutoa fedha za kigeni kama Tanzania. Tunachukua taratibu gani za kudhibiti maduka haya. Lakini haya mapato ya fedha za kigeni ndiyo yanaongeza kushuka kwa thamani ya shilingi kwa sababu kila hela inapopatikana, wanainunua itoke nje. Matokeo yake thamani ya shilingi kila siku inashuka. Naamini Serikali hawaliangalii suala hili vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo tutaambiwa wiki ijayo, sijui tutasemaje. Lakini naamimi kuna mambo ya msingi yakisimamiwa yataongeza mapato, lakini wakati huo huo yatadhibiti uchumi uwe na nguvu. Tuna matatizo ya ku-export bidhaa kwenda nje na *seriously* hatujali-address suala hili la *export incentives*. Maana kama hujapeleka bidhaa nje siku zote utakuwa na tatizo kwa sababu kwa vyovyote kuna mahitaji. Kamati imesema sisi tumeingiza bidhaa za trilioni tano, wakati tumeweza ku-export trilioni tatu. *Deficit* ile ya trilioni mbili ni lazima kwa vyovyote italetwa madhara. Sasa tumejizatiti vipi kungeza mapato yetu ya fedha za kigeni. Haya ni masuala ya msingi ambayo tuya-address katika uchumi. Bila kuyafanya haya tutaendelea kulalamika, mfumko wa bei utaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala lililosemwa hapa la mfumo wa masoko ndani. Kwa upande wa Kaskazini kulikuwa na soko zuri sana la ku-export mahindi. Kusini mahindi na mpaka leo ninavyozungumza mengine hayajatoka kwa wakulima. Leo Kaskazini inataka kutoa na tungeweza kupata fedha za kigeni na nilishauri kwamba jamani sikilizeni; kama wenzetu Wakenya wana matatizo undeni soko njiani. Hapo hapo na watu wa *TRA* wanakusanya kodi na mapato na mahindi yanatoka. Nunueni mahindi yaliyoko Kusini yaliteni huku, tutaweza kuijenga nchi hii. Lakini sasa mambo haya yanachukua muda mrefu, Waziri wa Fedha na Serikali tuko wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naogopa sana kwa sababu maamuzi ambayo ni dhahiri yanaweza kusaidia uchumi yanachukua muda mrefu kuamuliwa matokeo yake ndiyo hapa sasa kila mtu ananung'unika. Viongozi tunanung'unika, wananchi wananung'unika, tunakwenda wapi? Kwa hiyo ushauri wangu katika hili naomba sana na namaliza kwa kusema dawa hapa si kukata matumizi, maana tutaifanya Serikali isiweze kumudu kazi zake. Waziri nenda katafute maeneo mengine ya kupata mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui Kamati ya Fedha ilielewaje kuambiwa tunakata matumizi, Waziri anatamka tu kwamba tunakata matumizi haya na haya wakati ukweli uliopo ni kwamba mpaka sasa hivi Halmashauri zina athari kubwa sana za kutokupata fedha kutoka Serikali Kuu. Sasa, hivi sisi Wabunge wote tukikubali kitu batili ambacho kitatuletea matatizo kesho, tutakwenda kwa watendaji tutashindwa kuwadhibiti kwa sababu hatukuwapa nyenzo na sisi ndiyo tunaishauri Serikali na kuisimamia Serikali. Katika hili, nasema tumrudishe Waziri akaliangalie kwa kutafuta vyanzo vingine vya mapato ambavyo vitaweza kuchangia suala hili ili Serikali isiwe kiwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo. nikushukuru sana na naiomba Serikali kwa kweli kwa dhati kabisa bila kinyongo chochote, kafikirieni njia nyingine za kupata mapato badala ya kukata matumizi kwa upande wa Serikali wakati matumizi hayo hayatoshi. (Makofi)

MHE. SELEMANI S. JAFU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa ya mchana huu wa leo kwa ajili ya kuchangia Azimio hili muhimu kwa ajili ya mustakabili wa

nchi yetu. Pia naishukuru Serikali kuona kwamba ni vyema Azimio hili limekuja hapa ilimradi Wabunge tuweze kulijadili. Lakini kubwa zaidi ni suala zima na ajenda kubwa ni bei ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napata utata kwa sababu tuliongeza bei ya maji, sasa tumeshusha na tumeshusha mara baada ya kuona madhara yake katika matumizi kwani watu wa kawaida wanashindwa kupata maji safi na salama. Lakini kwa taarifa inajionesha dhahiri kwamba Tanzania bado tunaingiza maji kutoka nje. Ndugu zangu moja kwa moja tuseme hii ni aibu. Ni aibu kwa sababu tuna viwanda vinatengeneza maji hapa nchini, lakini bado kuna maji yanaagizwa na ina maana kwamba hatujafanya *commitment* ya kutosha kwa ajili ya kulinda viwanda vyetu vya ndani. Hii ina maana kwamba tunaathiri kwa kiwango kikubwa ajira za vijana wetu ambao jana tulikuwa tunataka mjadala mpana hapa wa jinsi gani ya kutatua tatizo la ajira katika nchi yetu. Naomba Mheshimiwa Waziri urejee moja kwa moja kwa nini tusiongeze kodi kwa maji yanayoagizwa hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kinatupa kikwazo, tunaogopa nini. Jambo hili linatutia mashaka mpaka kuna watu wengine wakawa na wasiwasi na sisi, inawezekana huenda tukawa na maslahi katika hayo maji yanayotoka nje. Naiomba sana Serikali kwanza ikiwezekana tukapunguza bei ya maji ndani, lakini hali kadhalika tuongeze bei ya maji ya nje ili mradi tu-*discourage* kitendo kizima cha kuazima maji kutoka nje. Lakini ndugu zangu siku zote tunazungumza kwamba thamani ya shilingi kila siku inashuka kwa sababu tunaagiza zaidi kuliko tunavyo-*export*. Kama maji tunaagiza, kama *furniture* tunaagiza, kila takataka tunaagiza, jamani *demand* ya dola *obviously* itakuwa kubwa kuliko iliyokuwepo. Ndiyo maana thamani ya shilingi yetu kila kukicha tunalalamika thamani ya shilingi inashuka. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana katika hili la bei ya maji, japo tunapunguza maji ya ndani, lakini hali kadhalika ikiwezekana tuongeze bei ya maji tunayoagiza kutoka nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, bahati nzuri Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha amezungumza wazi kwamba, tunaagiza mafuta ya kula kwa kiwango kikubwa kwelikweli. Mamilioni ya pesa yanatumika kwa ajili ya kuagiza mafuta ya kula hapa nchini. Ndugu zangu tuagize mafuta ya magari na mitambo, lakini hata mafuta ya kula tunaagiza na tunatumia pato la Taifa kwa kiwango kikubwa sana. Hali hii haiwezi ika-*stabilize* thamani ya shilingi ya Tanzania. Hili naomba ndugu zangu mlione kwa wazi kabisa wala halina kificho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika kuna mianya mingi kwenye Tanzania yetu hii na inasababisha kwamba hata upatikanaji wa mapato umekuwa ni tatizo. Ukiangalia bidhaa tunazoagiza kutoka nje zingine hazina hata sababu. Ukienda kwa wadau wa maziwa wandalamika, ukienda *supermarket* zote hata hapa Bungeni ukienda pale nje, hata haya maziwa tunayotumia sasa hivi yote yanaagizwa kutoka nje wakati sasa hivi Tanzania tuna ng'ombe wengi, ilitakiwa kufanya utaratibu mzima kwa jinsi gani hizi rasilimali za nchi yetu ziweze kutumika vizuri. Vitu hivi vyote maana yake tunaagiza kwa fedha za kigeni ndiyo maana shilingi inashuka kila siku, uchumi unaporomoka, hali kadhalika nchi yetu itakuwa katika hali mbaya zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia suala la OC. Bahati nzuri mzungumzaji wa awali ameshasema. Sasa hivi Halmashauri zetu zitafika muda hali ita-*stuck*. Maana yake hata mtu kufanya *monitoring* ya miradi itashindikana. Tukumbuke tulipopita katika bajeti yetu ya Serikali. Bajeti zote katika Wizara zote imeonekana kwamba gharama za matumizi haya imekua ni ndogo kwelikweli. Tumepitisha bajeti ile OC pale awali zilikuwa zimepungua sasa hivi ina maana kwamba tuna ajenda nyingine ya kupunguza hizi OC, nini maana yake? Maana yake ni kuwafanya watendaji wa Serikali wasiweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tulioko Vijijini, ina maana mnataka kusababisha hata watendaji wa Serikali washindwe kuibua miradi na hii inasababisha hata miradi mingine kuwa mibovu. Jengo linaweza likianza mpaka linamalizika, *Engineer* hajakwenda kukagua kwa sababu hana mafuta ya kwenda kutembelea mradi huo. Hili jambo nasema haliwezekani. Katika hili, Mheshimiwa Waziri nikushukuru sana kwa sababu ajenda hii imekuja hapa kwa sababu ya suala zima la kuokoa walaji wetu wa Tanzania ambao wengi ni wanyonge kwamba bei ya maji ishuke. Lakini, naiomba sana Serikali iangalie sehemu nyingine mianya ambayo inasababisha kwamba hali yetu iweze kuwa mbaya na uchumi uzidi kuwa katika hali ambayo si nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke ndugu zangu sasa hivi, ukitembelea sehemu zote za miji yetu tumekuwa kama ndiyo *dustbin*, kila kitu kinakuja nchini kwetu hapa. Nina wasiwasi sana jinsi gani tunaweka udhibiti wa hivi vitu vinavyoingia, maana tunaporomosha viwanda vyetu, tunaporomosha kila kitu kilichoko Tanzania. Lakini kila siku katika hoja tunatetea viwanda vya nchi yetu. Ndugu zangu hii jamani siyo *realistic*, lazima turejee upya kwamba tutafanyaje tuhakikishe kwamba hali ya uchumi wetu inakwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, tunapozungumzia maji maana yake tunazungumzia uchumi wa nchi. Naiomba Serikali kwa ujumla, hata ukiangalia gharama tunazotumia katika kuagiza mafuta kwa ajili ya mitambo mbalimbali imekuwa ni kubwa, lakini ukija kuangalia mafuta yale mengine yanasaidia katika suala zima la kuzalisha nishati ya umeme. Naomba tuharakishe mchakato mzima wa bomba la gesi. Tukiweza kupata umeme unaotokana na gesi, maana yake matatizo yote yanayowakabili wananchi yatashuka. Sasa hivi tunaona kwamba gharama ya umeme imepanda, japokuwa hoja inasema kwamba umeme uliopanda ni kwa ajili ya watumiaji wakubwa, hapana. Mtumiaji mkubwa maana yake anakwenda kuzalisha bidhaa, bidhaa itakapozalishwa maana yake itarudi tena kwa mtumiaji wa kawaida ambapo gharama ya bidhaa ile itakuwa ya juu kwa sababu gharama iliyotumika katika utumiaji wa umeme imekuwa ni kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mchakato wa pamoja tunapozungumzia hili, tuzungumzie uchumi kiupana zaidi, tuhakikishe kwamba waliopewa dhamana kuhakikisha kwamba bomba la gesi linatengenezeka, basi naomba tuweze kumaliza mradi huo ili tuweze kuleta unafuu kwa Watanzania. Hali sasa hivi ni mbaya, na lazima tukubali kwamba mwananchi wa kawaida anakuwa hoi, ni lazima tufanye kila sababu ya jinsi gani tutakavyomsaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, umesema niongee kidogo na mimi napenda kutumia busara yako, kabla sijagongewa kengele. Nadhani langu limefika. Ahsanteni sana. naomba kuunga mkono hoja hii, lakini haya yazingatiwe. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante, nakushukuru sana Mheshimiwa Selemani Jafo kwa mchango wako. Sasa mchangiaji wetu wa mwisho kabisa kwa dakika kama kumi hivi ni Mheshimiwa Zarina Madabida.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nitahakikisha nitazitumia dakika hizo hizo ulizonipa kwa sababu nina machache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba niipongeze Serikali kwa kuona umuhimu wa kulinda viwanda vyetu vya nchini. Hilo nawapongeza. Lakini, nilikuwa najiuliza maswali kwamba kuteremka kwa ushuru huu ambao nikichukua shilingi 69 ukatoa shilingi 12 zinazobaki, inapungua kwa shilingi 57 kwa lita. Shilingi 57 kwa lita, ukichukua chupa ndogo zile za 250mls, labda kuna punguzo hapo kama la shilingi 15. Ninajiuliza, kati ya watumiaji, tunajaribu kumsaidia nani? Maana katika kupunguza itapungua kama shilingi 15 kutoka 150 mpaka 135. Huyu mwananchi wa Kijijini tunayemsema kwamba tunajaribu kumpunguzia, ndiyo anayehitaji hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hilo siyo *concern* kubwa sana. *Concern* yangu ni ile nakisi ambayo inaletwa kwa punguzo hilo. Nakisi inayoletwa kwa punguzo hilo ni karibu bilioni 7.7. Sasa, nasema hivi, kweli ni sawasawa tukapunguza kupata mapato kwa bilioni 7.7 wakati tunajua *the end user* (mtumiaji wa mwisho) punguzo lake ni dogo sana kiasi kwamba hata kuliona pengine asilione. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kama tunataka kulinda viwanda vya hapa nchini, kitu ambacho naipongeza Serikali, kwa nini kwanza tusingeze ushuru kwa hizi bidhaa ambazo zinatoka nje? Lakini kama kuna umuhimu sana basi hata kuzipiga marufuku kabisa kwa sababu nchi zingine wanafanya. Kama viwanda vyetu vya nchini vinaweza kutengeneza maji kiwango ambacho kinakidhi mahitaji ya nchi, basi hakuna sababu ya kuagiza maji hayo. Njia hiyo ingekuwa bora zaidi kwa sababu tusingekuwa na nakisi moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile nakubaliana kabisa na Serikali kupunguza matumizi. Suala hili nakumbuka kabisa nililisema wakati nikichangia hotuba ya Waziri Mkuu wakati wa kipindi cha bajeti. Kupunguza matumizi, tunahitaji kupunguza matumizi ili kusudi tuweze kabisa kutumia hii nakisi ya bilioni 7.7

na huko kupungua kwa bilioni 7.7, tungepata bilioni 15.4 ambazo tungezitumia kwa mahitaji mengine muhimu sana. Sasa hivi tuna mahitaji muhimu. Tumesema kuna madawati ya watoto tunahitaji, hatuna, kuna mfumko mkubwa wa bei ambao tungeweza kabisa hata kupunguza bei za mafuta ya taa au *diesel* au ku-*subsidize diesel* ambayo ingepunguza bei ya vitu vingi kuchanganya pamoja na maji hayo kwa sababu usafiri wake ungepungua na hivyo kufanya hata yule mtu wa Kijiji akaweza ku-*afford* yale maji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napata shida sana wakati tunaposimama kuunga mkono hoja ya kupunguza shilingi 57, wakati hizi 57, nina hakika kabisa hazitokuwa na *impact* kubwa kwa mlaji wa mwisho. Kwa nini tusiache hivyo hivyo, tukatafuta jinsi nyingine ya kupunguza hii bei na vile vile tukaondoa hii nakisi ambayo itakuja kwenye bajeti yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo, naiomba Serikali na Wizara ikatafute mbinu nyingine, lakini, hii wasipunguze. Kusema kweli nasimama hapa siungi mkono hoja hiyo ya kupunguza hii bei kwa sababu nafikiri hatutakuwa tumempatia nafuu yoyote Mtanzania wa kawaida ambaye anatumia maji haya na hataiona *impact* yake. Nakuombeni ndugu zangu tuiangalie huko mbele, haitokuwa na *impact*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru sana kwa kunipa dakika chache. Ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Zarina Madabida. Ee...ndiyo Mheshimiwa!

MHE. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Kanuni ya 58, naomba hoja hii iondolewe ili Serikali ipate muda wa kuzingatia ushauri uliotolewa na Bunge. Naomba kutoa hoja! (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, hebu naomba utusomee hiyo Kanuni ya 58 ili twende pamoja.

MHE. WILLIAM A. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 58(1) inasema: "Endapo Mbunge anapenda kupendekeza mabadiliko yafanywe katika hoja kwa kufuata masharti ya Kanuni hizi, anaweza kutoa hoja yake ya kufanya mabadiliko wakati wowote baada ya hoja anayotaka kuibadilisha kutolewa, lakini kabla Bunge halijahojiwa liifanyie uamuzi".

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Bahati mbaya umewahisha shughuli, sijafikia mahali pa kuwahoji ili mmfanye uamuzi. Sasa, naomba nimwite Mheshimiwa Waziri aendelee na kutoa majibu. Tukifika wakati huo, kama mtakuwa bado mnahisi mna msimamo huo huo, basi unaweza kusimama tena na kuona nini tutafanya.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukrani za dharti kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Azimio la Kuridhia Amri ya Marekebisha ya Jedwali la Nne la Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 kwa kuzungumza humu ndani na wale waliochangia kwa maandishi. Sikutegemea kama hoja hii ingezua mjadala mzuri kiasi hicho, naona Waheshimiwa Wabunge wameichangamkia kweli kweli hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza niwataje wale waliochangia kwa kuzungumza. Mheshimiwa Dokta Abdallah O. Kigoda, Mbunge wa Handeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi; Mheshimiwa Christina L. Mughwai kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Fedha na Uchumi; Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Dokta Charles J. Tizeba, Mheshimiwa Riziki S. Lulida, Mheshimiwa Henry D. Shekifu, Mheshimiwa Selemani S. Jaffo na Mheshimiwa dada yangu Zarina S. Madabida. Kama kuna mtu nimemsahau, mtaniambia, tutamtaja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao:- Mheshimiwa John J. Mnyika, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Dkt. Getrude P. Rwakatare, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Zarina S. Madabida, alichangia pia kwa maandishi, Mheshimiwa Selemani S. Jaffo, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Mariam N. Kisangi, Mheshimiwa David Z. Kafulila na Mheshimiwa Felix F. Mkosamali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kwa maoni na ushauri wao na pia kwa kuunga mkono Azimio. Aidha, napenda pia kutoa shukrani zangu kwa Kambi ya Upinzani kwa maoni na ushauri wao na pia baada ya ushauri wao, kuunga mkono hoja. Naahidi kwamba Serikali itayafanyia kazi maelekezo na mawazo yote mazuri yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi na Kambi ya Upinzani na pia mawazo yote yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa kuzungumza na kuleta maoni yao kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajibu kwa ufupi sana kwa sababu hoja nyingi zilikuwa zinajirudia. Ni kwamba hoja zilikuwa ni zile zile, lakini kila Mheshimiwa Mbunge alizungumza kwa *style* yake. Napenda kwanza niseme kwamba hoja nyingi za kiuchumi, mambo ya mfumko wa bei na mengine yote ambayo yamejitokeza hapa ya kibajeti, tunao waraka maalum ambao nitawasilisha Bungeni hapa na Mheshimiwa Gavana wa Benki Kuu. Kwa hiyo, nisingependa kuondoa utamu kwa sababu katika waraka ule Serikali imejieleza kwa kirefu sana kwamba hali tuliyo nayo kibajeti na vile vile haya masuala yote ya mfumko wa bei, kushuka kwa thamani ya shilingi na masuala mengine yanayohusiana na uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nijielekeze zaidi kwenye yale yanayohusiana moja kwa moja na hoja iliyopo. La kwanza, hili lilizungumzwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, lakini pia lilizungumzwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Wabunge wengine wawili. "Kwa nini Azimio hili halikuletwa Bungeni mwezi Novemba". Nataka kusema kwamba kama mtakavyoona katika ile amri ambayo nillitoa, ni kweli baada tu ya Kikao cha Bunge kukamilika ile amri iliandaliwa na ilitolewa katika gazeti. Nadhani mwenzangu Mwanasheria Mkuu ataelezea zaidi, kwa bahati mbaya vitu vilikuwa vingi mno ambavyo vilikuwa vije hapa Bungeni mwezi Novemba, lakini, kikubwa ambacho nadhani *concentration* ilikuwa kubwa ni Sheria ya Katiba. Kwa hiyo, umuhimu nadhani ukapewa zaidi kwenye Sheria ya Katiba na hivyo sheria nyingine ambazo ilikuwa tuzilete hapa Bungeni, si kwa kudharau amri, ni kwa sababu ya muda wenyewe ulivyokuwa, zile nadhani zikasogezwa mbele kwa bahati mbaya ikiwa ni pamoja na hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kusema si kwamba Serikali ilidharau, lakini, nadhani hali halisi ilivyokuwa, ilifanya yatokee hayo. Sasa kwa niaba ya Serikali, naomba radhi kwa kuchelewa huko, lakini si kwamba tulifanya uzembe, ila hali halisi ndivyo ilivyokuwa kwamba *order* ilitayarishwa, lakini haikupata muda wa kuletwa hapa Bungeni kuzungumzwa. Lakini ni heri uchelewe kuliko kutofanya kabisa kile unachotakiwa ukifanye. Kwa hiyo, maadam Serikali imeamua kuleta Azimio hili, naomba sana sana Waheshimiwa Wabunge, ni vyema kwa kweli mkaliridhia ili... maana tumezungumza wengi, kuna wengine ambao wanawaonea huruma wananchi kwamba ni vizuri punguzo hili likatolewa ili wananchi wafaidike, lakini wako pia ambao wanaona kwamba inawezekana wananchi wasifaidike sana. Lakini wako ambao wangetaka tuelezwe hapa hapa kwamba ni nini kitafanyika, ndiyo Azimio hili liweze kupita.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengi ya Kiserikali huwa haiwezekani kwamba ukisema sasa hivi, kweli vitabu vyote vya bajeti na kila kitu viwe kichwani kwangu, niweze kusema kwamba hiki kitatoka hapa, hiki kitatoka hapa, hapana. Lakini, nataka kuahidi kwamba yale ambayo tumesema kwamba tutapunguza, kwanza niseme, kimsingi katika mawasilisho ya Serikali ya Bajeti ya 2011/2012, kitu kimoja ambacho tulisema ni kwamba, ni uamuzi wa Serikali kwamba, posho zote na matumizi yote ambayo hayana tija sana kwa nchi, tutayapunguza. Haya tuliyoyataja hapa ni yale ambayo tuliyasema tangu mwezi Juni mwaka jana. Kupunguza huku kumekuwa kukiendelea. Maeneo mengine yameshapunguzwa tayari, maeneo mengine yanaendelea kupunguzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani kwamba, tukisema bilioni 7.7 *ina-sound a lot of money*. Lakini baadhi ya kasma hizo zinazozungumzwa, kuna milioni 200, kuna milioni 50, kuna milioni ngapi. Kwa hiyo, si kwamba kila kasma iliyotajwa hapa, kila moja itapunguzwa *rationally* kwa kiasi hicho hicho, hapana. Kuna mahali ambapo tutapunguza kwa kiasi fulani, kuna mahali ambapo tutaweza kupunguza kidogo. Lakini, tunaamini kwamba maeneo haya tuliyoyataja, iko room ya kuweza kupunguza na kusiwe na athari yoyote kwa uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wazo lilijitokeza na wengi wamelizungumzia kwamba tukipunguza shilingi 57 kwa viwanda vya hapa nchini, kwa nini hizo zisipelekwe kwa wale wanaoagiza maji kutoka nje?

Kamati ya Fedha ililizungumza hilo na jana tulilifanyia kazi. Kwa bahati nzuri, hata bila Serikali kusema kwamba tunataka kufuta kabisa maji kutoka nje. Tulianza na asilimia 100 maji kutoka nje, sasa hivi ni *less than 20%* ya maji kutoka nje. Kwa hiyo, ile *component* ya haya maji yanayotozwa kodi ni *less than 20%* ndiyo maji ambayo sasa hivi yanatoka nje. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba hili soko la maji kutoka nje litajua lenyewe katika muda mfupi ujao. Sasa kwa hiyo, kwa sababu ni sehemu ndogo, hata kama ukisema kwamba zile shilingi 57 uzipeleke kwa ile sekta, hutapata hiyo 7.7 *billion* tunazozitafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya kufika hapa, tukasema okay, lakini ni lazima tutafute mahali pa kuziba pengo hili, tutapata wapi, ndiyo tukafikia kwamba basi ni vyema tuangalie maeneo ambayo tunaweza tukapunguza na yasiwe na athari kwenye uchumi wa nchi hii. Ndiyo tulipofikia, haya maeneo ambayo tayari hata kwenye Bunge hili tulishaahidi kwamba Serikali itapunguza matumizi kwenye maeneo hayo. Kwa hiyo, si jambo jipya, ni jambo ambalo tayari tulilisema na sasa hivi tunachoomba ni kwamba badala ya kusema...maana tukisema kwamba twende kwenye haya maji ya nje, kwa mwaka mzima kodi ya maji ya kutoka nje ni 1.4 *billion*, mwaka mzima. Kwa hiyo, hata kama ukisema kwamba uende ukaongeze kwa miezi iliyopatikana, hutopata 7.7.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, ningependa kuwaomba mturuhusu kwa kweli tufanye kitu ambacho tunakiomba na mimi nina hakika kwamba kitasaidia na Dada yangu Madabida itawasaidia wananchi kwa namna fulani, *not necessarily* kama ulivyosema shilingi hamsini na saba kwa kila mtu, lakini kutakuwa na punguzo fulani kwenye maji kule ambako tunakusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wamesema kwamba tulete kwenye *supplementary budget*, tunafikiri kwamba hatuna haja ya kuleta hii kwenye *supplementary budget* kwa sababu *supplementary budget* ni kwamba unaleta matumizi ambayo yamezidi kiwango ambacho Bunge liliidhinisha. Hili ninalolisema halitaongeza matumizi yale yaliyoidhinishwa na Bunge tayari, kwa hiyo, ni kwamba hii yote tutaipata ndani ya bajeti yetu tuliyonayo, kama itabidi kuleta *supplementary budget* tutaleta *performance report*, nadhani wakati huo utakapofika Wabunge wanaweza wakaizungumza, tukapata mawazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo kama ruzuku alizungumza Dada yangu Mughwai, kwamba ruzuku tuliyotoa kwenye mafuta ya taa ipelekwe kwenye umeme vijijini, nataka kukumbusha tu kwamba wakati tunaongeza kodi kwenye mafuta ya taa, tulipunguza kodi kwenye *diesel* na *petrol*, kwa hiyo kilichotokea ni kwamba, tuli-*balance* ili kuondoa uchakachuaji. Kwa hiyo, hakukuwa na pesa za kutosha kwa hatua ile iliyochukuliwa za kuweza kuzipeleka kwenye umeme vijijini, ninachoweza kukuhakikishia ni kwamba tuna mipango mingine ya kutafuta pesa kutoka vyanzo vingine kwa ajili ya umeme vijijini, nadhani hilo litakapofika hatua zake mwenzangu Ngeleja ataweza kuja kuliiongezea kwa umakini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo mengine ambayo ni pamoja na ndugu yangu Tizeba amezungumzia kwamba sawa, leo tumeleta hii ya maji lakini kuna maeneo mengine pia ambayo yanakodi kubwa kwenye mvinyo unaotengenezwa hapa Dodoma, lakini kuna kodi kidogo kwenye mvinyo ambao unatoka nje. Hilo itabidi tulifanyie kazi ili kuhakikisha kwamba, hilo ni kweli, lakini kama ni la kweli kuanzia mwezi ujao tunaanza mchakato wa bajeti ya 2012/2013, nadhani ningesema kwamba kwa kitu cha kisera kama hicho, siyo vizuri tukakitumbukiza kwenye Azimio hili la Maji.

Ni vizuri kitu cha kisera kama hicho kikaingia katika utaratibu mzuri na kikazungumzwa katika mfumo mzima wa kodi tutakapokuja nao mwezi wa Tatu (Machi) au mwezi wa Nne (Aprili) na baadaye tutakapowaleteeni bajeti kwenye Bunge mwezi wa Sita (Juni).

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningependa kusema tu kwamba wenzetu ambao mawazo mengi hapa yametoka ni mazuri sana, wale ambao tuna mawazo ya maeneo ambayo tungependa tuyaboreshe, ningesema kwamba si lazima tusembiri mpaka Waziri wa Fedha alete Azimio, tuandikiwe. Kwa mfano, kama hii ya maji tumeandikiwa na baada ya kuandikiwa na kuitazama tukashawishika kwamba kwa kweli ni nzuri, kweli Kamati ilitushauri na tukashawishika kwamba ni vizuri kwa kweli tukaangalia hii kodi ifike kama mahali fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine limezungumzwa hapa kwamba tuangalie na kupanua wigo wa kodi, nataka kumhakikishia ndugu yangu Tizeba kwamba tumeshaunda Kamati ya *Multidisciplinary*

Committee ya watu ambao wanaangalia *private sector* wamo, Serikali wamo, watu wa Wizarani kwangu wamo, watu wa benki wamo, kuangalia nini tufanye ili kuhakikisha kwamba si kila mwaka tunakuja hapa kuomba kutoza bia, kutoza sigara, tupate na maeneo mengine. Hilo linafanyiwa kazi na wakati muafaka litaletwa hapa Bungeni na tutaomba wenzetu mlitazame na kwa hivyo muweze kutupa ruhusa ya kulipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mengine yaliyozungumzwa Dada yangu Lulida nasema yote haya ni ya kiuchumi, yana nafasi yake, tunayachukua, tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapa kwamba mawazo yaliyotolewa ni mengi, tumeyachukua, tutayafanyia kazi na kwa wakati muafaka tutayatolea maelezo hapa Bungeni, lakini mengi ningependa kusema kwamba msubiri kunisurubu ile siku nitakapotoa waraka wa hali ya uchumi, ule waraka ni mrefu, unaeleza mambo mengi. Nadhani hata mjadala unaweza kuwa mjadala mtamu zaidi kuliko haka kaazimio kanakohusiana na maji, mimi ningeshauri kabisa kwamba juhudi zetu zote ziende kwenye Azimio hili, tulipitishie Azimio hili jinsi tulivyoomba, haya mengine yote yaje yaingie kwenye *paper* nyingine ambazo Serikali itazileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena kushukuru na kuwashukuru Wabunge wote waliozungumza humu ndani, na wale waliochangia kwa maandishi. Naomba kabisa kwamba, Bunge lako liridhie kupitisha Azimio hili ili ushuru wa maji upungue kutoka shilingi 69 kwa lita na kufika shilingi 12 kwa lita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Waziri, tunashukuru sana kwa kutoa hoja yako. Namuona tena Mheshimiwa Dokta Tizeba.

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Kanuni hiyo ya 58, naomba Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono hoja hii ya Serikali iondolewe kwa sababu haina manufaa kwa mwananchi, mlaji wa mwisho wa maji. Shilingi 27 itakayopunguzwa kwenye lita moja haitekelezeki katika *retail business*, shilingi 57 inayoondolewa kwa lita moja haitamfikia punguzo hilo mlaji wa maji wa kawaida, kwa hiyo, hili ni punguzo ambalo linalenga kuwanufaisha wenye viwanda na kama Waziri mwenyewe alivyokiri kwamba ameshawishiwa na wenye viwanda kwamba wafanye punguzo hilo. Kwa hivyo, nawaomba Wabunge mniunge mkono hoja hii ya Serikali iondolewe na kama mabadiliko haya wanafikiria kuyafanya basi wayalete katika Bunge la bajeti la mwezi Julai.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MHE. HERBERT J. MTANGI: Mheshimiwa Naibu Spika naafiki.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nakushukuru sana Dokta Tizeba, hoja yako imetolewa na imeungwa mkono, lakini tunarudi kwenye Kanuni uliyoitumia ambayo ni Kanuni ya 58 nitaisoma tena ili tuweze kwenda pamoja.

"Endapo Mbunge anapenda kupendekeza mabadiliko yafanywe katika hoja kwa kufuata masharti ya Kanuni hizi, anaweza kutoa hoja yake kwa kufanya mabadiliko wakati wowote, baada ya hoja anayotaka kubadilisha kutolewa lakini kabla ya Bunge halijahojiwa ili lifanye uamuzi"

Alichofanya Dokta Tizeba siyo kuleta hoja ya mabadiliko kwa sababu hapa sina hoja ya mabadiliko ya kwake inayosema mabadiliko yaweje. Nadhani Dokta Tizeba alitaka kutumia Kanuni ya 69 ambayo inasema: "Mbunge anayependa mjadala unaoendelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye, anaweza kutoa hoja kwamba mjadala huo sasa uahirishwe na atataja mjadala huo uahirishwe hadi wakati gani na pia atalazimika kutoa sababu za kwa nini anataka mjadala huo uahirishwe." Dokta Tizeba ametoa sababu kwa nini anataka mjadala huo uahirishwe.

Sasa ametumia Kanuni isiyokuwa sahihi sana, kwa hiyo, bahati mbaya hoja yake inakuwa imekaa tenge. Sasa Kanuni ya 69(2) inasema; Kama Spika atakuwa na maoni kwamba kuwasilishwa kwa hoja

hiyo ni kinyume cha uendeshaji bora wa shughuli za Bunge, atakataa kuitoa ili iamuliwe; vinginevyo, papo hapo atawahoji Wabunge juu ya hoja hiyo kadri atakavyoona inafaa.

Kwa jinsi hiyo basi na kwa uendeshaji bora wa Bunge mimi naomba niwahoji.

*(Hoja iliitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

(Bunge liliafiki kuondolewa kwa Azimio la Waziri wa Fedha)

NAIBU SPIKA: Eeh! Wasioafiki wameshinda. Kwa hiyo itabidi tujipange upya wakati mwingine kadri hali itakavyoruhusu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo uendeshaji wa shughuli za Bunge pamoja na mambo mengine tunakwenda kwa kujifunza na kwa wenzetu wanafanya nini. Katika nchi ya Misri juzi au jana kulikuwa na mechi ya mpira pakatokea washabiki wa timu mbili wakapambana, watu sabini na nne (74) wamepoteza maisha na Bunge la nchi ile lilikuwa lipo likizo, kutokana na vifo vile, Bunge la nchi ile limeitwa mara moja na hivi sasa tunavyoongea lipo kazini ili kupata kauli ya Serikali kuhusiana na kilichotokea. Sisi kwa hili jambo linaloendelea la matatizo katika sekta ya afya, Wabunge wameongea juzi, wameongea jana, wameongea leo, kwa kweli itakuwa ni jambo lisiloleweka kama kesho haitatoka kauli ya Serikali. *(Makofi)*

Kwa sababu kauli ya Serikali isipotoka kesho wakisimama Wabunge hapa ina maana ratiba yetu inaweza ikatibuka sana. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba kesho tutapata maelekezo ya Serikali kuhusiana na nini kinachoendelea ili kupitia kwetu wananchi wa Tanzania nao waweze kuisikia Serikali yao kwa sasa inasema nini.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo haya, naomba sasa nitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja leo jioni.

(Saa 7.00 Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2011 (The Written Laws [Miscellaneous Amendments] No. 2 Act, 2011)

(Kusomwa Mara ya Pili)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2007, kwa heshima na taadhima, naomba sasa kutoa hoja kwamba Muswada uitwao Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa mwaka 2011 yaani "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, (No.2), 2011", sasa usomwe Mara ya Pili; na kwamba Bunge lako Tukufu liujadili na hatimaye liupitishie kuwa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza hapa, kwa kupitia kwako, napenda kuchukua nafasi hii kukutakia wewe na Waheshimiwa Wabunge wote heri ya mwaka mpya na kuwatakiwa uwakilishi wenye manufaa kwa umma wa Watanzania kwa mwaka huu. Aidha, bila kuathiri Kanuni ya 151, ninapenda kutoa rambirambi kwa familia ya Mheshimiwa Regia Mtema, Mbunge wa Viti Maalum kupitia CHADEMA na familia ya Mheshimiwa Jeremiah Sumari - Mbunge wa Arumeru Mashariki kupitia CCM kwa kuwapoteza wanafamilia wao. Ninajumuika na Wabunge, wananchi wote na familia zao kuwaombea Marehemu hao ili wapate pumziko la milele na amani Peponi. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninamshukuru sana Mheshimiwa Pindi Hazara Chana - Mbunge Viti Maalum, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na kupitia kwake Wajumbe wote wa Kamati kwa mchango na kazi kubwa waliyoifanya kuuboresha Muswada ulio mbele ya Bunge lako Tukufu. Maoni na ushauri wao kwa kiasi kikubwa vimesaidia kuboresha sana Muswada huu. Hii inathibitishwa na marekebisho katika Muswada kama yanavyoonekana katika Majedwali mawili ya Marekebisho ambayo yatawasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa mwaka 2011 unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria 17 kwa lengo la kuondoa hitilafu na upungufu uliojitokeza wakati wa matumizi ya Sheria hizo, pia kuongeza masharti mbalimbali katika sheria hizo ili kuleta uwiano katika Sheria zinazorekebishwa pamoja na kusaidia utekelezaji madhubuti wa Sheria hizo, moja moja au kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa ni Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178; Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma, Sura ya 371; Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Mashirika ya Umma, Sura ya 372; Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 407; Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 50; Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399; Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara, Sura ya 208, Sheria ya Uendeshaji wa Mashtaka, Sura ya 430; Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma za Kipolisi, Sura ya 322; Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168; Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, Sura ya 96; Sheria ya Mapato kwa njia ya Uhalifu, Sura ya 256; Sheria ya kuzuia Ugaidi, Sura ya 19; Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200; Sheria ya Kuzuia Biashara ya Madawa ya Kulevya, Sura ya 95; Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6 na Sheria ya Korosho, Sura ya 203.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada unaopendekezwa umegawanywa katika Sehemu 18.

Sehemu ya Kwanza inaweka masharti ya Utangulizi, jina na kusudio la Muswada. Jina la Muswada ni kama ilivyo Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 2), 2011, yaani (*Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Act, 2011*).

Katika Muswada huu Ibara ya (4) ya sehemu ya pili, hususan Ibara ya (4) ya Muswada, inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha (5) cha Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (Sura ya 178) ili kuruhusu mwakilishi mmoja kutoka Tume ya Vyuho Vikuu (TCU) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) kuwa miongoni mwa Wajumbe wa Bodi waliotajwa kwenye kifungu cha 5(1) cha Sheria.

Ibara ya (5) ya Muswada: Marekebisho yanapendekezwa kufanyika katika kifungu cha (7) kuhusiana na mamlaka ya Bodi. Mamlaka ya Bodi yanaongezwa ni pamoja na haya matatu:-

(a) Kuamua idadi ya wadhiliwa watakaopewa mikopo kwa mwaka kutegemea bajeti.

(b) Kutoa masharti ya msaada (*grants*), usarifu (*bursaries*) na udhamini wa masomo (*scholarships*).

(c) Kuwasiliana na kuomba kupewa taarifa za wadaiwa wa mikopo kutoka kwenye Ofisi na Idara mbalimbali ambazo kwa njia moja au nyingine zitapata taarifa hizo za wadaiwa ili kurahisisha urejeshaji wa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki ya kifungu cha (7) kinachofanyiwa marekebisho kwa kufuta kipengele (i) na kukiandika upya ili kuipa Bodi mamlaka ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaostahili kulingana na ukomo wa bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha husika na kwa kuzingatia uwezo wa kiuchumi wa wazazi au walezi wa mwanafunzi husika. Pia marekebisho ambayo yamefanyika yanakusudia kuipatia Bodi uwezo wa kuomba na kupata taarifa mbalimbali za wadaiwa wa mikopo hiyo, kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Wakala wa Usajili wa Shughuli za biashara na leseni kwa lengo la kurahisisha urejeshaji wa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho mengine yanapendekezwa kufanywa katika kifungu cha 16 kama inavyoonekana kwenye ibara ya (6) ya Muswada, kifungu kinachohusiana na utoaji wa mikopo

kwa wanafunzi. Sheria ilivyo kwa sasa inaonyesha kuwa mikopo hutolewa kwa wanafunzi wote bila kujali kama amejunga kwa sifa linganishi, ametoka kazini au shuleni moja kwa moja. Kwa sasa inapendekezwa kwamba:-

- (i) Mikopo itatolewa tu kwa waombaji waliodahiliwa na Vyuo vya Elimu ya Juu na ambao wanatoka shuleni moja kwa moja (*Direct entrants*);
- (ii) Utoaji wa mikopo utazingatia pia uhitaji wa mwombaji na fani za kipaumbele za Taifa;
- (iii) Utaratibu wa kubaini wahitaji wa mikopo utazingatia vigezo vinavyopimika kwa urahisi kama vile shule aliyosoma, uyatima, ulemavu na uwezo wa kiuchumi wa mzazi/mlezi;
- (iv) Kiwango cha mikopo kwa wale wanaostahili kukopeshwa kitategemea matokeo ya tathmini ya uwezo wa kiuchumi wa mwombaji na mzazi/mlezi (*Means Testing*); na
- (v) Kwa kuzingatia kuwa wahitaji ni wengi, umuhimu utapewa kwa wahitaji wanaochukua fani za kipaumbele za Kitaifa ambao kwa sasa kama inavyoonekana kwenye jedwali la mabadiliko ni:-
 - (a) Ualimu;
 - (b) Sayansi za tiba (Udaktari wa Binadamu, Udaktari wa Mifugo, Udaktari wa Meno, Ufamasia na Uguzi);
 - (c) Uhandisi;
 - (d) Sayansi za Kilimo; na
 - (e) Sayansi za Mifugo.

Marekebisho yanayopendekezwa kufanywa kwenye kifungu cha 17 pia yanalenga kupanua wigo wa wanafunzi watakaopata mikopo kwa kuruhusu wanafunzi wanaosoma kwenye vyuo vilivyo na usajili wa muda nao kupewa mikopo tofauti na ilivyo sasa ambapo ni wanafunzi wale tu wanaosoma kwenye vyuo vyenye usajili wa kudumu tu ndio wanapewa mikopo. Marekebisho hayo pia yanampa mamlaka Waziri kuongeza masomo ambayo ni ya kipaumbele kwa Taifa kwenye Jedwali la Pili na kwamba wanafunzi wanaosoma masomo hayo watapelewa nafasi ya upendeleo katika kupewa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma, (Sura ya 371). Katika Sheria hii, hakuna kifungu kinachoruhusu Bodi kutoa taarifa maalum za wachangiaji wa Mfuko. Lengo la marekebisho haya ni kuweka kifungu kipya cha Sheria kinachoitaka Bodi kutoa taarifa maalum za wachangiaji wa mfuko ambao walikuwa wanadaiwa na Bodi ya Mikopo wa Elimu ya Juu, hii itarahisisha urejeshwaji wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Mashirika ya Umma, (Sura ya 372). Katika Sheria hii, hakuna kifungu kinachoruhusu Bodi kutoa taarifa maalum za wachangiaji wa Mfuko. Lengo la Marekebisho haya ni kuingiza kifungu kipya cha Sheria kinachoiruhusu Bodi kutoa taarifa maalum za wachangiaji wa mfuko ambao walikuwa wanadaiwa na Bodi ya Mikopo wa Elimu ya juu, ili kurahisisha urejeshwaji wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ibara ya 14, 15, 16: Kwanza futa "*Provident*" na weka "*Pensions*". Mantiki hiyo inatumika pia katika Sehemu ya Tano, inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mafao kwa Watumishi wa Serikali za Mitaa, (Sura ya 407). Katika Sheria hii, hakuna kifungu kinachoruhusu Bodi kutoa taarifa maalum za wachangiaji wa Mfuko. Lengo la Marekebisho haya ni kuingiza kifungu kipya kinachoruhusu Bodi kutoa taarifa maalum za wanachama wa mfuko ambao wanadaiwa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu, ili kurahisisha urejeshwaji wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ibara ya 17, 18, Sehemu ya Sita inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, (Sura ya 50) ili kuweka masharti yatakayoweza Mfuko

kutoa taarifa za wanachama kama taarifa za wanachama kama sheria zilizotangulia zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Saba, ambayo iko kwenye Ibara ya 19, 20 ya Muswada, inapendekeza kufanya marekebisha katika Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, (Sura ya 399). Katika Sheria hii, kifungu cha (8) kina masharti kuhusu usiri wa nyaraka au taarifa zinazohusiana na mapato, matumizi au shughuli nyingine za kifedha au hadhi ya mlipa kodi. Kwa kuwa kifungu hiki kinakataza utoaji wa taarifa kwa mtu mwingine, kifungu hiki kitarekebisha ili kuruhusu utoaji wa taarifa zitakazoombwa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa lengo la kurahisisha urejeshwaji wa mikopo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nane ambayo inaonekana kwenye Ibara ya 21 na 22 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisha katika Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara, (Sura ya 208) kwa ajili ya kuingiza kifungu kipya kitakachomruhusu Msajili Mkuu kutoa taarifa za waombaji wa usajili kwa Bodi ya Mikopo wa Elimu ya Juu kwa ajili ya kurahisisha urejeshwaji wa mikopo. Hatua hizi zitakuja baadaye kurahisishwa na ukamilishwaji wa vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tisa inapendekeza kufanya marekebisha katika kifungu cha 18 cha Sheria ya Huduma za Uendeshaji wa Mashitaka, (Sura ya 430). Kwa sasa kifungu hicho cha 18 kimempa Mkurugenzi wa Mashitaka mamlaka ya kutoa amri, miongozo na maelekezo ambayo maafisa waendesha mashitaka wanapaswa kuyafuata. Hata hivyo, kifungu hicho hakielezi iwapo amri, miongozo na maelekezo hayo ni lazima yachapishwe katika Gazeti la Serikali. Lengo la marekebisha haya sasa ni kuweka masharti katika Sheria ili amri, miongozo ya maelekezo yanayotolewa na Mkurugenzi wa Mashitaka yawe yanachapishwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi inapendekeza kufanya marekebisha kwenye Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma za Polisi, (Sura ya 322). Kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 26 na 27 za Muswada, kifungu cha (7) cha Sheria hii kinampa mamlaka Inspekta Jenerali wa Polisi kutoa amri mbalimbali za jumla kwa lengo la kulisimamia Jeshi la Polisi katika kutekeleza majukumu yake. Hata hivyo, katika Sheria hii hakuna masharti yanayoelekeza kuwa amri hizo ni lazima zichapishwe kwenye Gazeti la Serikali. Lengo la marekebisha haya ni kuweka masharti yanayoelekeza kuwa amri zinazotolewa na Inspekta Jenerali wa Polisi chini ya kifungu cha (7) zinaweza kuchapishwa katika Gazeti la Serikali hasa kwa kuzingatia Ulinzi Shirikishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Moja kama inavyoonekana kwenye Ibara ya 28 na 29 ya Muswada ina lengo la kufanya marekebisha katika kifungu cha 25 cha Sheria ya Usalama Barabarani, (Sura ya 168). Madhumuni ya marekebisha haya yanalenga kuingiza kifungu kipya ndani ya Sheria hii cha kushughulikia na kusimamia leseni za udereva. Kifungu kinapendekeza kuweka utaratibu wa leseni za udereva kupewa alama maalum kwa namba na pale mwenye leseni anapotenda kosa au anapohukumiwa kwa kosa lolote linalohusiana na uvunjifu wa Sheria ya Usalama Barabarani, basi namba hizo zitakuwa zikipunguzwa. Kuingizwa kwa kifungu hiki kipya kunalenga kuwawajibisha wenye leseni za udereva kuwa makini na kufuata masharti yaliyopo katika leseni za udereva kwa lengo la kupunguza ajali za barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya 12 kama inavyoonekana katika Ibara ya 30, 31, 32, 33, na 34 za Muswada, inapendekeza marekebisha ya vifungu mbalimbali vya Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (Sura ya 96). Mapendekezo ya marekebisha yanatarajiwa kufanywa katika vifungu vya 3, 4, 21 na kifungu cha mwisho cha 22. Marekebisha kwenye kifungu cha (3) yanalenga kupanua tafsiri ya neno "Waziri" ili kumhusisha pia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Masuala ya Muungano. Marekebisha haya pia yanafanywa katika kifungu cha (4) ili kumtambua Afisa Kiongozi au Afisa aliyeteuliwa na Katibu wa Bunge kuwa Msimamizi wa Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Sehemu hii inapendekeza pia marekebisha katika kifungu cha 21 ili Ofisa Mfawidhi kuwa Msimamizi Mkuu wa Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo. Mwisho, marekebisha yanapendekezwa katika kifungu cha 22 ili Afisa Mipango wa Wilaya na mmoja kati ya Madiwani waliotajwa katika kifungu cha 10(c) kuwa ndio watia saina wateule wa Kundi 'A' na 'B' kwa pamoja kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ibara ya 35, 36, 37, 38, 39, 40, 41 na 42, Sehemu ya 13 inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Mapato kwa Njia ya Uhalifu, (Sura ya 256). Marekebisho yanayokusudiwa yanalenga vifungu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kifungu cha (3). Kifungu cha tatu (3) kinahusiana na tafsiri ya baadhi ya maneno. Mapendekezo yanatarajia kurekebisha tafsiri ya neno "*tainted properties*" "*property*" na "*trustee*". Lengo la marekebisho haya ni kutoa tafsiri pana zaidi ili iweze kukidhi matakwa yaliyokusudiwa katika Sheria. Kifungu cha (5) cha Sheria kinapendekezwa kifanyiwe marekebisho ili maneno "*except section 4*" yaondolewe kwa kuwa kuwepo kwa maneno hayo kunaondoa maana ya kifungu cha 4(1) (c). Marekebisho pia yanapendekezwa katika kifungu cha 12 ili kuondoa utata uliopo. Kwa sasa endapo mtuhumiwa anayechunguzwa akitoroka, Mahakama haina uwezo wa kutoa amri ya kufilisi mali ya mtuhumiwa huyo kutaka kuzipa pengo hilo.

Sehemu hii inapendekeza marekebisho kwa kuongeza kifungu kipya cha 13(a) ili kuondoa utata uliopo wa kutaifisha mali ya mtuhumiwa ambaye yupo chini ya uchunguzi au ameshitakiwa au kabla ya kutiwa hatiani, anafariki. Kwa sasa kama nilivyosema, Mahakama haina mamlaka ya kutoa amri ya kufilisi mali ya mtuhumiwa huyo. Marekebisho ambayo yamefanywa yanakusudia kuipa Mahakama mamlaka ya kutoa amri ya kufilisi mali ya mtuhumiwa aliyefariki au anatoroka wakati akiwa anafanyiwa uchunguzi au baada ya kushtakiwa Mahakamani. Aidha, inapendekezwa pia kufanya marekebisho katika kifungu cha 38. Marekebisho haya yanakusudia kumpa mamlaka Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuiomba Mahakama kutoa amri ya kuzuia mali ya mtuhumiwa wakati uchunguzi unafanyika dhidi yake ili kumzuia kuhamisha au kugawa mali aliyoiipata kwa njia isiyo halali. Kifungu cha 39 kinafanyiwa marekebisho ili kiweze kutoa mwongozo ambao Mahakama itatumia katika kumteua msimamizi wa mali iliyozuliwa wakati tuhuma zikipelelezw.

Chimbuko la mapendekezo haya ni mahitaji ya Mikataba ya Kimataifa inayohusiana na Madawa ya Kulevya (*The United Nations Convention Against Illicit Traffic in Narcotic Drugs and Psychotropic Substances*) 1998, Mkataba wa Umoja wa Mataifa unaoitwa (*United Nations Convention Against Transnational Organized Crime, 2000*) au Mkataba wa Paremo, Mkataba dhidi ya Makosa ya Rushwa (*United Nations Convention Against Corruption 2003*). Mikataba yote hii inataka nchi wanachama kuchukua hatua kuhakikisha kwamba hakuna mtu yeyote atakayenufaika na vitendo vya ufisadi na kutunga sheria za kuchukua mali zinazotokana na vitendo hivyo vya ufisadi. Nchi nyingine kama Zambia, Kenya, Afrika ya Kusini zimekwishatunga sheria za aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya 14 inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Kuzuia Ugaidi, (Sura ya 19 - Ibara ya 43-45). Mapendekezo hayo yanalenga kurekebisha tafsiri ya maneno "*property*" yaani mali na "*fund*" ili kutoa tafsiri inayolandana na Sheria ya Mapato kwa Njia ya Uhalifu, Sura ya 256.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya 15 kama inavyoonekana inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Uhujumu Uchumi, (Sura ya 200 - Ibara ya 46-47). Mapendekezo yanalenga kurekebisha kifungu cha 23 kinachohusu kutaifisha mali au kifaa kilichohusika au kusaidia kutendeka kwa kosa la jinai kwa mujibu wa Sheria hii. Kifungu hiki kinamtambua mwenye mali aliyekutwa nayo, bila kujali kuwa mali hiyo inaweza kuwa ya mtu mwingine. Marekebisho haya yanalenga kutoa tafsiri ya neno "*owner*" ili lihusishe hata yule mtu mwingine au mmiliki lakini asiyehusika na utendaji wa kosa la jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya 16 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kuzuia na Kusafirisha Madawa ya Kulevya, (Sura ya 95). Marekebisho yanapendekezwa kufanyika katika kifungu cha (2) ili kutoa tafsiri sahihi ya neno "*Court*" na kuonyesha aina gani ya makosa yatafunguliwa Mahakama za Mahakimu wakazi na ni makosa gani yatafunguliwa Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 12 kinahusu makosa ya kulima mmea wowote wa madawa ya kulevya, ambapo maneno "*manufactured drugs*" na kifungu cha maneno "*or any preparation containing any manufactured drugs*", yanavyoonekana kwenye kipengele cha (d) yapo kimakosa. Hivyo, tunapendekeza yafutwe ili kuondoa utata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 16 kinahusu makosa ya usafirishaji wa madawa ya kulevya. Kifungu hiki kinarekebisha ili kuondoa utata wa kiasi cha madawa mtu atakachopatikana nacho bila kujali wingi. Mapendekezo pia yanapendekezwa ili kuongeza kifungu kipya cha 17 (a) kinachotoa adhabu

kwa mtu atakayepatikana akitumia madawa ya kulevya au mmiliki wa eneo na kuruhusu eneo lake litumike kutayarishia au kuzalishia madawa ya kulevya, na hii hasa ni kwa wale ambao wanakodisha mashamba kwa watu wenye tabia hizo. Vile vile kuainisha kosa la kupatikana na vifaa au zana za kuzalishia madawa ya kulevya au kushawishi mtu kutumia madawa ya kulevya au kushawishi mtu mwingine kujingiza katika kundi na kuvuta au kutumia madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya 17 inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ushahidi, (Sura ya 16). Kifungu cha 34 (b) kinaelekeza utaratibu wa kutoa ushahidi Mahakamani kwa mtu ambaye hakuweza kupatikana na kutoa ushahidi wake ili maelezo yake yatumike kama ushahidi Mahakamani. Katika kutoa maelezo hayo, yapo masharti ambayo endapo yatatekelezwa, basi maelezo hayo yanaweza kupokelewa Mahakamani. Miongoni mwa masharti hayo, ni kwamba kusiwepo pingamizi la kupokea maelezo hayo ndani ya muda wa siku kumi kutoka upande mwingine kuanzia tarehe ya kusudio la kutoa maelezo hayo. Sheria kama ilivyo hivi sasa haitoi fursa kwa Mahakama kupima uzito wa pingamizi hilo endapo litatolewa. Lengo la marekebisho haya ni kuipa Mahakama mamlaka na fursa ya kupima uzito wa pingamizi linaloweza kutolewa kabla ya kukubali au kukataa pingamizi lililotolewa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya 14 inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 17 (a) cha Sheria ya Korosho, (Sura ya 203). Marekebisho haya kwa sasa yameondolewa kutokana na sababu kuwa mjadala unaohusiana na mapendekezo haya bado unaendelea kujadiliwa na wadau na hawajafikia muafaka. Hivyo sehemu hii kwa sasa inafutwa kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, napenda kupitia kwako kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kujadili Muswada huu na kuipitisha katika hatua mbili, yaani Kusomwa kwa Mara ya Pili na Kusoma kwa Mara ya Tatu. Nina imani kwamba Bunge lako litaridhia marekebisho yote yaliyopendekezwa na litakubali marekebisho haya yawe sehemu ya Sheria za Nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja iliitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hoja yako ambayo imeungwa mkono. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia jambo hili kutoka Kamati ya Katiba na Sheria. Mheshimiwa Karibu.

MHE. JADDY S. JADDY (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2011, *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No.2) Act, 2011)*. Lakini kabla sijafanya hivyo, kwa niaba ya Kamati, napenda kutoa pole kwako na kwa familia za Wabunge wenzetu ambao leo hii hatuko nao hapa baada ya kutangulia mbele za haki.

Kamati inaungana na familia za Marehemu Mheshimiwa Regia Mtema na Mheshimiwa Jeremiah Sumari katika kipindi hiki kigumu kwao. Aidha, Kamati inapenda kutoa pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Steven Galinoma ambaye katika Bunge la Tisa alikuwa ni Mbunge mwenzetu na Mjumbe wa Kamati hii. Pamoja na Marehemu Ndugu Nicodemus Luther Senge ambaye alikuwa Mfanyakazi wa Ofisi ya Bunge.

Kamati inawafariji wafiwa wote na kuwaombea Marehemu wote kwa Mwenyezi Mungu azipumzishie Roho zao mahali pema Peponi. Amen. Bwana alitoa na Bwana ametwaa, jina lake na lihimiwiwe. *Innalillah wa Inna Illaih Rajiun.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kamati yangu ndiyo iliyoshughulikia Muswada wa Mabadiliko ya Katiba, 2011 katika Mkutano wa Bunge uliopita, napenda kwa niaba ya Kamati kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kusaini Muswada huo tarehe 29 Novemba, 2011 na kuwa ni Sheria. Kamati inawaomba Watanzania popote pale walipo bila kujali itikadi zao, kutoa ushirikiano kwa Tume

inayotarajiwa kuundwa na Mheshimiwa Rais, pindi Tume hiyo itakapoanza kazi ya kuratibu na kukusanya maoni kwa ajili ya Katiba Mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuuleta kwenye Kamati yetu Muswada huu muhimu utakaosaidia kuboresha sheria mbalimbali zinazopendekezwa ili ziweze kufanya kazi vizuri kulingana na wakati tulionao sasa na nyakati zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuipangia Kamati yangu kazi ya kushughulikia Muswada huu kwa Mujibu wa Kanuni ya 84(1), tarehe 24/01/2012, Kamati ilikutana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Frederick Werema, pamoja na wataalamu wake kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kupata maelezo ya Serikali kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Kamati ilialika Wadau mbalimbali ili waweze kufika mbele ya Kamati na kutoa Maoni yao juu ya Muswada huu kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi wake. Wadau walipata fursa ya kutoa maoni yao mbele ya Kamati siku ya Jumanne tarehe 24/01/2012 katika Ukumbi wa *Dar es Salaam International Conference Centre*.

Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Wadau waliofika mbele ya Kamati ili kutoa maoni yao na wale waliotoa maoni kwa maandishi. Kamati inapenda kutambua mchango mzuri wa Wadau hao ambao ni pamoja na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Kituo cha Msaada wa Sheria kwa Wanawake (WLAC), Chama cha Wanasheria Wanawake wa Tanzania (TAWLA), Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TSL), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tume ya Kuzuia Madawa ya Kulevya (LPF), Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Bodi ya Korosho, Polisi, Uhamiaji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao hicho, Mtoa Hoja alieleza Kamati kuwa, Muswada wa Sheria ya Marekebisha ya Sheria Na. 2 wa Mwaka 2011, unapendekeza kufanya marekebisha katika Sheria 16 kwa lengo la kuondoa upungufu uliobainika wakati wa matumizi ya Sheria hizo, na kuongeza masharti mbalimbali ili kuleta uwiano katika sheria zinazorekebishwa pamoja na kusaidia kuwepo kwa utekelezaji mzuri wa Sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa ni Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178, Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Mashirika ya Umma, Sura ya 372; Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 407; Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 50; Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399; Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara, Sura ya 208; Sheria ya Uendeshaji wa Mashitaka, Sura ya 430; Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma za Kipolisi, Sura ya 322; Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168; Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, Sura ya 96; Sheria ya Mapato kwa Njia ya Uhalifu, Sura ya 256; Sheria ya Kuzuia Ugaidi, Sura ya 19; Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200; Sheria ya Kuzuia Biashara ya Madawa ya Kulevya, Sura ya 95; Sheria ya Ushahidi, Sura ya 16, na Sheria ya Korosho, Sura ya 203.

Aidha, Sheria ya Korosho, Sura ya 203, Serikali ilitoa taarifa kuwa imeonekana upo umuhimu wa kuifanyia marekebisha zaidi kwa lengo la kuiboresha na hivyo kuiondoa kwenye Orodha ya Sheria zinazofanyiwa marekebisha kwa sasa hadi hapo maboresho zaidi yatakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Marekebisha ya Sheria mbalimbali Na. 2 wa Mwaka 2011 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments (No.2) Act, 2011*).

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa kamati ni kama ifuatavyo: Katika suala la Utungaji Sheria, lazima uzingatie masharti ya Katiba na Mahitaji ya Kisheria kwa wakati unaokusudiwa. Kamati yangu ilipokuwa inajadili Muswada huu, ilipenda kujiridhisha kuhusu masuala ya Msingi ikiwemo kasoro za Kisheria zinazokusudiwa kurekebishwa na kuboreshwa kwa kuzingatia masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Kamati ilihoji masuala mbalimbali ya msingi pamoja na kutafakari kwa kina mapendekezo ya Serikali pamoja na maoni ya wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitumia mamlaka yake kwa kumshauri Mtoa Hoja kuufanyia Muswada mabadiliko kama inavyoainishwa katika Kanuni ya 84(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007. Ni kutokana na ushauri huo wa Kamati, ndio maana mtoa hoja amewasilisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho ambalo limezingatia maoni mbalimbali na ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imeridhika kwamba endapo Bunge lako Tukufu litapitisha Muswada huu pamoja na kuzingatia ushauri wa Kamati, litakuwa limeondoa upungufu uliobainika wakati wa matumizi ya Sheria hizo, pia kuongeza masharti mbalimbali ili kuleta uwiano katika Sheria zinazorekebishwa pamoja na kusaidia utekelezaji madhubuti wa Sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na baadhi ya mapendekezo ya Serikali ya kurekebisha Sehemu ya Pili ya Muswada huu inayopendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (Sura ya 178). Hata hivyo, Kamati inashauri maeneo mengine yafanyiwe maboresho zaidi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178, katika Kifungu cha 4(b) na 4(d) maneno "*or his representative*" yaongezwe baada ya neno "*Director of Higher Education*". Sababu za mapendekezo hayo ni kutoa nafasi kwa mtu mwingine zaidi ya Mkurugenzi kuhudhuria Mkutano wa Bodi ya Mikopo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Elimu ya Juu pale ambapo anakuwa hayupo.

Maneno "*not less than nine*" kama yalivyoandikwa kwenye Kifungu cha 4(a) yaondolewe kwani hayaleti mantiki. Neno "*second*" kama lilivyoandikwa kwenye Kifungu cha 4(b) liondolewe na kuwekwa neno "*schedule*". Sababu za mapendekezo hayo ni kwamba neno "*second*" kama linavyopendekezwa kuongezwa halipo kwenye Sheria inayorekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri wakati wa uteuzi pande zote za Muungano zizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kamati inashauri kwamba maneno: "*The in-service students shall not be eligible for grant of loan under this Act.*" kama yalivyoandikwa katika Kifungu cha 6(6) yaondolewe. Sababu za mapendekezo haya ni kwamba Kifungu hiki kinaweka makundi na mgawanyo ambao utawanyima haki ya mkopo wanafunzi ambao wanatoka kazini, na hasa kwa kuzingatia kuwa wengi wa wafanyakazi kama vile Walimu na wengineo, wanapoomba ruhusa ya kwenda kusoma, hukatisha ajira zao, na hivyo basi kuwaondolea mkopo kutawafanya wasiweze kumudu kulipia gharama za masomo. Kamati inashauri kuwa ipo haja ya kuzingatia Wafanyakazi walioko kazini wanaotaka kujiendeleza zaidi hususan wale wanaochukua masomo ya vipaumbele vya Kitaifa (*National Priority Courses*).

Aidha, katika Kifungu cha 6(8), maneno "*subject to the provisions of this Act, the Board shall charge interest on Loans and other financial assistance granted to students at the rate and manner to be determined by the Minister*" yaondolewe ili kuepuka marudio yasiyokuwa ya lazima, kwa sababu suala la utozaji wa riba tayari limekwishainishwa kwenye Kifungu cha 7(h) cha Sehemu ya Tatu ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Sura ya 178.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu cha 7 (c) (ii) Kamati inapendekeza maneno "*past records of school fees in secondary schools*" yaondolewe kabisa kwa sababu yakiendelea kuwepo yatawanyima fursa wanafunzi wengi wasiokuwa na uwezo wa kulipia gharama za Chuo Kikuu kwa sababu tu walisoma shule za binafsi katika ngazi za Elimu ya Msingi na Sekondari.

Kamati inapendekeza dhana ya uwezo wa Mwombaji wa Mkopo "*means of testing*" izingatiwe zaidi kwani inawezekana mwanafunzi akawa amelipiwa elimu ya sekondari au msingi kwa kufadhiliwa, au wazazi wake wamefariki kwa wakati huu, au uwezo wa mzazi kiuchumi umeshuka ukilinganishwa na wakati uliopita. Hivyo, uwepo wa Kifungu kinachopendekezwa, yaani kinachoinisha historia ya miaka ya nyuma katika ulipaji wa ada wa Shule za Sekondari unaonyesha ubaguzi kwa wanafunzi ambao hawana uwezo kwa sasa kwa sababu tu walisomea Shule za kulipia katika miaka ya nyuma. Kifungu hiki kinakwenda kinyume na Ibara ya 13(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inayotamka

kwamba; "Ni marufuku kwa Sheria iliyotungwa na mamlaka yeyote katika Jamhuri ya Muungano kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taadhira yake."

Kamati inaamini kwamba, kusoma shule binafsi siyo lazima mzazi awe na uwezo wa fedha wakati huo kwani mara nyingine ni sababu ya kukosa nafasi kwenye Shule za Serikali. Kamati inashauri herufi "s" inayoonekana kwenye neno "needness" Kifungu cha 7(c)(i) iondolewe kutoka neno hilo kwani haina sababu ya kuwepo sehemu hiyo.

Katika Kifungu 7(4) Kamati inapendekeza kuongeza maneno "the provision of" katikati ya maneno "notwithstanding" na "subsection". Katika Kifungu 7(5) kuongeza maneno, "by notice, published in the gazette" katikati ya maneno "may" na "vary".

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kwamba katika Kifungu cha 7(5) ifafanuliwe zaidi ili Waziri anapofanya mabadiliko ya kozi za vipaumbele kwa Taifa alazimike kutangaza kwenye Gazeti la Serikali ili kutoa nafasi kwa Umma kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kama yalivyotolewa kwenye vifungu vya 8(b) na (9) hata hivyo, inashauri kuwa Kozi nyingine kama vile *Medical Laboratory, Clinical Medicine* na *Dentistry* ziongezwe kwenye jedwali la pili katika Kifungu cha (9). Pia maneno "as the board shall describe" kama lilivyoandikwa kwenye mstari wa mwisho wa Kifungu cha 8(b) yaondolewe na badala yake maneno "prescribed by the board" yaingizwe.

Katika Kifungu cha (9) Kamati inashauri kwenye Kifungu cha Sheria kinachotoa Mamlaka ya kutengeneza Jedwali la Sheria badala ya 17(3) Kifungu kisomeke 17(4).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiasi kikubwa Kamati inakubaliana na marekebisho yaliyofanywa na Serikali kwa madhumuni ya kuipatia Bodi uwezo wa kuomba na kupata taarifa mbalimbali za wadaiwa wa mikopo kutoka mamlaka ya mapato Tanzania, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Wakala wa Usajili wa Shughuli za Biashara na Leseni kwa lengo la kurahisisha urejeshwaji wa Mikopo, kama ilivyoelezwa katika Sehemu ya III hadi VIII ya Muswada huu. Hata hivyo, Kamati inapenda kupata maelezo ya Serikali kuhusu ni jinsi gani Serikali itaweza kurejesha Mikopo kutoka kwa watu ambao wamejiajiri binafsi na wanaofanya shughuli ndogo ndogo na shughuli nyingine za sekta isiyo rasmi.

Kamati inashauri kuwa ni vyema Serikali iongeze vifungu vya sheria vitakavyoainisha namna ya kurejesha mikopo iliyotolewa kwa Wahitimu walionufaika na mikopo hiyo, lakini hawana ajira au biashara yoyote. Ili zoezi hili la urejeshwaji wa mikopo lifanikiwe pasipokuwa na shaka, Kamati inatoa wito kwa Serikali kuharakisha mchakato wa Vitambulisho vya Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa neno "supply" kama lilivyotumika kwenye Vifungu vya 13, 15, 16, 18, 20(3), 22 libadilishwe na kuwekwa "furnish" ili kuleta maana nzuri ya kisheria. Aidha, neno "provident" kama lilivyotumika kwenye kichwa cha habari Sehemu ya V "Amendment of the Local Authorities, Provident Fund Act" libalidishwe na kuweka "pension".

Kamati inashauri katika Kifungu cha 11(c) neno "Scheme" liondolewe na kuingizwa neno "Fund" kama ilivyo katika Sheria ya Mfuko wa Mafao ya Wastaafu Watumishi wa Umma, Sura ya 371. Vile vile katika Kifungu cha 15(1) maneno "its contribution" yaondolewe na badala yake yaingizwe maneno "insured persons" na katika Kifungu cha 15(2) neno "supplied" liondolewe na kuwekwa neno "furnished". Pia katika Kifungu cha 30(3) yaongezwe neno "granted" katikati ya maneno "loan" na "under". Pia Kifungu 22(1) na 33(2) neno "the beneficiary" yaondolewe na kuweka maneno "a beneficiary".

Vile vile, Kamati inashauri, neno "may" katika vifungu vya 24(a)(1) na 27(3) libadilishwe na kuwa "shall". "The orders, guidelines and instructions issued under this section may be published in the Gazette." Vilevile pamoja na kuwekwa kwenye Gazeti la Serikali kama inavyoainishwa kwenye Kifungu cha 24(b), ni vyema taarifa hizo zikachapishwa katika vyombo vingine vya habari kama vile magazeti ya kila siku ili hata watu wanaokaa Vijijini waweze kupata taarifa hizo.

Katika Kifungu cha 25(1), Kamati inashauri maneno “any Lawyer’ yafutwe na badala yake yaingizwe maneno “any Legal Officer” ili kuleta maana ya Kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya 10, Kamati inakubaliana na Mapendekezo ya Serikali kama yalivyotolewa kwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Jeshi la Polisi na huduma za kipolisi, Sura ya 322. Kamati inaamini marekebisho yaliyofanywa ya kumpa sharti Inspekta Jenerali wa Polisi kutangaza na kuchapisha kwenye Gazeti la Serikali amri mbalimbali anazotoa katika kulisimamia Jeshi la Polisi, yataongeza ufanisi na uwajibikaji ndani ya chombo hicho muhimu cha Serikali. Hata hivyo, katika Kifungu 27(3) Kamati inashauri neno “Instructions” liondolewe na kuwekwa neno “directions”

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria nyingine ambayo imefanyiwa marekebisho ni Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168. Pamoja na Kamati kukubaliana na mapendekezo ya Serikali kama yalivyoonyeshwa kwenye Sehemu ya 11 ya Muswada huu ambapo inapendekezwa kuwekwa kwa utaratibu wa leseni za Udereva kwa kupewa alama maalum kwa namba na pale mwenye leseni anapotenda kosa, basi alama hizo zitakuwa zikipunguzwa. Ni vyema Serikali iangalie kwa makini suala hili kwani linaweza kuchochea rushwa kati ya Madereva na waliopewa dhamana ya kusimamia utekelezaji wa Sheria hii. Kamati inashauri kuwa, suala la kupunguza alama lifanyike Mahakamani na siyo kwa Watendaji moja kwa moja ambao hata hivyo hadi sasa ni eneo mojawapo linalolalamikiwa kwa vitendo vya rushwa. Kamati inatoa angalizo Kanuni zitakazowekwa na Waziri zingatia mfumo mzuri wa utoaji haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali yaliyofanywa kwenye Sehemu ya 12 ili kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, Sura ya 96. Kamati inaamini mapendekezo haya yamelenga kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria hii kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Hata hivyo, Kamati inashauri maneno “officer in charge” yaondolewe na badala yake yawekwe maneno “Clerk of National Assembly or his designated”.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imechambua kwa makini Sehemu ya 13 ya Muswada huu inayopendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Mapato yatokanayo na uhalifu, Sura ya 256. Kwa kuzingatia Ibara ya 13 (6) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inayotoa misingi ya haki na kupiga marufuku kwa mtu aliyeshitakiwa na kosa la jinai kuhesabika mkosaji kabla ya kutiwa hatiani. Kamati inashauri kuwa mapendekezo hayo yaliyoko Kifungu 39 (kutaiifisha mali ya mtu aliyekufa kabla ya kutiwa hatiani) yatizamwe upya na Sheria hii iangaliwe upya kwani mapendekezo haya yanakiuka misingi ya haki (*principles of natural justice*). Kwani kwa mujibu wa sheria, ushahidi kwenye Masuala ya Jinai ni kwa anayeshitaki kuthibitisha pasipo shaka (*he who alleges must prove beyond reasonable doubt*) na haiwezi kulegezwa kuwa “*balance of probabilities*”. Hivyo, mapendekezo ya kuipa Mahakama mamlaka ya kutoa amri ya kufilisi mali ya mtuhumiwa wa kosa la jinai aliyefariki wakati akiwa anafanyiwa uchunguzi au hata baada ya kushitakiwa Mahakamani kabla ya kutiwa hatiani yanakiuka misingi ya haki kwa sababu mtu yeyote anahesabiwa hana hatia hadi ithibitishwe ana hatia pasipo shaka yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaafiki mapendekezo ya Serikali kama yalivyotolewa kwenye Sehemu ya 14 inayohusu Marekebisho katika Sheria ya Kuzuia Ugaidi, Sura ya 19 na sehemu ya 15 inayohusu marekebisho ya Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200. Kamati inaamini marekebisho haya yataongeza ufanisi wa utekelezaji wa Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na Mapendekezo ya Serikali yaliyofanywa katika Sura ya 16 ya Muswada kuhusu Sheria ya Kuzuia na Kusafirisha Madawa ya Kulevya, Sura ya 95. Hata hivyo, Kamati baada ya kupokea maoni toka kwa Wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Tume ya Kuzuia Madawa ya Kulevya inashauri kuwa mapendekezo yaliyofanywa kwenye Kifungu cha 51 cha Muswada huu yaangaliwe upya na hasa kwenye hukumu ya Kifungu cha Maisha kwa Mtuhumiwa aliyepatikana na hatia ya kukutwa na kiasi cha madawa ya kulevya bila kujali idadi na kiasi. Kamati inashauri kwamba ili kuepuka matumizi mabaya ya Sheria hii, ni vyema kuweka adhabu ya chini (*minimum sentence*) kwa baadhi ya makosa kwenye vifungu hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Kifungu 53 kiondolewe chote kwani kinajirudia sawa na Kifungu cha 52.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sehemu ya 17, Kamati inaomba Serikali itoe ufafanuzi zaidi juu ya sababu zilizopelekea marekebicho ya Kifungu hiki kwenye Sheria ya Ushaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuhitimisha Maoni ya Kamati kuhusu Muswada huu, napenda kuchukua fursa hii kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa kutuamini na kutupa kazi ya kufanya uchambuzi wa Muswada huu. Vile vile, napenda kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali - Ndugu George Masaju, Wataalamu wote wa Serikali na Wadau wote waliotoa maoni yao ambao kwa ujumla wao wameisaidia Kamati katika kufanya Uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii ambao bila kuchoka na kwa kutumia uzoefu na utaalumu wao katika fani mbalimbali zikiwemo fani za Sheria, Utawala na kadhalika walifanya kazi hii kwa ufanisi, umakini na uvumilivu mkubwa. Naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Pindi Chana - Mwenyekiti, Mheshimiwa Angella J. Kairuki - Makamu Mwenyekiti na Wajumbe ni Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mheshimiwa Rashidi Ali Abdallah, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Azza Hillary, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Fakharia K. Shomari, Mheshimiwa Zahra Ali Hamad, Mheshimiwa Gosbert Blandes na Mheshimiwa Mustapha Akunaay.

Wengine ni Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, Mheshimiwa Abbas Mtemvu na Mheshimiwa Nimrod Mkono. Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas D. Kashilillah, Mkurugenzi wa Kamati za Bunge, Ndugu Charles J. Mloka na Katibu wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala - Ndugu Peter Magati na Msaidizi wa Kamati Ndugu Catherine Kitutu kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy. Nakushukuru sana kwa kutoa maoni haya kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Sasa kabla sijamwita Msemaji wa Upinzani, niseme tu kwamba kwa kweli wachangiaji ni wengi sana, lakini nitaje tu wachache ambao nitaanza nao. Wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Dkt. Ndugulile atafuatiwa na Mheshimiwa Angella Kairuki na Mheshimiwa Mohammed Mnyaa atakuwa anajiandaa. Naomba sasa nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

MHE. TUNDU A. M. LISSU - MSEMaji WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA SHERIA NA KATIBA: Mheshimiwa Naibu Spika, yafuatayo ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Sheria na Katiba kuhusu Muswada ya Sheria ya Marekebicho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Marekebicho ya Sheria Mbalimbali (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill (No. 2), 2011*) ulichapishwa katika *Gazeti la Serikali* la tarehe 4 Novemba, 2011. Muswada huu umesomwa kwa Mara ya Kwanza na hatua zake zote kwa mujibu wa kanuni ya 93(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2007.

Juzi tarehe 31 Januari, 2012. Aidha, kabla ya kusomwa kwa mara ya kwanza, Muswada huu ulishapelekwa kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa ajili ya kujadiliwa na Kamati hiyo. Hii ilikuwa kinyume na matakwa ya kanuni ya 83(1) ikisomwa pamoja na kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Bunge zinazoelekeza kwamba Muswada wowote wa Sheria ambao umetangazwa katika *Gazeti* kupelekwa kwenye Kamati husika baada ya Kusomwa kwa Mara ya Kwanza. Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge hili Tukufu, Muswada wa Sheria ambao umetangazwa katika *Gazeti* hauwezi kupelekwa katika Kamati husika bila kwanza Bunge Zima kupatiwa taarifa rasmi juu ya Muswada wenyewe kwa kupitia Muswada Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu uliotumika kuwasilisha Muswada huu Bungeni na kuujadili hauna tofauti yoyote ya kimsingi na utaratibu wa kuwasilisha miswada kwa Hati ya Dharura chini ya Kanuni ya 93(3) ya Kanuni za Bunge. Hii ni kwa sababu, lengo, madhumuni na athari ya matumizi ya kanuni ya 93(2) na 93(3) ni kufupisha muda unaotumika katika utungaji wa sheria kwa kudhibiti mjadala Bungeni.

Kama nilivyowahi kusema wakati wa kujadili Muswada wa Sheria ya Uendeshaji Mahakama, 2011 katika Mkutano wa Tatu wa Bunge hili Tukufu: "Muda wa kutunga sheria ukifupishwa maana yake ni kwamba Wabunge na wadau mbalimbali hawatapata muda wa kutosha wa kuusoma, kuuchambua na kuuelewa Muswada wa Sheria na kuchangia katika uboreshaji wake. Kwa sababu hizi, utaratibu huu utumika tu ili kupitisha sheria zinazohitajika wakati wa maafa, vita au dharura nyingine za aina hiyo. Kwa maana nyingine, utaratibu wa kutumia hati ya dharura katika kutunga sheria ni utaratibu usiokuwa wa kidemokrasia, lakini ambao unahalalishwa pale kunapokuwepo na dharura ya kweli inayohitaji sheria itungwe haraka ili kukabiliana nayo."

Kama nilivyoieleza wakati huo, matokeo ya kutumia kanuni ya 93(2) na 93(3) ya Kanuni za Bunge ni kuwa na sheria zinazotungwa haraka haraka na kwa hiyo zinakosa uhalali wa kisiasa kwa sababu ya kukosa ushiriki wa Wabunge na wadau wengine. Vile vile, sheria hizo zinakuwa na makosa mengi kwa sababu ya kukosekana umakini katika kuzitunga na utekelezaji wake kisiasa na kisheria unakuwa mgumu. Aidha, sheria za aina hiyo zinafisha demokrasia na uwajibikaji wa Serikali kwa Bunge na kwa wananchi kwa sababu jukumu la kikatiba la Bunge kama Baraza la Kutunga Sheria na la kusimamia Serikali linageuzwa kuwa ni la kupiga muhuri maamuzi na mapendekezo yanayoletwa na Serikali. Mwisho Bunge la aina hiyo linakosa hadhi na heshima kwa wananchi na hivyo kukaribisha aina nyingine za siasa za nje ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile ulichapishwa katika Gazeti tarehe 4 Novemba, 2011, Muswada huu ungeweza kuwasilishwa kwa ajili ya Kusomwa kwa Mara ya Kwanza katika Mkutano wa Tano wa Bunge hili Tukufu ulioanza tarehe 8 Novemba, 2011. Hii ingeipa Kamati husika, Wabunge wote na wadau wengine nje ya Bunge muda wa kutosha kufanya maandalizi kwa ajili ya mjadala wa kuipitisha katika Mkutano huu wa Bunge. Badala yake, Bunge hili Tukufu sasa linatakiwa kuujadili na kuipitisha Muswada ambao hauna sababu yoyote ya dharura, siku mbili tu baada ya Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya kuongezeka kwa hatari ya Bunge hili Tukufu kugeuzwa kuwa la kugonga muhuri Miswada na mapendekezo ya Serikali, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Kamati ya Uongozi ya Bunge pamoja na wewe mwenyewe kutumia mamlaka yenu chini ya kanuni za 80(5) na (6) na Kanuni ya 93(2)(b) ya Kanuni za Bunge kulinda mamlaka, hadhi na heshima ya Bunge hili Tukufu kwa kuhakikisha kwamba Miswada ya Sheria isiyokuwa na dharura yoyote inawasilishwa, kujadiliwa na kupitishwa kwa kutumia utaratibu wa kawaida uliowekwa na Sehemu ya Nane ya Kanuni za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kujadili mapendekezo ya marekebisho ya sheria mbalimbali yaliyoko katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada unapendekeza kufanya marekebisho katika vifungu kadhaa vya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura ya 178 ya Sheria za Tanzania. Kwanza, inapendekezwa kurekebisha kifungu cha (5) cha Sheria hiyo kwa kuongeza idadi ya Wajumbe wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kutoka Wajumbe 13 walioko chini ya Sheria ya sasa hadi Wajumbe 14. Hii inafanywa kwa kuongeza mwakilishi wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania na mwakilishi wa wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu za Umma, na kwa kupunguza uwakilishi wa watu mashuhuri wenye utadlamu na uzoefu katika uendeshaji wa Taasisi za Elimu ya Juu. Kwa mujibu wa Sheria ya sasa, Tume ya Vyuo Vikuu na wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu za Umma hawana uwakilishi katika Bodi ya Mikopo.

Pamoja na inayoonekana kuwa nia njema ya kutoa fursa ya uwakilishi wa Taasisi hizi katika Bodi ya Mikopo, hakuna ushahidi wa kuthibitisha kwamba kutokuwepo kwao kumeathiri utendaji wa Bodi ya Mikopo. Aidha, hakuna uhakika kwamba uwepo wao katika Bodi ya Mikopo utaiongezea Bodi hiyo tija yoyote. Hii ni kwa sababu, kwa mujibu wa kipengele cha (9) cha nyongeza ya Sheria ya Bodi ya Mikopo, maamuzi ya Bodi hayawezi kubatilishwa kwa sababu tu ya kutokuwepo kwa Mjumbe, au kutokana na mapungufu ya uteuzi wa Mjumbe yeyote.

Vile vile, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepata taarifa kwamba licha ya kuwa Wajumbe wa Bodi ya Mikopo kwa mujibu wa Sheria ya sasa, mwakilishi wa wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu za binafsi amekuwa haalikwi kwenye vikao vya Bodi kwa nyakati mbalimbali. Hii ina maana kwamba kuongeza uwakilishi wa wanafunzi wa Taasisi za Umma wakati wawakilishi wenzao wa Taasisi za binafsi hawashirikishwi kwenye vikao vya Bodi hakutatua matatizo mbalimbali ya Bodi ya Mikopo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili inayopendekezwa kurekebisha ni kifungu cha (7) cha Sheria ya Bodi ya Mikopo. Kifungu hiki kinaainisha mamlaka mbalimbali ya Bodi ya Mikopo. Hapa inapendekezwa kurekebisha kifungu cha 7(i) kwa kuipa Bodi mamlaka ya kuamua idadi ya juu ya wanafunzi wanaostahili kupatiwa mikopo kila mwaka kwa kuzingatia ukomo wa bajeti ya Serikali. Kwa mujibu wa Madhumuni na sababu za Muswada huu, kwa sasa Sheria, inaelekeza mikopo itolewe kufuatana na vigezo vya ukopeshaji ambavyo vinaruhusu wanafunzi wengi kukopeshwa bila kuzingatia ukomo wa bajeti. Pendekezo hili linaleta dhana potofu kwamba Bodi inatoa mikopo kwa wanafunzi wengi bila kuzingatia ukomo wa bajeti inayotolewa kwa Bodi kwa ajili hiyo.

Ukweli, kama Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo alivyoieleza Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ni kwamba Bodi ya Mikopo inazingatia ukomo wa bajeti ya Serikali kwa sababu Serikali ndiyo chanzo pekee cha fedha za mikopo ya wanafunzi zinazotolewa na Bodi. Kwa hiyo, hata bila kuwepo kwa maneno 'kwa kuzingatia ukomo wa bajeti ya Serikali' kwenye Sheria hii, Bodi ya Mikopo inalazimika kuendelea kuzingatia ukomo wa bajeti ya Serikali katika kutoa mikopo kwa wanafunzi! Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba sababu halisi ya pendekezo hili ni kuipa Bodi ya Mikopo na Serikali kinga ya kisiasa dhidi ya tuhuma kwamba imeshindwa kutatua matatizo makubwa ya mikopo ya wanafunzi ambayo yamepelekea migogoro isiyokwisha kati ya Serikali na wanafunzi karibu taasisi zote za elimu ya juu nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu inayopendekezwa kurekebisha ni kuiongezea Bodi ya Mikopo mamlaka ya kutoa ruzuku (*grants*), msaada wa masomo (*bursary*) na fedha za kusomea (*scholarships*). Hata hivyo, utekelezaji wa lengo hili zuri unaelekea kukanushwa na kuffishwa na sharti la 'uwepo wa fedha' ambalo limewekwa katika pendekezo la kifungu kipya cha 7 (j) cha Sheria ya Bodi ya Mikopo. Kama imeshindikana kuwapa wanafunzi mikopo wanayohitaji kila mwaka kwa madai ya uhaba wa fedha, Bodi ya Mikopo itatumia muujiza gani kupata fedha za kutoa ruzuku? Fedha za msarifu na misaada ya masomo ambayo kwa kawaida hutolewa bure kwa wanafunzi wanaostahili?

Pendekezo la kifungu kipya cha 7 (k) nalo linatia mashaka makubwa juu ya utekelezaji wake. Kifungu hicho kinapendekeza kuipa Bodi ya Mikopo mamlaka ya kuomba na kupatiwa taarifa za wanufaika wadaiwa wa mikopo kutoka kwenye mifuko ya hifadhi za jamii kama vile LAPF, NSSF, POPF na PSPF.

Masharti haya yatazihusu pia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA). Kwa vile hakuna masharti kwa Taasisi zote hizi kuisaidia Bodi ya Mikopo kukusanya madeni ya wanufaika wadaiwa, kama ilivyo kwa waajiri kwa mujibu wa vifungu vya 20 na 21 vya Sheria ya Bodi ya Mikopo, haieleweki ni kwa namna gani taarifa za wanufaika wadaiwa zilizoko kwenye mifuko ya hifadhi za jamii au BRELA au TRA zitarahisisha urejeshwaji wa mikopo inayodaiwa, kama inavyodaiwa kwenye Madhumuni na Sababu za Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tano lenye utata linahusu mapendekezo ya marekebisho ya vifungu vya 16 na 17 vya Sheria ya Bodi ya Mikopo. Kifungu cha 16 kinaipa Bodi wajibu kisheria wa kutoa mikopo kwa wanafunzi; mamlaka ya kupanga asilimia ya gharama za Elimu ya Juu ambayo mwanafunzi atatakiwa kuchangia, na kinachomtaka mwanafunzi kuchangia kiwango cha fedha, sawa na asilimia ambayo imepangwa na Bodi. Kwa mujibu wa mapendekezo ya marekebisho, mikopo sasa itatolewa kwa wanafunzi waliodahiliwa moja kwa moja kwenye taasisi ya Elimu ya Juu baada ya kumaliza Elimu ya Sekondari. Aidha, inapendekezwa kwamba wanafunzi wanaotokea makazini hawatastahili kupewa mikopo, ijapokuwa makatazo haya hayatawahusu wanafunzi waliodahiliwa kusomea taaluma za kipaumbele cha kitaifa.

Kwa upande mwingine, kifungu cha 17 kinaainisha sifa mbalimbali anazotakiwa kuwa nazo mwombaji wa mikopo. Sasa inapendekezwa kwamba licha ya sifa hizo, Bodi ya Mikopo inatakiwa iangalie

pia uwezo wa kitaaluma wa mwombaji, mahitaji yake na udahili katika taaluma za kipaumbele kitaifa. Vile vile Bodi inatakiwa kuangalia mwenendo wa zamani wa mwombaji katika kulipa ada katika Shule za Sekondari, uwezo wa kifedha wa mzazi au mlezi, na hali ya kifamilia kwa maana ya uyatima au ulemavu wa mwombaji.

Hata hivyo, licha ya masharti haya mapya, Bodi inatakiwa kuwapa kipaumbele wanafunzi waliodahiliwa katika kozi za kipaumbele kitaifa zilizoainishwa katika nyongeza ya pili inayopendekezwa kuingizwa katika Sheria. Kozi zinazotajwa katika nyongeza hiyo ni pamoja na Ualimu wa Sayansi na Hisabati, Sayansi, Sayansi za Udaktari na Uhandisi. Nyingine ni Sayansi za Kilimo, Mifugo, Udaktari wa Mifugo na Hisabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo haya yanazua maswali mengi ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuyajibu mbele ya Bunge hili Tukufu. Kwanza, mapendekezo ya marekebisho ya kifungu cha 16 yanakinzana moja kwa moja na masharti ya kifungu cha 17 cha Sheria ya sasa. Hii ni kwa sababu, wakati marekebisho yanapendekeza wanafunzi waliotokea makazini wasipewe mikopo isipokuwa tu kama wamedahiliwa kusomea taaluma za kipaumbele kitaifa, kifungu cha 17(1) (e) cha Sheria ya sasa kinampa haki ya kufikiwa kupatiwa mkopo kila mwanafunzi anayeendelea na masomo na ambaye amefaulu mitihani ya kumwezesha kuendelea na masomo kwa mwaka au hatua ya masomo inayofuata. Kifungu hiki hakijaguswa kabisa na mapendekezo ya marekebisho ya kifungu cha 17.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya ukimya huu, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe tamko rasmi mbele ya Bunge hili Tukufu kama athari za kupitishwa kwa mapendekezo ya ibara ya (6) ya Muswada huu ni pamoja na kurekebisha, *by implication*, masharti ya kifungu cha 17(1)(e) ya Sheria ya sasa kwa kadri inayowahusu wanafunzi waliotokea makazini. Vile vile, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itamke hadharani kama wanafunzi wanaotokea makazini, na ambao kwa mujibu wa kifungu cha 17(1)(e) cha Sheria ya sasa wanastahili kupatiwa mikopo, watanyimwa mikopo hiyo endapo mapendekezo ya marekebisho ya kifungu cha 16 yatapitishwa na kuwa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari ya pili ya kupitishwa kwa mapendekezo ya marekebisho ya vifungu vya 16 na 17 vya Sheria ya Bodi ya Mikopo itakuwa ni kuingiza ubaguzi mkubwa katika mfumo wa utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu katika nchi yetu. Kwa mfano, wanafunzi wanaotokea makazini sasa wataweza kunyimwa mikopo wakati wanafunzi wanaotokea Shule za Sekondari moja kwa moja watakuwa na haki ya kupata mikopo hata kama wote wanasomea taaluma zile zile. Aidha, wanafunzi waliodahiliwa katika kile kinachoitwa 'kozi za kipaumbele kitaifa' watakuwa na haki ya kupatiwa mikopo wakati wanafunzi wenzao waliodahiliwa katika kozi nyingine zilioruhusiwa na Serikali kupitia Tume ya Vyuo Vikuu hawatakuwa na haki hiyo. Kama ni hivyo, kwa nini Serikali isitangaze wazi kwamba ni marufuku kwa wanafunzi wa Kitanzania kusomea taaluma ambazo Serikali inaziona siyo za kipaumbele kitaifa? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo haya yanaleta ubaguzi mkubwa pia kati ya maskini na matajiri hapa nchini na kati ya wanafunzi wanaotokea vijijini na wale wanaotokea mijini. Hii ni kwa sababu hakuna mtu anayeweza kubishia ukweli kwamba Shule za Sekondari za Kata ambazo zimejengwa kwa maelfu katika maeneo ya vijijini, ni shule za watoto wa maskini ambao kwa kiasi kikubwa wanaishi vijijini. Vile vile, hakuna anayeweza kubishia ukweli kwamba shule hizo zina upungufu mkubwa wa karibu kila kitu kinachotakiwa katika elimu ya sekondari, kuanzia Walimu wa masomo yote, vyumba vya madarasa, maabara kwa ajili ya masomo ya sayansi, maktaba, vitabu, madawati, mabweni, chakula, maji, umeme na kadhalika. Aidha, hakuna anayeweza kubishia ukweli kwamba shule nyingi za binafsi na za Serikali zinazoongoza kwa ubora wa miundombinu yake na ubora wa mahitaji ya kitaaluma ndizo zinazoongoza kwa viwango vya ufaulu na ndizo zinazosomesha wanafunzi wanaotoka kwenye familia tajiri na/au za wenye kipato kikubwa. Nyingi ya shule hizi pia ziko maeneo ya mijini au pembezoni mwa miji na kwa hiyo zimeunganishwa na miundombinu bora ikilinganishwa na shule za vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu za upungufu wa mahitaji haya muhimu kielimu, ufaulu wa wanafunzi wa Shule za Sekondari za Kata ni wa chini sana kulinganisha na ufaulu wa wanafunzi wa Shule za Sekondari za Binafsi au za Serikali zilizoko kwa kiasi kikubwa katika maeneo ya mijini. Kwa mapendekezo ya marekebisho ya kifungu kipya cha 17(3)(a)(i) cha Sheria ya Bodi ya Mikopo, itakuwa ndoto kwa wanafunzi wanaotoka katika familia maskini za vijijini na mijini na ambao wamesomea katika Shule za

Sekondari za Kata kupatiwa mikopo kwa sababu ya ufaulu wa chini kwa ujumla wa shule hizo na kwa sababu ya ufaulu wa chini katika masomo ya sayansi ambao utawazuia wanafunzi hao kusomea 'taaluma za kipaumbele kitaifa.'

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, kwa mapendekezo haya, ni wanafunzi wanaotoka familia zenye vipato vikubwa na wanaoishi maeneo ya mijini na kusomea katika shule bora za binafsi na za Serikali ndio pekee watakaokuwa na haki ya kupatiwa mikopo na Bodi ya Mikopo kwa sababu ya viwango vyao vikubwa vya ufaulu katika masomo yote kwa ujumla na hasa hasa katika masomo ya sayansi. Endapo mapendekezo haya yatapatishwa na kuwa Sheria, Bunge hili Tukufu na Serikali ya Chama cha Mapinduzi itakuwa imetimiza kile kilichoandikwa katika Maandiko Matakafifu kwamba 'aliyenacho ataongezewa na asiyekuwa nacho atanyang'anywa hata kile kidogo alichu nacho'! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 13(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inatamka wazi kwamba "ni marufuku kwa sheria yoyote iliyotungwa na mamlaka yoyote katika Jamhuri ya Muungano kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taathira yake." Ibara ya 13(5) inatafsiri neno 'kubagua' kumaanisha "... kutimiza haja, haki au mahitaji mengineyo kwa watu mbalimbali kwa kuzingatia ... pahala walipotokea ... au hali yao ya maisha kwa namna ambayo watu wa aina fulani wanafanywa ... dhaifu au duni na kuwekewa vikwazo au masharti ya vipingamizi ambapo watu wa aina nyingine wanatendewa tofauti au wanapewa fursa au faida iliyoko nje ya masharti au sifa za lazima..." Vile vile, Ibara ya 11(2) inatamka wazi kwamba "kila mtu anayo haki ya kujielimisha, na kila raia atakuwa huru kutafuta elimu katika fani anayopenda hadi kufikia upeo wowote kulingana na stahili na uwezo wake." Zaidi ya hayo, Ibara ya 11(3) inaitaka Serikali kufanya "... jitihada kuhakikisha kwamba watu wote wanapata fursa sawa na za kutosha kuwawezesha kupata elimu na mafunzo ya ufundi katika ngazi zote za shule na vyuo vinginevyo vya mafunzo."

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jana tu Bunge hili Tukufu limepitisha Azimio la Kuridhia Mkataba wa Vijana wa Afrika wa mwaka 2006. Ibara ya 2(2) ya Mkataba huo inazitaka nchi wanachama kuchukua "... hatua zinazofaa kuhakikisha vijana wandilindwa dhidi ya aina zote za ubaguzi kutokana na hali ... walizo nazo." Hata kabla wina uliotumika kuandikwa Azimio hilo haujakauka, Bunge hili Tukufu linaombwa kupitisha Sheria ambayo itaongeza ubaguzi kati ya vijana maskini na matajiri na kati ya vijana wanaosomea Shule za Kata zilizoko vijijini na wale wanaosomea Shule za Binafsi na/au za Serikali zilizoko mijini!

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa kauli mbele ya Bunge hili Tukufu kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya vifungu vya 16 na 17 ambayo ni ya kibaguzi kwa 'dhahiri na kwa taathira yake', na kwa hiyo yanakiuka Katiba yetu. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulithibitishia Bunge hili Tukufu kwamba ubaguzi huu katika mfumo wa utoaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu nchini unalenga kurekebisha matatizo gani mahsusi katika jamii yetu ili uweze kuhesabika kuwa sio 'ubaguzi' kwa minajili ya Ibara ya 13(5) ya Katiba yetu. Kama Serikali itashindwa kutoa maelezo ya kuridhisha juu ya mapendekezo haya ya kibaguzi katika Sheria ya Bodi ya Mikopo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawaomba Waheshimiwa Wabunge wote, bila kujali itikadi au kambi za kichama, wapige kura ya nafsi (*conscience*) zao kukataa kupitisha Muswada huu kuwa sheria. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa utoaji mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu nchini umekuwa na migogoro mingi na inayoelekea kuwa sugu. Kiashiria kikuu cha migogoro hii ni migomo ya mara kwa mara ya wanafunzi wa taasisi karibu zote za elimu ya juu hapa nchini ambayo imepelekea masomo kukatishwa, vyuo vikuu vingi kufungwa na wanafunzi wengi kufukuzwa vyaoni na wengine wengi kukamatwa na kufunguliwa mashtaka ya jinai Mahakamani. Aidha, vyuo vingi vimekuwa kama uwanja wa mapambano vyenye kukaliwa kwa nguvu za kijeshi na vikosi vya kuzuia ghasia vya Jeshi la Polisi. *Militarization* hii ya vyuo vikuu vya nchi yetu imeenda sambamba na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu za wanafunzi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira haya, mwezi Machi mwaka jana Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete aliteua Tume chini ya Uenyekiti wa Profesa Makenya Maboko wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kuchunguza kiini na sababu za migogoro isiyoisha katika vyuo vyetu vikuu pamoja na mfumo mzima wa utoaji mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu hapa nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kwamba Tume ya Profesa Maboko ilikamilisha kazi yake baada ya kufanya uchunguzi ndani

na nje ya nchi yetu na kuwasilisha ripoti yake kwa Mheshimiwa Rais mnamo mwezi Oktoba, 2011. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitegemea – kwa kuzingatia unyeti na udharura wa hali ya sasa katika vyuo vyetu vikuu – kwamba Serikali ingewasilisha ripoti ya Tume ya Profesa Maboko hapa Bungeni sambamba na Muswada huu ili iwasaidie Waheshimiwa Wabunge kuelewa kiini na sababu za matatizo ya mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na kuweza kuchangia katika uboreshaji wa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, licha ya jitihada nyingi, sio Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala wala Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliyopatiwa nakala ya ripoti ya Tume hiyo. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa kauli kwa Bunge hili Tukufu ni kwa nini ripoti ya Tume ya Profesa Maboko imefichwa hadi sasa hivi, licha ya kutumia mamilioni ya fedha za walipa kodi wa Tanzania. Aidha, Serikali itoe kauli ni lini, kama nia hiyo ipo, ripoti hiyo itatolewa hadharani ili sisi wawakilishi wa wananchi tuweze 'kuisimamia na kuishauri' ipasavyo Serikali juu ya masuala ya mikopo kwa wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu hapa nchini, kama ilivyo wajibu wetu kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Biashara ya Madawa ya Kulevya, Sura ya 95 ya Sheria za Tanzania. Inapendekezwa kwamba Sheria ya Kuzuia Biashara Haramu ya Madawa ya Kulevya, Sura ya 95 ya Sheria za Tanzania irekebishwe ili kuongeza adhabu kwa makosa kadhaa yanayohusiana na madawa ya kulevya. Inapendekezwa, kwa mfano, kwamba adhabu ya kosa la kupatikana na madawa ya kulevya au mchanganyiko wa madawa hayo, au la kufanya au kushindwa kufanya tendo au kitu chochote kuhusiana na madawa ya kulevya iwe ni kifungo cha maisha. Adhabu ya sasa kwa makosa hayo, kwa mujibu wa kifungu cha 16(1)(a) cha Sheria ya Kuzuia Madawa ya Kulevya, ni faini ya shilingi milioni kumi au mara tatu ya thamani ya madawa au mchanganyiko wa madawa hayo katika soko au yoyote iliyo kubwa zaidi katika faini hizo, au kifungo cha maisha au vyote viwili, yaani kifungo cha maisha na faini.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapendekezwa pia kuongeza adhabu ya kosa la kufanya biashara ya madawa ya kulevya kuwa kifungo cha maisha. Adhabu ya kosa hilo, kwa mujibu wa kifungu cha 16(1)(b) cha Sheria ya sasa, ni faini ya shilingi milioni kumi au mara tatu ya thamani ya madawa hayo katika soko au yoyote iliyo kubwa zaidi katika faini hizo, na kifungo kisichopungua miaka ishirini hadi kifungo cha maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, makosa mengine ambayo yanapendekezwa kuongezewa adhabu ni pamoja na kuvuta, kunusa au kutumia madawa ya kulevya kwa namna nyingine; kuvuta, kunusa au kutumia madawa hayo ndani ya nyumba, chumba au mahala pengine; kukutwa na kiko au vifaa vingine vinavyotumika kuvutia, kunusia au kutumia madawa hayo. Endapo mapendekezo ya Muswada huu yatapitishwa na kuwa sheria, adhabu ya makosa hayo itakuwa faini ya shilingi milioni moja au kifungo cha miaka kumi au vyote viwili, yaani kifungo na faini.

Mheshimiwa Naibu Spika, adhabu hii ni sawa na adhabu ya makosa hayo chini ya kifungu cha 16(2)(a) na (b) cha Sheria ya sasa ambacho kinapendekezwa kufutwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haifahamu hasara au matatizo yaliyokuwa yanatokana na makosa hayo kuwekwa katika kifungu cha 16 (a) na (b) cha Sheria. Vivyo hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haijafahamishwa juu ya faida, kama ipo, ya kuyahamisha makosa hayo na adhabu zake kutoka kifungu cha 16(2)(a) na (b) kwenda kifungu kipyua cha 17A kinachopendekezwa na Muswada huu. Inaelekea pendekezo la marekebisho ya kifungu hiki yameletwa Bungeni bila kuzingatia ufinyu wa muda wa Bunge hili Tukufu na kwa hiyo Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza mapendekezo haya yasikubaliwe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unapendekeza pia kuongeza adhabu ya makosa ya wamiliki, watumiaji au wasimamizi wa majengo au vyombo vya usafiri wanaoruhusu majengo au vyombo vyao kutumiwa kuandaa au kuzalisha madawa ya kulevya; au wanaokutwa na vyombo au vifaa vya kutengenezea madawa ya kulevya. Adhabu ya sasa ya makosa hayo ni faini ya shilingi milioni moja au kifungo cha miaka kumi au vyote viwili, yaani kifungo na faini. Adhabu inayopendekezwa katika kifungu kipyua cha 17B ni kifungo cha maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri na ni busara kwa Bunge lako Tukufu kuhoji sababu halisi za mapendekezo ya kuongeza adhabu za makosa haya. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Mheshimiwa William

Vangimembe Lukuvi kwamba "matumizi na upatikanaji wa dawa za kulevya bado ni tatizo kubwa hapa nchini." Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu hatari kwa nchi yetu na madhara kwa jamii yetu kutokana na matumizi ya madawa ya kulevya; na hivyo umuhimu wa kuendelea kupiga vita biashara na matumizi haramu na hatari ya madawa ya kulevya hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa uchambuzi wa Muswada huu, Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala ya Bunge lako Tukufu ilipata ushuhuda kutoka kwa Kamishna Christopher J. Shekiondo wa Tume ya Kuratibu Udhubiti wa Dawa za Kulevya nchini. Katika ushuhuda wake, Kamishna Shekiondo alieleza Kamati kwamba ni muhimu kwa adhabu za makosa ya madawa ya kulevya zikaongezwa kama inavyopendekezwa kwa sababu tatizo la biashara hii haramu na matumizi ya dawa hizi imekuwa ikiongezeka hapa nchini. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haitakuwa inakosea kwa kuamini kwamba hii ndiyo sababu au *rationale* pekee ya mapendekezo ya kuongeza adhabu hizi kama inavyopendekezwa na Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu na *rationale* ya kuongeza adhabu kwa makosa ya madawa ya kulevya kama inavyopendekezwa haiendani na hali halisi ya tatizo la biashara na matumizi ya madawa ya kulevya nchini. Aidha, maelezo aliyoyotoa Kamishna Shekiondo kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala hayalingani na ushahidi uliopo katika taarifa mbalimbali rasmi zilizoandaliwa na Tume ya Kuratibu Udhubiti wa Dawa za Kulevya na kuwasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu kwa mujibu wa kifungu cha 6 cha Sheria ya Kuzuia Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya. Kwa mfano, katika Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2010, Tume hiyo imeonyesha kwamba kiasi cha bangi kilichokamatwa mwaka 2010 ni tani 4.03 ikilinganishwa na tani 964.1 zilizokamatwa mwaka 2004. Vilevile, wastani wa kiasi cha bangi kilichokamatwa kila mwaka katika kipindi cha miaka mitano kufikia mwaka 2010 ulikuwa ni tani 80.4 ukilinganishwa na wastani wa tani 441.8 zilizokamatwa kwa mwaka kati ya 2001 na 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa za Tume ya Kuratibu Udhubiti wa Dawa za Kulevya zinaonyesha pia kupungua kwa biashara ya mandrax, morphine, bangi iliyosindikwa na bangi kavu katika kipindi cha miaka kumi kati ya mwaka 2000 na 2010. Ni kweli kwamba takwimu za Tume zinaonyesha kuongezeka kwa biashara ya madawa ya *heroin* na *cocaine*. Kwa mfano, kiasi cha *heroin* kilichokamatwa kimeongezeka kutoka kilo 5.3 mwaka 2000 hadi kilo 185.8 mwaka 2010; vilevile, kiasi cha *cocaine* kilichokamatwa katika kipindi hicho kimeongezeka kutoka kilo 2.104 mwaka 2000 hadi kilo 62.966 mwaka 2010, ikiwa "... ni takriban mara mbili zaidi ya kiasi chote kilichowahi kukamatwa katika kipindi cha miaka kumi iliyotangulia." Aidha, idadi ya kesi zinazotokana na madawa ya *heroin* imeongezeka kutoka kesi 160 mwaka 2000 hadi kesi 317 mwaka 2009 na ile ya *cocaine* imeongezeka kutoka kesi 36 mwaka 2000 hadi kesi 336 mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Takwimu za Tume zinaonyesha kwamba idadi ya watuhumiwa wa makosa wa biashara ya *heroin* imepungua kutoka watuhumiwa 412 mwaka 2001 hadi watuhumiwa 15 mwaka 2010 na wale wa biashara ya *cocaine* wamepungua kutoka watuhumiwa 251 mwaka 2008 hadi watuhumiwa 8 mwaka 2010. Hii ni licha ya kuongezeka kwa kiwango cha madawa hayo kinachokamatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kimoja ambacho hakionyeshwi na Taarifa pamoja na takwimu zote za Tume ya Kuratibu Udhubiti wa Biashara ya Dawa za Kulevya ni idadi ya watuhumiwa waliopatikana na hatia ya makosa haya Mahakamani. Kamishna Shekiondo alipoulizwa juu ya jambo hili kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala alijibu kwamba ni mtu mmoja tu ambaye amepatikana na hatia ya makosa haya katika kipindi chote cha Taarifa za Tume! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamishna Shekiondo, alielezea sababu ya hii ya kustaajabisha kuwa ni rushwa iliyokithiri katika Mahakama zetu ambapo alisema watuhumiwa wengi wamekuwa wakiachiliwa huru kwa sababu ya kutoa rushwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kauli ya Kamishna Shekiondo kuhusiana na sababu za watuhumiwa wa biashara haramu ya dawa za kulevya kutopatikana na hatia Mahakamani ni ya kuaminiwa, basi ni wazi kwamba tatizo la kuendelea kushamiri kwa biashara haramu ya dawa za kulevya nchini halitokani na udogo wa adhabu zilizowekwa na Sheria ya sasa kwa makosa hayo bali ni rushwa na uozo ulioko Mahakamani na kwenye mamlaka za uandaaji na uendeshaji mashtaka ya makosa hayo.

Kwa maana hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba dawa ya tatizo la rushwa na ufisadi katika taasisi hizo haiwezi kuwa kuongeza adhabu za makosa hayo bali kuzisafisha Mahakama na taasisi za uandaaji na uendeshaji mashtaka ili kuondokana na rushwa na ufisadi huo! Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haiwezi kuunga mkono mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya yaliyoko kwenye Muswada huu kwani hayalengi kuondoa kiini cha tatizo ambacho ni rushwa na ufisadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaridhika na maoni na ushauri wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusiana na mapendekezo ya marekebisho mengine ya Sheria yaliyoko kwenye Muswada huu na haioni haja ya kuyarudia maoni na ushauri huo. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani chini ya uongozi wa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman A. Mbowe kwa ushauri na ushirikiano uliowezesha maandalizi ya hoja hii. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala, chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, kwa michango yao mbalimbali wakati wa kujadili Muswada huu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nichukue fursa hii kumshukuru Msaidizi wa Masuala ya Kibunge, Oliver Mwikila, kwa msaada na ushauri wa kitaalam uliofanikisha maandalizi ya hoja hii. Mwisho naomba nichukue fursa hii kuwashukuru viongozi, wanachama na wapenzi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na wananchi wote wa Tanzania ambao wameendelea kutuunga mkono na kututia nguvu katika kipindi hiki muhimu katika historia ya nchi yetu. Msimamo wetu ni ule ule, hakuna kulala mpaka kieleweke! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema kwamba siungi mkono hoja. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Huyo alikuwa ni Mheshimiwa Tundu Lissu, Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika Wizara hiyo ya Sheria na Katiba. (Makofi)

Sasa kama nilivyosema, kwa kweli wachangiaji ni wengi sana na kwa vyovyote vile jambo hili itabidi tuendelee nalo kesho. Kabla sijawaita wachangiaji niliokuwa nimewataja mwanzo kwa kuanzia, naomba niwatangazie Wabunge wote wa CCM kuwa, kutakuwa na kikao cha Chama mara tu baada ya kuahirishwa kwa Bunge hili, Ukumbi wa Pius Msekwa. Tangazo hili limeletwa na Katibu, Mheshimiwa Jenista Mhagama.

Sasa namwita Mheshimiwa, Dokta Faustine Ndugulile, Mheshimiwa Angellah Kairuki, ajiandae.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kuwa mchangiaji wa kwanza katika Muswada huu wa *Miscellaneous Amendment*. Kwa niaba ya Kamati ya Huduma za Jamii, sisi tunapinga moja kwa moja Muswada huu. Kamati yetu ya Huduma za Jamii ambayo inasimamia Sekta ya Elimu na Afya, haikushirikishwa kwa namna yoyote katika uandaaji wa Sheria hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tutoe masikitiko yetu kwamba, hata pale Mheshimiwa Rais alipokuwa ameteuwa Tume ya kuzunguka kuangalia chanzo cha migogoro katika Bodi ya Mikopo, Taarifa tuliyotolewa na kupewa na Wizara ilikuwa ni ya vipandevipande. Kwa hiyo, ile Taarifa haikuweza kutupa sisi mwelekeo wa kuweza hata kuchangia namna bora ya kutatua migogoro ya mikopo katika nchi yetu. Vilevile Rasimu hii ya Sheria na sisi hatujaiona hadi leo hii na sisi tunaikuta hapa Mezani, kwa hiyo, sisi hatuungi mkono. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rasimu ya Sheria hii itatuletea migogoro na migomo katika Vyuho vyetu vya Elimu ya Juu. Rasimu ya Sheria hii, si rafiki wa Elimu ya Juu Tanzania. Rasimu ya Sheria hii itatuweka kwenye migongano na vijana wetu wanaohitaji elimu nchini Tanzania. Waheshimiwa Wabunge, nitaomba sana mtuunge mkono katika hili. Sisi kama Wabunge na wawakilishi wa wananchi tukiunga mkono Muswada huu, hatutakuwa na sehemu ya kuweka nyuso zetu tukitoka hapa. Tutawaambia nini vijana wa Tanzania ambao wapo elimu ya juu? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma tumezungumzia sanasana suala la *means testing* tukawaambia wenzetu tukae tuangalie njia bora za kuboresha hii *means testing*. Hii *means testing* mpaka

sasa hivi hata kwa Sheria hii ambayo imekuja bado haijafanyiwa maboresho ya kutosha, tukiruhusu ikaendelea namna hii migogoro na migomo katika Vyuo Vikuu haitaisha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii inaleta ubaguzi kati ya watoto wa maskini na watoto wa matajiri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kamati yetu tulishauri Serikali tusingalie sana vipaumbele, tuangalie uhitaji, tuchukulie mfano mtoto wa Mbunge, mtoto wa Waziri, amesoma shule nzuri ya *private* akafaulu akaenda kusoma *medicine*, lakini kuna mtoto yatima katika familia ya watoto kumi na hii ndiyo mifano ambayo ninayo kwangu, vijana wangu kule Mbagala, kijana katika familia maskini ya watoto kumi kajitahidi kusoma, kachaguliwa kwenda kusoma Sheria anakataliwa kwenda kusoma, hatma ya kijana huyu ni nini? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *means testing* tuliangalie vizuri kuhakikisha vijana wetu waliokuwa wanasoma katika Shule zetu za Kata na ambazo shule zenyewe sisi tumezjenga, tuwape kipaumbele. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua mahitaji ya hizi kada maalum lakini kwa kweli uhitaji nao tuangalie kwa namna ya peke yake. Kuna watumishi wetu kule vijijini, *Clinical Officers, Assistant Medical Officers, Assistant Nursing Officers* na hao ambao wanataka kujiendeleza katika elimu lakini kwa sheria hii nayo inawabagua. Tunatuma ujumbe gani kwamba kusoma ni dhambi, tuikatae. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika Sheria hii tunaongelea suala la *interest rates* katika masuala ya mikopo, mimi kwa ushauri wangu nafikiria badala ya kuiacha ikawa wazi tuweke vigezo *interest rate* iwe *fixed*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna hili suala kwamba *TRA*, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, *BRELA*, wawe wanatoa taarifa za mtu kuhusiana na udaiwa wake, jamani kuna masuala ya *privacy* hapa na vilevile hatujui kwamba hizo taarifa wewe ukishajua mimi na *own* kampuni, wewe inakusaidiaje katika kudai hela yako? Sasa lazima tukae tuweke utaratibu mzuri, badala ya kuongezea majukumu mengine yasiyokuwa na msingi katika taasisi hii kwa kuwa wanatoa taarifa ambazo kwa kweli nazo zinamlinda mtu kwa sababu kuna masuala ya siri kwamba na mtu naye anaweza kuwa analinda taarifa zake zisiwe zinatoka hovyohovy. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna kifungu sasa nahamia kwenye *Traffic Law*, nimeshtuka sana na Waheshimiwa Wabunge sijui kama ninyi mmeona wanataka ku-*introduce point system* katika *leseni* za udereva, sijui kama ninyi mlikuwa mna taarifa ya suala hili. Hilo linakuja hapa, hakuna elimu ya kutosha, hakuna uhamasishaji wa kutosha na sijui kwa nini tunakuwa na uharaka na hili suala linakuja kwa kifichoficho. Nafikiri hakuna haja ya kuleta hivi vitu vya uharaka, tunahitaji tukae tutulize vichwa chini, tutafakari, tupanue wigo wa majadiliano ili tuje na kitu bora kwa maslahi ya nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia Kanuni ya 69(1), naomba kutoa hoja kwamba mjadala huu uahirishwe mpaka kikao kingine cha Bunge ili kutoa muda wa kutosha kuafikiana, naomba Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono katika hili. (Makofi)

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. (Makofi)

(Hoja iliitolewa na iliungwa mkono na Wabunge wengi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, umetumia Kanuni gani?

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Naibu Spika, nimetumia Kanuni ya 69(1) kuomba kwamba mjadala huu sasa uahirishwe hadi mwezi wa nne ili kupata fursa ya kutosha kwa Waheshimiwa Wabunge kufanya majadiliano na *consultation*.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, wakati tunaendelea kutafakari kuhusu hilo, nimeona hoja hiyo imeungwa mkono, sasa naomba nimwite mchangiaji wa pili...

WABUNGE FULANI: Aaaaaah!

NAIBU SPIKA: Halafu nitatoa majibu ya hoja hii muda si mrefu.

MBUNGE FULANI: Eeh, hatari!

MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuwa mchangiaji wa pili katika Muswada huu uliopo mbele yetu wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunatambua kwamba mfumo wa sasa wa utoaji wa mikopo wa elimu ya juu unakabiliwa na changamoto nyingi na unagubikwa na migomo na migogoro mbalimbali ambayo imekuwa ikikabili taasisi za elimu ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo unaotumika sasa kwa kweli siyo endelevu kwani waombaji ni wengi na bajeti ambayo imekuwa ikitolewa ni ndogo. Vilevile mfumo huu ambao unatumika hivi sasa usimamizi wake wa fedha kwa kweli sio madhubuti unatakiwa uimarishwe ili kuhakikisha kwamba fedha husika zinawafikia walengwa wa mikopo hiyo na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, yamejitokeza matukio mbalimbali mfano kumekuwa na wanafunzi hewa ambapo mikopo imekuwa ikiidhinishwa kwa ajili yao wakati hawapo. Kwa kweli Sheria hii inatakiwa kuandikwa upya na si kuleta tu marekebisho haya madogo kwani mfumo mzima umeoza, tutakapoleta kifungu kimoja kimoja inaleta matatizo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema huko baadaye tufikirie kuifanyia marekebisho makubwa Sheria hii inayohusiana na Bodi ya Mikopo ili kuhakikisha mfumo mzima baadaye unakuwa endelevu na sahihi kabisa.

WABUNGE FULANI: Toa hoja!

MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI: Nini ninyi? Mimi naiunga mkono hoja, kwa hiyo, naomba mniache niendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema badala ya kuendelea na mfumo huu tukaanzisha benki mahsusi ambayo itakuwa ikisimamia mfumo wa elimu ya juu ambapo wanafunzi wataweza kupewa mikopo lakini pia watu mbalimbali ambao wanamiliki vyo mbalimbali vya elimu ya juu wanaweza wakakopeshwa ili kuweza kufanya miradi mbalimbali ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi hii ya Mikopo ilipoanzishwa ilikuja kama baraka, watu wengi walijua wataweza kufaidika na elimu na kupata mikopo hiyo lakini kinyume chake wanafunzi wengi wamekuwa wakiomba lakini wamekuwa wakipata masikitiko, wamekuwa hawapati mikopo hiyo. Bodi hii imekuwa ikilalamika sana kwa ukosefu wa fedha, lakini ni sawa na mtu ambaye analalamika ana kiu ya maji lakini ameweka miguu yake ndani ya beseni la maji. Yote haya ni kutokana na mfumo mbovu wa kukusanya madeni ya mikopo. Tangu mwaka 1994 mpaka 2011 Bodi hii ya Mikopo imetoa shilingi bilioni 630.6 lakini hadi kufikia mwaka huu ni shilingi bilioni 6.7 tu ambazo zimeweza kurejeshwa, ukiangalia kwa takwimu hiyo ni asilimia moja tu. Hivyo, ni vyema Bodi hii ikaangalia mfumo mzima wa namna ambavyo inaweza ikarejesha fedha ambazo imezikopesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wako wahitimu mbalimbali kuanzia miaka ya nyuma mpaka mwaka 2005 imekuwa ni vigumu kuwapata kutokana na changamoto mbalimbali zilizokuwa zikijitokeza huko nyuma. Bodi ilijitahidi kutengeneza database ili kuweza kuwapata walionufaika na mikopo, ilipata wanufaika 48,948 lakini ni wanufaika 27,000 tu ndiyo walioweza kufahamika mahali walipo. Ni vyema basi Bodi ikaweka mfumo thabiti utakaohakikisha wanafunzi hawafanyi udanganyifu pindi wanapojaza maombi ya fedha za mikopo ili waweze kupatikana kwa urahisi na madeni haya yaweze kulipika. Pia ni vema kukawa na mkakati wa makusudi wa kuwashughulikia wale ambao wanafanya udanganyifu katika maombi ya mikopo kwa kutoa taarifa ambazo si sahihi au anuani ambazo si za kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema kila mwenye sifa ya kusoma akaweza kusoma bila ya kuangalia hali yake kiuchumi. Ukiangalia katika mapendekezo ya Sheria hii katika kifungu cha 5, kinapendekeza kuipa mamlaka Bodi ya Mikopo kuamua idadi ya juu ya wanafunzi wanaostahili kupatiwa mikopo na kwamba mkopo huo utategemea ukomo wa bajeti lakini hapohapo tunaelezwa kwamba wanatumia *means testing* au dhana ya uwezo. Ni vyema wakajikita katika ufaulu badala ya kujikita katika *means testing* kwani unaweza kukuta wengi wana sifa za *means testing* na bado ukashindwa. Kwa hiyo, ni vyema kila mwenye sifa ya ufaulu basi aweze kupatiwa fursa ya kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona katika mapendekezo ya Sheria moja ya kigezo kinachotumika katika *means testing* ni hali ya uyatima pamoja na hali ya ulemavu, wako yatima wengine pia wamekuwa wakisoma katika shule za binafsi na wamekuwa wakihukumiwa kusoma kwao kwenye shule hizi za binafsi kutokana na ufadhili wa watu mbalimbali kwamba wana uwezo. Hivyo basi, tutakavyotumia dhana ya ufaulu itasaidia kuondoa malalamiko ya watu waliosoma katika shule binafsi au watu wengine wenye hali ya uyatima au ulemavu au watu ambao wana mzazi mmoja kwamba walisomeshwa na mtu mwenye uwezo au katika shule yenye fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu cha 6, kinawazuia wafanyakazi ambao wako kazini kwenda kujiendeleza na kwamba hawataweza kunufaika na mikopo, kwa kweli niungane na wasemaji wengine waliotangulia kwamba kifungu hiki kitaleta ubaguzi kwa wafanyakazi ambao wako tayari kujiendeleza na Taifa hili linahitaji wataalam, sasa leo hii tutapataje wataalam waliotosheleza kama mtu anataka kujisomesha mwajiri wake hajampa fursa yeye mwenyewe kwa jitahada zake unamnyima fursa ya kwenda kusoma, kwa kweli hili halikubali kwa mfanyakazi yeyote na nikiwa mwakilishi wa wafanyakazi hili nitalipigia kelele mpaka mwisho wa kufa kwangu. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Toa hoja!

MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kifungu cha 8, kuna mapendekezo kwamba mfanyakazi aliyenufaika na mkopo akatwe asilimia nane ya mshaharagha au *basic salary*, kwa kweli hili halijakaa vizuri. Napendekeza Serikali ije walau na vigezo au jedwali ambalo litakuwa likianisha mapato mbalimbali mfano shilingi milioni moja mpaka shilingi milioni mbili wakatwe asilimia tano, shilingi milioni mbili mpaka shilingi milioni tatu wakatwe labda asilimia nane, shilingi milioni tatu mpaka shilingi milioni nne labda asilimia kumi kutegemea na kipato cha mtu aliyekopeshwa, isiwe ni *blanket* kwa sababu wapo watumishi wengine mishahara yao ni midogo sana. Unapomwekea asilimia nane sawasawa na mtu mwingine anayepata mshahara mkubwa, nimeambiwa kuna Wabunge wengine wanakatwa shilingi 30,000/= kwa kweli ni kiwango kidogo, itenganishwe kutokana na hali na mapato ya mtu mmojammoja isiwe *blanket*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wale ambao wana kipato cha juu watakapotengewa makato tofauti itasaidia mikopo yao kurejeshwa kwa haraka lakini pia itasaidia waombaji wengine na wenyewe waweze kufaidika na mikopo hii ili waweze kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sehemu ya Tatu, ya Nne, ya Tano na ya Sita inayohusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kwa kweli sehemu hizi nne sidhani kama zilikuwa na haja ya kuwepo hapa, ni marudio yasiyokuwa ya lazima, ingeweza kuwa na kifungu kimoja tu ambacho kingeweza kuzitaka taasisi hizo kuweza kupeleka taarifa za wafanyakazi wao au taarifa za wanachama wa mifuko yao katika Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukiangalia pamoja na mapendekezo haya, bado Sheria haituelezi, utakapopata taarifa zile inakusaidiaje wewe katika kurejesha mikopo kwani tunaelezwa kwamba bado *database* wanayo, walipata wafanyakazi 48,000 lakini wamefanikiwa kupata marejesho kutoka kwa watu 26,000 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niingie katika Sheria kuhusiana na mapato yanayopatikana kwa njia ya uhalifu. Kwanza kabisa niseme kwamba kwenye kipengele hiki nakiunga mkono asilimia 100 na kipengele hiki kinahusiana na ufilisi wa mali ya mtuhumiwa anayepelelezwana anapotoroka na pia inasaidia kuondoa utata pale itakapotokea mtuhumiwa anayepelelezwana,

alibeshtakiwa na ambaye hukumu haijatolewa pindi anapofariki Mahakama iweze kutoa amri ya kufilisi mali ya mtuhumiwa huyo. Kwa kufanya hivyo, itasaidia wale ambao wanafanya uhalifu wasiendelee na vitendo vyao kwani imekuwa kama ni tabia watu wanaofanya uhalifu wanapata sifa na wamekuwa wanapata mapato makubwa kutokana na vitendo hivi viovu.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, najua wenzangu wengi wamekuwa wakitetea haki za Kikatiba lakini tunatambua Ibara ya 24 ya Katiba inayotoa haki ya kumiliki mali, Ibara hii haiwezi kuruhusu haki ya kumiliki mali ambayo si halali. Haiwezekani mtuhumiwa leo hii ameniibia mimi gari, akaondoka na gari langu, ikatokea shitaka linaendelea Mahakamani, mimi ndio mwathirika, akatokea mshtakiwa yule akafariki, kweli nione mke wake au familia yake inaendelea kutanua na gari langu mimi ambalo nililichuma kwa jasho langu? Hiyo ndiyo mantiki ya kifungu hiki. Kwa hiyo, niwashawishi Wabunge wenzangu kwa kweli sehemu hii, najua mtapinga lakini sehemu hii na tutahukumikiwa kwa kweli kwa kupitisha kitu ambacho hakiko sahihi, Katiba haiwezi kukumbatia uhalifu hata siku moja. Haiwezekani ukakaa na mali ambayo hukupata kihalali na tutakuwa tunazidi kufuga mafisadi na wote hapa mmekuwa mkipigia kelele ufisadi leo hii Serikali imeleta mapendekezo basi walau kushughulikia mali zile ambazo zimepatikana isivyo halali, haiwezekani! Kwa hiyo, naomba jamani kwenye hili lipite kama lilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipotekeleza mfumo huu, wahalifu wataendelea kuwa tishio katika jamii, lakini wahalifu wataendelea kuwa tishio katika maendeleo ya uchumi wa Taifa letu na dhana itazidi kujengeka kwamba uhalifu ndiyo unaolipa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuliona hili Tanzania si pekee kwa kuwa na kitu kama hiki, hata hivi sasa mali za watu waliofanya makosa ya jinai zinaweza zikafilisiwa isipokuwa Sheria ilikuwa na upungufu, ilikuwa haijaainisha inapotokea mtuhumiwa huyo amefariki kabla shitaka halijafika mwisho, mali ile inafanywaje? Kwa kweli na mikataba mbalimbali ya kimataifa ililiona hili, Tanzania hatupo peke yetu, Uingereza wanafanya hivi, Zambia wanafanya hivi, Kenya wanafanya hivi na Namibia pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hata katika vifungu vyetu vya *Criminal Procedure Act*, kifungu cha 351 na kifungu cha 352 vya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai vinaipa mamlaka Mahakama kufilisi mali iliyotumika katika kutenda makosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa ufilisi wa mali iliyopatikana kwa uhalifu huwa unaanza kwa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupeleka maombi katika Mahakama kwamba nahitaji kufilisi mali ya mtuhumiwa ambayo ilipatikana kwa makosa ya jinai...

(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa kama nilivyosema mwanzo tungekuwa na wachangiaji watatu wa mwanzo na sasa tumsikilize mchangiaji wa tatu baada ya hapo tutamsikiliza *Chief Whip* wa Serikali kabla sijatoa mwongozo wangu kuhusu ombi lililokuwa limetolewa. Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa!

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Hoja iliyo mbele yetu ni ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali. Jambo la kwanza katika hoja hii ni kwamba kuna tofauti katika uwasilishaji; Mwanasheria Mkuu alipozitaja Sheria tunazotaka kuzifanyia marekebisho ni 17 na Kamati imesema ni 16. Sheria moja ile ya Bodi ya Korosho mpaka ifanyiwe marekebisho, kwa hiyo, nina wasiwasi ni ipi sheria nyingine iliyoingia wakati sasa kuna tofauti baina ya Mwanasheria Mkuu na Kamati, 17 au 16? Muswada huu una Sheria 16 au 17? Mimi naungana kabisa na Wabunge wenzangu kuhusu suala la Bodi ya Mikopo liahirishwe kwa sababu ni chafu. Hatuwezi kutunga au kukubali marekebisho ya sheria ambayo ina makosa mengi na italeti ubaguzi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huohuo ikiwa sheria tunazozijadili hapa ni nyingi, zimo nyingine ambazo zinahitaji tuzirekebishe na zina manufaa kwetu na Taifa, nisingetumia muda huu kusema tuahirishe mjadala wote wakati ni sheria nyingi na tuna uwezo wa kukizataa vifungu hadi vifungu zile ambazo hazifai

na zinazofaa tukaweza kuutumia muda wetu huu na tukaendelea na mjadala na tunaruhusiwa kupeleka *schedule of amendments*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msimamo huo, naomba uniruhusu kabla sijaendelea kwa kutumia Kanuni hiyohiyo na mimi natoa hoja kwamba, tuendelee na mjadala na tuweze kuzipitisha sheria zinazokubalika na zile ambazo hazitufai tuziache na ziondolewe. Naomba Waheshimiwa Wabunge tuwe makini, tutumie muda wetu huu. Naomba kutoa hoja na naomba mniunge mkono kwamba, tuendelee na mjadala kwa sheria nyingine na tuzikatae ambazo hazifai.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

MBUNGE FULANI: Hoja iliishatolewa.

MBUNGE FULANI: Tupige kura! Kura zihesabiwe!

KUHUSU UTARATIBU

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zitto unatakiwa kusimama tu usiwashe *microphone* kwanza mpaka nikuruhusu.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Sawa, naomba radhi!

NAIBU SPIKA: Ee, endelea!

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza iliyotolewa kwa mujibu wa Kanuni zetu hairuhusiwi kufanyiwa *ammendments*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi masharti ya Kanuni yanakutaka utuletee hoja hiyo tuiamue mara moja. Kwa hiyo, naomba hoja ambayo Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ameitoa uilete tuiamue na ndiyo baadaye uweze kutoa maelekezo yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa *Chief Whip*, halafu AG, kisha tutaendelea. Nilikuwa nimeahidi kukupa nafasi *Chief Whip*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Vilevile nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao tayari wameishajadili hoja hii ya *Miscellaneous Ammendments*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa suala la mikopo ya wanafunzi ni jambo nyeti, jambo muhimu na ni jambo ambalo linataka umakini wetu sisi Wabunge wote kwa sababu suala la elimu ya watoto wetu ni la uhai wa Taifa letu. Ni kweli vilevile kwamba, pamoja na unyeti wake pengine suala hili linahitaji mjadala zaidi, lakini *Miscellaneous Ammendments* si kwa sheria moja tu, ni sheria nyingi ambazo zinahusika katika mabadiliko hayo. Kwa hivyo, ni kweli kabisa inawezekana kabisa tukasema suala hili la mikopo ya wanafunzi tulipe muda zaidi na kwa sababu ya unyeti na umuhimu wake, Kamati husika nayo inapaswa kuliangalia lakini vilevile ni kweli kwamba, sheria hizi nyingine ambazo zinahitaji kufanyiwa mabadiliko ni muhimu. Kwa hiyo, naomba kama alivyopendekeza Mheshimiwa Eng. Habib Mnyaa na ambavyo mimi mwenyewe naamini, tuendelee kujadili maeneo mengine ya mabadiliko haya ya Sheria hizi ambazo zimeletwa na *Attorney General (AG)*, hili la mikopo ya wanafunzi tukubali kwamba tulipe muda ili tuliangalie kwa umakini wake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, *Miscellaneous Ammendments* inapelekwa kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kama jambo ni muhimu vilevile inawezekana kupelekwa kwenye Kamati husika kama

hili suala la mikopo kwa wanafunzi wetu. Lakini tulifikiri mabadiliko haya yanayoletwa ni kwa ajili ya kuboresha hali tete ambayo imekuwepo, tukafikiria kwamba, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilitosheleza mjadala ule lakini kutokana na maoni yenu inaonekana kwamba, suala hili linahitaji muda zaidi. Serikali ikubali hili tulirudishe, tuliangalie upya ili tuboreshe hali halisi ya mikopo ya wanafunzi wetu lakini mabadiliko mengine yaendeleo kujadiliwa. Nitashukuru sana kama Waheshimiwa Wabunge watalisikia hili ili kwa manufaa ya Bunge letu na kwa manufaa ya sheria zile zingine ambazo ni muhimu ambazo hazina utata wowote ziendeleo kujadiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja na wengine nao waniunge mkono. Simameni bwana Mawaziri! (Kicheko)

(Hapa kulikuwa na minong'ono miongoni mwa Wabunge wakionesha kupinga hoja hiyo)

MBUNGE FULANI: Tuamue hoja ya kwanza.

KUHUSU UTARATIBU

MBUNGE FULANI: Kuhusu utaratibu!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki!

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu!

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa ni wakati wa AG halafu tutaendelea na utaratibu. Tutaendelea, nitakupa nafasi Mheshimiwa Tundu Lissu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali sio kama mtoa hoja. Nilivyosikiliza kwa makini mtoa hoja, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ametumia Kanuni ya 69. Pingamizi lake Mheshimiwa Dkt. Ndugulile lilikuwa katika sehemu mbili kama nimemsikia vizuri. Kwanza, ni hili ambalo Mheshimiwa Waziri wa Nchi ambaye sasa ndiye *Chief Whip* amelizungumzia kuhusu Bodi ya Mikopo. Mimi nakubaliana na Waziri wa Nchi, kama Waheshimiwa Wabunge nyie ndio mnatunga sheria, sisi tunaleta mapendekezo tu, hatuwezi kuwalazimisha kutunga sheria kwa sababu upo upepo unapita ndani na nje ya Bunge na hatuwezi kudharau upepo huo. Mamlaka ya kutunga sheria ni mamlaka ya Bunge. Kwa hiyo, kama anavyosema Waziri wa Nchi, tunaweza kuliondoa hilo la Bodi ya Mikopo. Tumekaa, tumefikiri, tukaona mapendekezo haya yanatufaa. Sasa kwa sababu hiyo ni hoja ambayo iko Bungeni, mimi nasema tu kwamba, muamue.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo Mheshimiwa Ndugulile amelizungumzia, mimi nadhani kuna tofauti kati ya watu wa kawaida na Waheshimiwa Wabunge.

WABUNGE FULANI: Aahh!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Ninasema hivyo nikifahamu wajibu wa Wabunge katika nchi kama viongozi. Kwa hiyo, mniache nizungumze.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili alilozungumza ni kuhusu Sheria ya *Traffic* kuweka *points* na akasema kwamba, kwa sababu na nyie ni madereva ni hatari. Mambo mawili lakini mambo mengine haya kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Nchi, tunaweza kuendelea kuyajadili hayo mengine lakini ninyi ndio mnatunga sheria, mimi napendekeza tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, narudia kusema kwamba, mimi bado sijafukuzwa Ujaji. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, huu ni mhimili muhimu sana. Huu mhimili ni muhimu sana lakini sisi kwa kauli zetu, kwa tabia zetu, kwa majibu yetu tunaweza kuuharibu Mhimili huu mzuri. Kwa hiyo, kama hatutaheshimu Kiti cha Spika, kwa kweli nimekaa katika kazi ya Ujaji sijawahi kuona hivyo Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani unaweza kutoa maamuzi. Unaruhusiwa na Kanuni na sisi tutaheshimu maamuzi yote ambayo utakuwa umeyatoa.

NAIBU SPIKA: Naomba wa mwisho katika suala hili awe Mheshimiwa Tundu Lissu.

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nizungumze lugha ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile inahusu kuahirishwa kwa mjadala huu. Hoja inayotakiwa kuahirishwa ni hoja ya Marekebicho ya Sheria Mbalimbali na hiyo ndiyo hoja pekee iliyoko katika mjadala. *(Makofi)*

MHE. KABWE Z. ZITTO: Ndiyo, hamna hoja nyingine. *(Makofi)*

MHE. TUNDU A.M. LISSU: Hiyo ndiyo hoja pekee iliyoko katika mjadala. Sasa kuna mambo mawili; jambo la kwanza kama kwa busara zako Mheshimiwa Naibu Spika unaamini kwamba, hoja hiyo ukiikubali itavuruga utaratibu wa kuendesha vikao vya Bunge utaikataa. Pili, kama hoja unaona ina mashiko unatakiwa uwaulize Waheshimiwa Wabunge wanaikubali au la, ili waitolee maamuzi. Hakuna namna nyingine kwa mujibu wa Kanuni zetu. Hakuna uwezekano wa kuanza kuikata vipande vipande. Sheria hii tuiondoe, sheria ile ibaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja inapoondolewa, inaondolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 90, inaondoka yote. Kwa mujibu wa Kanuni ya 69(4) hakuna uwezekano wa kui-*ammend* hoja hiyo. Kanuni inasema, Mbunge yeyote hataruhusiwa kutoa hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja iliyotolewa kwa mujibu wa Kanuni hii. Kwa hiyo, hii habari ya kwamba tuondoe Sheria ya Bodi ya Mikopo, tuendelee na mengine ni hoja ya watu wanaotaka kuvuruga Kanuni za Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba utoe maamuzi *either* tuendelee na mjadala kama unaona kwamba hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile haina maana au vinginevyo Wabunge waamue.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge...

(Hapa kulikuwa na minong'ono kutoka kwa Wabunge)

NAIBU SPIKA: Ikiwa zamu yangu hapa inakuwa taabu, inakuwaje? *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tumesikiliza pande zote, tumesikiliza hoja zote, hoja zote ni nzito na sasa turudi kwenye Mwongozo wetu. Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ametumia Kanuni ya 69(1) na ili twende pamoja naomba niirudie kuisoma, inasema:-

"Mbunge anayependa mjadala unaoendelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye anaweza kutoa hoja kwamba mjadala sasa uahirishwe na atataja mjadala huo uahirishwe hadi wakati gani pia atalazimika kutoa sababu kwa nini anataka mjadala uahirishwe."

Mheshimiwa Dokta Faustine Ndugulile aliungwa mkono sana ndani ya Bunge na ameeleza sababu za mjadala kuahirishwa na ameeleza uahirishwe hadi kikao kijacho. Kilichopo hapa ni juu ya hoja,

hoja iliyo mbele yangu na mbele yetu sote ni hoja moja, kwa hiyo, kwa namna yoyote ile hatuwezi kuigawa. (Makofi)

Kwa hiyo, kifungu cha pili yake kinanitaka mimi niamue lakini mimi nawaomba ninyi muamue kwa kuwahoji. Sasa tusikilizane vizuri maana yake wakati mwingine inakuwa taabu, mnisaidie na Makatibu tusikilize vizuri.

(Hapa Waheshimiwa Wabunge walihojiwa kuhusu hoja ya Mhe. Dkt. Faustine E. Ndugulile na kura kuhisiwa kufungana)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kura zihesabiwe.

NAIBU SPIKA: Tunarudia kwa mara ya mwisho ili tuone ipi iko clear.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Hoja ya Mheshimiwa Dkt. Faustine E. Ndugulile ilishinda)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, hoja hii inaahirishwa hadi kikao kijacho cha Bunge. (Makofi)

(Muswada wa Sheria ya Marekebisha Mbalimbali wa Mwaka 2011 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No. 2 Act, 2011) Umeahirishwa hadi Kikao cha Bunge cha Mwezi Aprili, 2012)

NAIBU SPIKA: Nawakumbusha Wabunge wa CCM kikao katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Baada ya maneno hayo, naomba sasa kuwashukuru sana kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya kwa siku ya leo na kwa jinsi hiyo naahirisha kikao hiki hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.00 usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumamosi,
Tarehe 3 Februari, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*